ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tisa – Tarehe 20 Mei, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa marekebisho ya Kanuni zetu za Baraza la Wawakilishi, tulizofanya mwishoni mwa 2016. Kanuni ya 40(4) inahitaji maswali ya nyongeza yanayojibiwa kwa maandishi yawasilishwe mbele ya Baraza kupitia Taarifa ya Spika. Madhumuni ya Kanuni hii ni kuwawezesha wananchi kufahamu majibu na maswali hayo yanayoulizwa kwa niaba ya wananchi wanaowakilishwa kwenye chombo hiki.

Waheshimiwa Wajumbe katika Kikao cha Baraza cha Tarehe 10 Mei, 2017 Mhe. Hassan Khamis Hafidh aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na kuahidiwa kujibiwa kwa maandishi. Katika kutimiza masharti ya Kanuni hiyo ya 40(4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016 Wizara hiyo imeleta majibu kama Waziri wa Wizara hiyo alivyoahidi. Waheshimiwa Wajumbe napenda kuwasomea majibu hayo kwenu Waheshimiwa Wajumbe na kwa wananchi wote kwa jumla.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh alitaka kujua ni kiasi gani cha fedha kimelipwa kwa Kampuni iliyoleta dawa ya kuulia magugu. Na majibu wa Wizara hii kama ifuatavyo:

Hakuna malipo ya fedha yaliyofanyika kwa Kampuni hiyo, aidha Mhe. Hassan Khamis Hafidh, alitaka kujua Kampuni iliyoleta dawa hiyo imeshalipwa fedha za manunuzi na majibu wa Wizara ni kama ifuatavyo:-

Hakuna malipo yoyote yaliyofanyika aidha, Mhe. Hassan Khamis Hafidh alitaka kujua zimesharudishwa Serikali na kama hazijarudishwa ni siku gani fedha hizo zitarudishwa na majibu ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

Kwa vile hakuna fedha iliyolipwa kwa manunuzi haya, hivyo hakuna fedha zilizorudishwa kwa sababu Serikali haikulipa fedha hizo.

Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuruni sana.*(Makofi)*

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Bismillahi Rahman Rahim, Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Hati Mezani kwa Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2017/2018.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Suleiman Ali:(Mwenyekiti wa Kamati Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii) Mhe. Mwenyekiti, naomba kuweka Hati Mezani Hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kuhusu Hotuba ya Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha katika Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia, kufika siku ya leo tukiwa wenye afya njema, umoja, bashasha na furaha. Aidha, tunamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze ili tuweze kujadili mambo muhimu ya maendeleo ya Taifa letu na kutekeleza kazi ya kuwatumikia wananchi katika bajeti hii kwa hekima, busara uadilifu na mafanikio ya ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati ili lipokee, lijadili na hatimaye likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo naomba nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la

Mapinduzi, Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake bora wenye busara na hekima ambao umeleta maendeleo makubwa kwa wananchi wa Zanzibar kwa kipindi chote cha uongozi wake.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo napenda kumpongeza tena Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein kwa kutimiza ahadi yake aliyoitoa katika kipindi cha kampeni ya Uchaguzi Mkuu wa 2015 kwa kuongeza maslahi ya wafanyakazi wa kima cha chini kwa asilimia zote 100 kutoka shilingi 150,000 hadi shilingi 300,000. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema ili aendelee kulitumikia Taifa letu na wananchi wa Zanzibar kwa maendeleo ya kizazi cha sasa na baadae. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa juhudi zake kubwa za kumsaidia na kumshauri vyema Rais wa Zanzibar katika kutekeleza majukumu yake ya kuiongoza nchi na kuleta manufaa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kukushukuru wewe binafsi na wasaidizi wako wote wakiwemo Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wenzio wa Baraza, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Maofisa na wafanyakazi wote wa Baraza kwa kazi nzuri za kuliendeleza Baraza hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kumpongeza kwa dhati Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi, Mhe. Ali Suleiman Ali tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu amjaalie uwezo, hekima na busara katika kuiongoza vyema Kamati yetu. Aidha, naomba kuwapongeza wajumbe wote wa Kamati yetu ambao kwa umoja wao hutusaidia kwa kiasi kikubwa katika kutoa miongozo na ushauri juu ya kutatua changamoto za Wizara yangu kwa lengo la kufikia malengo iliyojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kulijulisha rasmi Baraza lako Tukufu kwamba kuanzia mwaka huu wa fedha 2017/2018, Chuo cha Maendeleo ya Utalii kitaondoka katika Taasisi za Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na kwa sasa kimeshaunganishwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) kwa lengo la kukipa hadhi zaidi na kukipandisha daraja ili kiweze kutoa Shahada ya Kwanza ya Utalii na hatimae kutoa Shahada nyengine za juu. Napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake huo katika kuendeleza Sekta ya Utalii nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo imeundwa na sekta kuu nne ambazo ni Sekta ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo zilizo chini ya taasisi 15 kama zifuatazo:-

i. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
ii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
iii. Ofisi Kuu Pemba
iv. Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC)
v. Idara ya Habari Maelezo
vi. Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS)
vii. Chuo cha Uandishi wa Habari
viii. Tume ya Utangazaji
ix. Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX)
x. Kamisheni ya Utalii
xi. Idara ya Utamaduni na Michezo
xii. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale
xiii. Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA)
xiv. Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU)
xv. Baraza la Taifa la Michezo (BTMZ)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa niruhusu kutoa maelezo kuhusu bajeti ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2017/2018. Katika maelezo hayo nitatoa uchambuzi wa utekelezaji wa programu tulizoahidi kutekeleza katika mwaka wa fedha 2016/2017.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ilikadiria kupata shilingi 16,281,900,000/= kwa ajili ya kutekeleza programu kuu 5 na miradi ya maendeleo ya Wizara. Kati ya hizo shilingi 9,684,400,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 6,597,500,000/= kwa kazi za maendeleo. Katika fedha za miradi ya maendeleo ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikadiriwa kutoa shilingi 1,000,000,000/= kati ya hizo shilingi 600,000,000/= ni kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Maabara ya Utalii na shilingi. 400,000,000/= kwa ajili ya mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha *Mao-Tse-Tung Stadium* ikiwa ni mchango kutoka Serikalini. Aidha, shilingi 5,597,500,000/= ni mchango kutoka Serikali ya Jamuhuri ya Watu wa China. Kwa upande wa mapato Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 2,547,268,000/= zinazokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi

2,010,000,000/= zinazokusanywa na kutumiwa moja kwa moja na Taasisi husika.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi jumla ya shilingi 7,306,440,612/= zilipatikana kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 75 ya lengo la shilingi 9,684,400,000/=. Aidha, Wizara ilikusanya shilingi 2,306,911,046/= sawa na asilimia 91 zilizoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ikilinganishwa na lengo la shilingi 2,547,268,999/=. Vile vile, shilingi 1,430,814,073/= sawa na asilimia 71 ambazo zimekusanywa na kutumiwa na Taasisi za Wizara ikilinganishwa la lengo la shilingi 2,010,000,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mishahara Idara zilizomo ndani ya Wizara yangu pamoja na Kamisheni ya Utalii zimepatiwa jumla shilingi 2,440,235,860/= sawa na asilimia 74 ya lengo la shilingi 3,301,000,000/=. Taasisi zinazopokea ruzuku zilipata jumla ya shilingi 2,030,782,700/= ikiwa ni malipo ya mishahara ambapo ni sawa na asilimia 79 ya lengo la shilingi 2,558,600,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi mengine jumla ya shilingi 1,669,164,242/= zilipatikana kwa taasisi zilizomo ndani ya Wizara sawa na asilimia 69 ya lengo la shilingi 2,424,800,000/=. Vile vile, kwa taasisi zinazopata ruzuku zilipata jumla ya shilingi 1,166,257,710/= sawa na asilimia 83 ya lengo la shilingi 1,400,000,000/=

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za maendeleo zinazotokana na mchango wa Serikali jumla ya shilingi 689,535,000/= zimeshapatikana sawa na asilimia 69 ya lengo la shilingi 1,000,000,000/=. Aidha, kwa upande wa msaada wa ujenzi wa uwanja wa *Mao-Tse-Tung* kutoka kwa ndugu zetu wa Jamuhuri ya watu wa China wenye jumla ya shilingi 5,597,500,000/= Wizara yangu bado haijapata takwimu halisi ya fedha ambazo zimetumika mpaka sasa lakini ujenzi wa uwanja huo umeshaanza na unaendelea vizuri sana. Kiambatisho namba 1 A hadi 1C kinaonesha taarifa hizo.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha huo nilioutaja Wizara imefanikiwa kutekeleza miradi ifuatayo:-

1. Programu ya Pamoja ya Kuimarisha na Kuendeleza Sekta ya Utalii:

Mhe. Mwenyekiti, sekta ya utalii ni moja kati ya nyenzo zinazokuza uchumi wa Taifa letu. Katika kuimarisha sekta hii, Serikali kwa kuhusisha wadau mbali mbali waliibua maeneo sita makuu ambayo yalihitaji kuimarishwa ili kubadilisha hali ya utalii na kufikia utalii wa daraja la juu kama inavyoelezwa katika Sera ya Utalii na Mipango Mikuu ya Serikali. Maeneo makuu sita ni bidhaa za utalii na huduma, kuimarisha harakati za utangazaji wa Sekta ya Utalii, kuongeza ulinzi na usalama kwa watalii na wawekezaji pamoja na mali zao, kuimarisha miundombinu ya utalii, kuimarisha mazingira na faida za utalii kwa jamii na mwisho kuimarisha utawala katika Sekta ya Utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016 Wizara yangu iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 600,000,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Maabara ya Utalii lakini hadi kufikia Machi 2017 programu hii imeingiziwa jumla ya Shilingi 315,750,000/= za utekelezaji sawa na asilimia 53.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha maeneo yaliyoainishwa katika programu ya kuendeleza utalii yanatekelezwa kwa ufanisi, Wizara imelipia gharama za mabanda ya maonesho ya Zanzibar yaliyokuwepo Dubai na Ujerumani kwa lengo la kutoa fursa kwa Zanzibar kuendelea kutangaza bidhaa na huduma ya utalii za Zanzibar ili kuvutia watalii wote nje ya nchi kutembelea na kuongeza idadi ya watalii.

Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Mao-Tse-Tung

Mhe. Mwenyekiti, hatua za ujenzi wa kiwanja cha *Mao-Tse-Tung* umeshaanza kwa vizuri kwa kushirikiana na mkandarasi wa kampuni ya *Zhengtai Group Co, Ltd* kutoka Jamhuri ya Watu wa China. Shughuli ambazo zimeshatekelezwa kwa sasa ni uwekaji wa umeme katika eneo la Ujenzi wa Uwanja wa *Mao-Tse-Tung*, usafishaji wa eneo kwa ajili ya hatua za ujenzi. Aidha, Wizara imejenga nyumba za muda wa wakandarasi katika eneo la Matumbaku na kuzungushia uzio wa bati kwa ajili ya uhifadhi wa vifaa vya ujenzi na uwekaji wa miundombinu ya maji kwa kuchimba kisima katika eneo la Madema na kusambaza mabomba katika eneo la uwanja na kwenye makazi ya wakandarasi katika eneo la Matumbaku. Vile vile, Wizara imegharamia utoaji wa vifaa vyote vilivyokwisha ingia vya ujenzi kutoka China.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 mradi huu ulipangiwa jumla ya shilingi 5,597,500,000/= ikiwa ni mchango kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na jumla ya 400,000,000/= mchango kutoka Serikali. Hadi

kufikia Machi 2017 asilimia 93 imetekelezwa ikiwa ni sawa shilingi 373,785,000/= elfu. Kiambatanisho namba 1 kinaonesha hatua hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ilipangiwa kutekeleza programu kuu 5 kama ifuatavyo:-

1. Programu ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji.
2. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Utalii na Michezo.
3. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii.
4. Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii.
5. Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

PROGRAMU YA MAENDELEO YA HABARI NA UTANGAZAJI

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la programu hii ni kuwa na jamii iliyoimarika katika maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kupitia habari.

Programu hii inaundwa na programu ndogo 2 nazo ni Upatikanaji na Usambazaji wa Habari na Usimamizi wa vyombo vya Habari na Utangazaji.

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari inatekelezwa na Taasisi na Idara tofauti nazo ni, Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS), Chuo cha Uandishi wa Habari na Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX).

Mhe. Mwenyekiti, huduma ambazo zinatolewa katika programu hii ndogo ni urushaji wa vipindi kupitia Televisheni na Redio, utoaji wa taarifa, picha, makala, filamu na sinema, uchapishaji wa magazeti, utoaji wa mafunzo ya habari na mawasiliano na usambazaji wa maudhui ya utangazaji.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji la Zanzibar limefanikiwa kurusha hewani vipindi vya *ZBC TV* vya ndani 6,946 vikiwemo vya unyanyasaji wa kijinsia, jee wajua, rushwa, ijue sheria, udhalilishaji wa watoto, *ZBC Doctor* na kujikinga na maradhi ya kipindupindu. Aidha, vipindi vya nje 3,936 vimerushwa. Vile vile, Shirika limerusha vipindi vya *ZBC Radio* 13,991 vikiwemo paukwa pakawa, kutoka vijijini, jielimishe, sauti ya watoto, adhuhuri njema na Qur–an tukufu. Pia, Shirika limerusha hewani jumla ya matangazo 15,416 kupitia *ZBC TV* na *Radio*.

Mhe. Mwenyekiti, matangazo 50 ya moja kwa moja yakiwemo ya maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, uzinduzi wa hospitali ya Abdalla Mzee Pemba, Mkutano Mkuu wa CCM Dodoma, Watoto Mapinduzi Cup, Sherehe za kutimia mwaka mmoja kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi baada ya kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu, tulioshinda kwa kishindo kikubwa sana matangazo ya vikao vya Baraza la Wawakilishi pamoja na makongamano na mijadala inayowahusu wananchi katika kuimarisha uchumi, kulinda na kudumisha amani na utulivu wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha wananchi wanapata habari za uhakika na kwa wakati, Idara ya Habari Maelezo imesambaza taarifa 408 zinazohusu udhalilishaji wa watoto na wanawake, umuhimu wa chanjo ya vitamin A, uzazi salama kwa afya ya mama na mtoto na mambo ya kijamii na kiuchumi kwa vyombo vya habari mbali mbali vikiwemo ZBC, Zanzibar Leo, Chuchu FM, Redio Jamii Micheweni, Al – Noor, Hits FM na mitandao ya kijamii ikiwemo Michuzi Blog. Mikutano ya waandishi wa habari inayohusiana na mafanikio ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ pia imesimamiwa. Aidha, mikutano mengine iliyohusu maadili ya vyombo vya habari na uharibifu wa mashamba ya mikarafuu Pemba iliratibiwa vizuri sana. Pia, Idara imechapisha picha za matukio muhimu na kuziweka katika mabango ya Idara yaliyopo katika maeneo tofauti ya mikusanyiko ya watu ndani ya mji wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, Idara imeweza kusajili kijarida cha SUMAIT University Journal, SHAHIDI na kusambaza picha za viongozi 1,804 zikiwemo za viongozi wakuu, Baraza la Mawaziri na viongozi wastaafu. Aidha, imechapisha na kusambaza vitambulisho vya waandishi wa Habari 161 wa ndani na nje ya nchi. Vile vile, kwa kutumia gari la sinema Idara imeweza kufika vijijini kwa kuonesha filamu mbali mbali zikiwemo za kilimo cha mboga, upandaji wa mikarafuu, elimu ya afya na ziara za Mhe. Rais wa Zanzibar katika Mikoa tafauti ya Unguja na Pemba. Miongoni mwa vijiji vilivyooneshwa filamu hizo ni Fujoni, Kinyasini, Donge Mchangani, Umbuji, Ndijani, Machui, Mtende, Makunduchi, Muungoni, Zingwezingwe, Bandamaji na Kitope kwa upande wa Unguja bila ya Uria. Vile vile kwa upande wa Pemba ni Chonga, Pujini, Kungeni, Kangani, Mtambile, Kiwani, Makombeni, Ziwani, Mchanga Mdogo, Mzambarauni, Selemu na Gando.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS) limefanikiwa kuchapisha Magazeti ya *Zanzibar Leo* na kuyasambaza katika

Mikoa ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa lengo la kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha jamii juu ya masuala mbali mbali ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Jumla ya nakala 810,000 kwa gazeti la kila siku la *Zanzibar Leo* na matangazo 563 yamechapishwa. Aidha, Shirika la Magazeti ya Serikali limefanikiwa kuweka gazeti la *Zanzibar leo* kwenye tovuti yake ili kutoa fursa kwa wasomaji wa ndani na nje kupata habari zinazohusu nchi yetu katika masuala ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika pamoja na kazi zake za msingi linakusudia mwaka huu kuongeza wigo wa usambazaji wa magazeti katika sehemu mbali mbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kueneza Sera za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kukuza na kusambaza lugha ya Kiswahili katika Ukanda wa Afrika ya Mashariki. Pia, Shirika linakusudia kushirikiana na wadau mbali mbali kuandaa matoleo maalum ya Jukwaa la Fursa za Uwekezaji na Biashara ili kutoa fursa kwa Mikoa na wadau kutumia fursa za kibiashara na uwekezaji Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS), limefanikiwa kuhamia katika jengo la kudumu katika eneo la makutano ya barabara ya Kikwajuni na Maisara - Zanzibar baada ya kufanyiwa matengenezo makubwa yaliyosimamiwa na Wakala wa Majengo ya Serikali ambapo jumla shilingi 135,000,000/= zimetumika kwa ukarabati mkubwa wa jengo. Aidha, shilingi 24,000,000/= zimetumika kwa ujenzi wa ukuta na kujaza kifusi eneo linalozunguka jengo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa madeni, Shirika hadi Disemba 2016, lilikuwa likidaiwa shilingi 400,801,780/= na Shirika la Uchapaji Tanzania (TSN) zikiwa ni deni la uchapaji wa magazeti ya *Zanzibar Leo, Zanzibar Leo Jumapili* na *Zaspoti.* Hadi kufikia April, 2017 Shirika la Magazeti ya Serikali limefanikiwa kuilipa TSN jumla ya shilingi 192,000,000/= na kubakisha deni la shilingi 335,748,544/= ambalo limetokana na deni la mpaka Desemba 2016 huku tunakoendelea tuko vizuri. Pamoja na madeni yaliongezeka mwezi wa Januari mpaka April kwa TSN. Pia, Shirika la Magazeti ya Serikali limelipa shilingi 26,655,000/= ikiwa ni sehemu ya punguzo la deni kwa wadai mbali mbali wa shirika.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, hadi Januari, 2017 limefanikiwa kulipwa deni la shilingi 161,155,406/= kati ya shilingi 340,318,388/= zinazodai kwa muda mrefu Wizara pamoja na Taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ). Kwa sasa deni lililosalia ni shilingi 179,162,982/=.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Uandishi wa Habari kimehamia katika jengo lake jipya liliopo Kilimani ambapo kwa sasa nafasi za wanafunzi za kujiunga na chuo zimeongezeka na chuo kimeongeza fani za masomo zitakazosomeshwa katika chuo hicho. Aidha, chuo kimepitia na kufanya marekebisho ya mitaala kwa kozi zilizokuwepo ili kuweza kukidhi mahitaji ya soko la habari na mawasiliano. Pia, chuo kimeandaa muundo wa utumishi na muundo wa taasisi ambao umewasilishwa Kamisheni ya Utumishi kwa hatua za kuimarishwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa masomo 2016/2017 chuo kimeweza kudahili jumla ya wanafunzi 248 katika fani mbali mbali zinazotolewa chuoni hapo na kuendeleza mafunzo kwa vitendo kwa kufanya ziara kwa wanafunzi za kutembelea maeneo ya kihistoria na vijijini pamoja na kutembelea skuli 10 za Unguja na Pemba. Aidha, chuo kimeendelea kufundisha somo la lugha ya Kichina ambapo jumla ya wanafunzi 56 wa Cheti na 43 wa Stashahada wamehitimu masomo na kukabidhiwa vyeti. Pia, jumla ya vitabu rejea 150 na kompyuta 25 zimenunuliwa ambazo zinatumika kwa mafunzo ya wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, Kampuni ya Usambazaji Maudhui imefanya ufuatiliaji katika vituo vyake saba vya Unguja na Pemba navyo ni Masingini, Nungwi, Muyuni, Rahaleo, Bungala, Chake Chake na Kichunjuu kwa lengo la kufanya ukaguzi na kuhakikisha maudhui yanapatikana muda wote matantazo yanaporushwa. Aidha, Kampuni imeunganishwa na mkonga wa taifa kwa ajili ya urushwaji matangazo yake ili yaweze kuwafikia watumiaji kwa uhakika zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Programu ndogo iliidhinishiwa jumla ya shilingi 3,441,652,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2017 imefanikiwa kupata shilingi 2,796,661,021/= sawa na asilimia 81 na kutakiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,535,000,000/= hadi kufikia Machi 2017 jumla ya shilingi 1,159,560,314/= zimekusanywa sawa na asilimia 75 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E)

Mhe. Mwenyekiti, Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari na Utangazaji inatekelezwa na Taasisi 2 ambazo ni, Idara ya Habari Maelezo na Tume ya Utangazaji.

Mhe. Mwenyekiti, huduma zinazotolewa katika programu ndogo ni udhibiti na usimamizi wa shughuli za habari na utangazaji kupitia Sera na Sheria za Habari na Utangazaji.

Mhe. Mwenyekiti, katika kufanikisha huduma zake, Idara ya Habari Maelezo imefanikiwa kutoa vibali 10 vya upigaji picha na uchukuaji filamu katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar. Miongoni mwa Kampuni zilizopewa vibali hivyo ni: *Tui, Reizen, Fly Dubai, Royal National Life, Boat Institution, France TV na France 3TV.*

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Utangazaji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imeweza kutoa kanuni ya utoaji leseni za utangazaji. Pia, Tume imefanikiwa kurikodi na kufuatilia matangazo ya redio 19 zilizopatiwa leseni. Aidha, Tume imeandaa na kurusha hewani vipindi 12 vya kuelimisha jamii juu ya teknolojia ya utangazaji wa dijitali kupitia ZBC Redio na ZBC TV.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, programu ndogo iliidhinishiwa jumla ya shilingi 219,144,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2017 imefanikiwa kupata shilingi 151,374,735/= sawa na asilimia 69 na kutakiwa kukusanya jumla ya shilingi 100,000,000/= hadi kufikia Machi 2017 jumla ya shilingi 51,188,000/= zimekusanywa sawa na asilimia 51. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E)

PROGRAMU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa Utamaduni wa Zanzibar unawaendeleza wasanii kiuchumi na kupunguza umasikini pamoja na kuwa na rasilimali watu wenye ujuzi na ustadi wa kukuza utalii nchini na kuifanya michezo kuwa ni sehemu ya kujenga afya na ajira kwa jamii. Programu hii ina programu ndogo 2 ambazo ni uimarishaji wa utamaduni na maeneo ya kihistoria pamoja na uendelezaji wa rasilimali watu katika utalii na ukuzaji wa michezo.

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo ya uimarishaji wa utamaduni na maeneo ya kihistoria imeundwa na taasisi zifuatazo:

- Idara ya Utamaduni na Michezo,
- Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni,
- Baraza la Kiswahili na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale.

Mhe. Mwenyekiti, huduma zinazotolewa na programu ndogo hii ni uendelezaji na ukuzaji wa shughuli za utamaduni kwa wananchi, kurikodi kazi za sanaa kupitia studio ya filamu na muziki, uratibu wa kazi za sanaa na wasanii, ukaguzi wa filamu na sanaa za maonesho, utoaji wa elimu kuhusu matumizi

fasaha ya lugha ya kiswahili, uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya kihistoria pamoja na uelimishaji na ushirikishaji wa jamii katika uhifadhi wa maeneo ya kihistoria na urithi wa utamaduni.

UTEKELEZAJI HALISI

Mheshimiwa Spika, katika uendelezaji na ukuzaji wa shughuli za utamaduni kwa wananchi, matamasha matano yameratibiwa na kufanyika ambayo ni:

- Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari,
- Mwaka Kogwa, Kae,
- Vyakula vya Asili ya Kimakunduchi, Zumari ya zungu,
- Tamasha la Elimu Bila ya Malipo na Tamasha la Washirazi.

Aidha, kikundi kimoja cha Tarabu asilia (Kitara) kimeshiriki Tamasha la Muziki nchini Marekani kuanzia tarehe 30/08/2016 hadi 2/09/2016. Aidha, jumla ya vikundi 16 vimeshiriki matamasha ya ndani vikiwemo kikundi cha wanawake cha mwanandege, kikundi cha ngoma cha Taifa, kikundi cha ngoma ya kilua na kikundi cha Taarab asilia cha *Culture.*

Mhe. Mwenyekiti, katika kuiendeleza na kuimarisha Nyumba ya Sanaa matengenezo ya dari yamefanyika, ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi za uzalishaji vikiwemo kompyuta, mashine ya kukatia mbao, *'tetron roll', 'canvas roll',* kamba na rangi. Aidha, wafanyakazi wa nyumba ya sanaa wamepatiwa mafunzo ya fani ya uchongaji, uchoraji, uchapishaji na utengenezaji wa mazulia ya kamba ya kupangusia miguu. Aidha, jumla ya wanafunzi tisa kati ya hao wanawake wanne na wanaume watano ndio wanaopatiwa mafunzo katika Nyumba ya Sanaa, ambapo wanafunzi sita ni walemavu wa macho.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni limeweza kukusanya taarifa za wasanii wakongwe wa kazi za sanaa nchini. Katika hatua ya mwanzo jumla ya wasanii saba wamehojiwa na kupatikana taarifa zao ambapo taarifa hizo zitahifadhiwa na kutumika kwa maendeleo ya sanaa na wasanii nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza limefanikiwa kuandaa na kutoa mafunzo kwa walimu wakuu na wale wanaofundisha somo la utamaduni na sanaa katika skuli za msingi Unguja na Pemba. Mafunzo hayo yalihusiana na ujengaji wa maadili kwa wanafunzi wa skuli za msingi na namna bora ya kuibua vipaji vya sanaa kwa wanafunzi hao. Mafunzo hayo yalihusisha walimu 50 kutoka Mkoa wa Kaskazini Pemba, 53 Mkoa wa Kusini Unguja na walimu 50 kutoka Mkoa wa

Kaskazini Unguja. Katika mafunzo hayo Baraza lilishirikiana na Idara ya Michezo na Utamaduni kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, Baraza limetoa leseni 68 na vibali 240 kwa kazi za sanaa pamoja na kuwajengea uwezo vikundi vitatu vya sanaa kwa kupatiwa mafunzo yatakayowasaidia kukuza vipaji vyao ili kuzalisha kazi bora za sanaa zikiwemo uandaaji wa filamu, namna ya kuzalisha kazi bora za sanaa za kiasili, michezo ya jukwaani na ubunifu katika ngoma za asili. Vikundi hivyo ni pamoja na kikundi cha taifa cha sanaa ya ngoma, kikundi cha sanaa cha Bweleo na kikundi cha sanaa cha Mchikicho kutoka Nungwi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha mila, silka na desturi za Mzanzibari zinalindwa, zinahifadhiwa na kuendelezwa, jumla ya filamu 102 za sanaa za maonesho zimekaguliwa kati ya hizo filamu tatu zimerejeshwa kwa marekebisho. Aidha, jumla ya maonesho 85 yamekaguliwa na kupatiwa maelekezo kwa kasoro ndogo ndogo kwa marekebisho kabla ya kuruhusiwa kuoneshwa hadharani. Baraza limefanya usajili kwa kuvisajili upya jumla ya vikundi 45 vya sanaa.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya kamati za sanaa za Wilaya 11 za Unguja na Pemba zimezinduliwa na kupewa mafunzo ya namna ya utekelezaji wa majukumu yao kwa kuzingatia Sheria ya Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni. Aidha, vikao vinne vya uandaaji wa kanuni ya Sheria ya Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni vimefanyika. Pia, Baraza limerusha hewani jumla ya vipindi sita kupitia *ZBC Redio, Hits FM, Bahari FM, Chuchu FM, Bomba FM na Furaha Cable.*

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya kazi za sanaa 40 zimerikodiwa kupitia *studio* ya filamu na muziki, zikiwemo ngoma za asili, kizazi kipya, kwaya, kasida, maulidi ya homu na sanaa za maigizo. Pia, Baraza limefanya vikao vya bodi vitatu kwa lengo la kujadili kazi za Baraza na kutoa ushauri na maelekezo ya kitaalamu katika kuhakikisha Baraza linatekeleza shughuli zake kwa ufanisi unaotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) limerusha jumla ya vipindi 43 katika redio na televisheni za Serikali na binafsi ambazo ni Shirika la Utangazaji Zanzibar *(ZBC)*, Shirika la Utangazaji la Taifa *(TBC)*, Zenji FM, Swahiba *FM*, *Coconut FM*, Bomba *FM*, Chuchu *FM* na *Hits FM*, mada mbali mbali ziliwasilishwa na kuchangiwa katika vipindi hivyo zikiwemo Uingiaji holela wa maneno ya Kiswahili na athari zake, Uchambuzi wa Mashairi, Usahihi wa maneno katika Lugha ya Kiswahili, Matumizi fasaha na

sahihi ya maneno kwa waandishi wa habari, Kiswahili bidhaa muhimu katika Utalii na Maendeleo ya Kiswahili ya Miaka 53 ya Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuadhimisha siku ya Kiswahili Zanzibar, Baraza limefanikiwa kutekeleza shughuli mbali mbali zikiwemo kufanya kongamano katika siku ya Kiswahili. Jumla ya washiriki 400 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar walishiriki katika kongamano hilo na kuchangia mada zilizowasilishwa ambazo ni:

Nafasi ya Kazi za Fasihi katika Kukuza na Kupunguza Umasikini Zanzibar na Mwachano na Mikutano ya Kiswahili katika Mwambao wa Afrika ya Mashariki. Baraza pia, limefanya mashindano ya hadithi fupi kwa wanafunzi wa Msingi, Sekondari na Vyuo kwa lengo la kuibua na kukuza vipaji vya utunzi kwa washiriki wa mashindano hayo. Pia, Baraza limetoa mafunzo kwa waandishi wa habari 40 kuhusu matumizi sahihi na fasaha ya Kiswahili kutoka vyombo vya Serikali na binafsi. Mada kuu zilizowasilishwa ni Makosa ya Kiswahili yanayofanywa na vyombo vya habari pamoja na Kiswahili ni nyenzo kuu ya kutoa na kupokea habari.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza limefanya maonesho ya vitabu kwa lengo la kushajiisha jamii kuwa na utamaduni wa kupenda kusoma vitabu. Pia, limeshiriki katika maonesho ya wajasiriamali yaliyofanyika katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi la Zamani kwa lengo la kutangaza na kuuza vitabu kwa jamii. Aidha, Baraza limeshiriki makongamano mbali mbali yakiwemo Kongamano la Chama cha Wanafunzi wa Kiswahili Afrika ya Mashariki (CHAWAKAMA) lililofanyika katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi la zamani-Kikwajuni na katika Chuo Kikuu cha Sumait Zanzibar, Kongamano la Chama cha Lugha na Fasihi ya Kiswahili Tanzania (CHALUFAKITA) lililofanyika Iringa, Kongamano la Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari na Kongamano la Chama cha Kiswahili Duniani (CHAUKIDU) ambalo lililofanyika Nairobi, Kenya. Katika makongamano hayo Baraza limeshiriki katika uwasilishaji wa makala na mijadala ya taaluma za Kiswahili, kuuza machapisho pamoja na kulitangaza Baraza na kazi zake. Pia, Baraza limeweza kuandaa Jarida la BAKIZA ambalo huhusisha makala za taaluma ya Kiswahili katika isimu na Fasihi.

Mhe. Mwenyekiti, katika uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya kihistoria Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imefanya matengenezo katika maeneo saba ya kihistoria yakiwemo Kidichi, Ujenzi wa vyoo Mangapwani, kibanda cha kuuzia tiketi Dunga, kuweka milango na matengenezo ya madirisha na kuliwekea uzio jengo la kihistoria la Chuini. Aidha, matengenezo ya

Makumbusho ya Pete kwa awamu ya pili yamekamilika kwa uchimbaji wa kisima, kutia milango na madirisha, kuezeka bati, umeme, vyoo na mnara wa maji. Vile vile, Makumbusho ya Viumbe Hai Mnazi Mmoja Idara imeweka sakafu ya zege na kufanya matengenezo ya baraza za kukalia watu pale Ngome Kongwe. Aidha, Idara kwa kushirikiana na taasisi inayoshughulika na uhifadhi wa maeneo ya kihistoria imefanya matengenezo ya ukuta katika eneo la kihistoria la Hamamni yaani *(Hamamni Bath)*.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuyatangaza na kutoa mwamko kwa wananchi ili kuyajua, kuyatembelea na kuyalinda maeneo ya kihistoria. Idara imerikodi jumla ya vipindi 24 vya elimu na kurushwa hewani kupitia *ZBC Redio* na *TV*, *Zanzibar Cable Television*, *Hits FM*, Chuchu *FM*. Bahari *FM* ikiwemo na Mwenge *FM* juu ya historia ya Kuumbi, Matumizi ya zana za mawe, Sanaa ya ufinyazi, Kuundwa Idara ya Makumbusho, Historia ya Mji Mkongwe na maeneo ya kihistoria yaliyomo Mji Mkongwe. Aidha, elimu kuhusu dhana ya utalii kwa wote imetolewa kwa makundi manne kuhusu historia na vivutio vya utalii kwa Masheha 23 wa Wilaya ya Mjini, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi 22, Waandishi wa Habari wanane na Maofisa na wapiganaji 22 wa Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM).

Mhe. Mwenyekiti, Idara imefanya ukaguzi na kukusanya taarifa za awali katika mapango 25 ya kihistoria katika Shehia ya Nyamanzi na Dimani njia kuu, Bambi na Umbuji na baadae kuzifanyia uchambuzi wa kihistoria ili kubaini shughuli zilizokuwa zikifanyika katika sehemu hizo jambo ambalo litapelekea kuibua maeneo mapya ya kihistoria na kuongeza mapato ya Idara. Pia, imeendelea na utafiti wa Akiolojia kwa maeneo matatu ya kihistoria ya Kuumbi na Pete Machaga kwa Unguja uliofanywa na Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam na Pango la Kijijini Makangale Pemba uliofanywa na Chuo Kikuu cha Carlifonia nchini Marekani kwa kushirikiana na wataalamu wa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Makumbusho imepokea jumla ya wageni 33,136 ambao wenyeji ni 2,129, watoto 23, wanafunzi 18,443 na wageni maalumu 186 walitembelea maeneo ya kihistoria na urithi wa utamaduni. Aidha, wageni 12,046 na watoto 309 kutoka nje ya nchi walitembelea maeneo yetu ya kihistoria na urithi wa utamaduni.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,508,943,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2017 imefanikiwa kupata shilingi 1,108,773,205/= na kutakiwa kukusanya jumla ya shilingi 392,268,000/= lakini hadi kufikia Machi 2017

jumla ya shilingi 170,110,202/= zimekusanywa sawa na asilimia 43. (kiambatishi namba 1D na 1E ni muongozo)

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo ya uendelezaji wa utalii na ukuzaji wa michezo inatekelezwa na Taasisi na Idara zifuatazo:

1. Chuo cha Maendeleo ya Utalii,
2. Idara ya Utamaduni na Michezo na
3. Baraza la Taifa la Michezo (BTMZ).

Mhe. Mwenyekiti, huduma zinazotolewa katika programu ndogo hii ni utoaji wa mafunzo ya utalii, ukarimu na ujasiriamali, uratibu na uendelezaji wa shughuli za michezo, uendelezaji wa miundombinu ya michezo na usimamizi wa shughuli za vyama vya michezo kupitia Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, katika kufanikisha huduma zake Chuo cha Maendeleo ya Utalii kimedahili wanafunzi wapya 267 kati ya hao wanawake 118 na wanaume 149 sawa na asilimia 95, ikiwa ni kubwa ongezeko la asilimia 10 ikilinganishwa na mwaka wa masomo 2015/2016. Aidha, chuo kimefanya marekebisho ya mitaala na kupelekea kuongezwa kwa kozi mpya nne na kozi fupi 12 pamoja na wanafunzi kuongezewa vipindi vya mafunzo ya vitendo. Katika kuongeza uelewa kwa wanafunzi, chuo kimeratibu ziara za kimasomo, mazoezi ya vitendo nje ya chuo pamoja na mitihani. Aidha, chuo kimefanya mahafali kwa kuwatunuku vyeti na stashahada wahitimu 177, wa Kizanzibari kati ya yao wanaume 80 na wanawake 97 na kugharamia uchapishaji wa vyeti 196.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo kimewapatia wafanyakazi mafunzo ya muda mrefu, ili kufikia lengo la kuunganishwa na Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) ambapo mfanyakazi mmoja wa kada ya taaluma amepatiwa nafasi ya masomo ya juu kusoma Stashahada ya Pili katika fani ya Utalii na Ukarimu. Vile vile, mfanyakazi mmoja amepatiwa nafasi ya kusoma ngazi ya Shahada ya Kwanza katika fani ya Ununuzi na Ugavi, pia, wafanyakazi wawili wamepatiwa fursa ya kusoma ngazi ya Cheti katika fani ya Ufundi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kukitangaza chuo ndani na nje ya nchi, chuo kimeshiriki katika maonesho yaliyoandaliwa na Chuo cha Karume na kushiriki katika maonesho ya wajasiriamali pamoja na kutangaza shughuli za chuo katika

Jarida la *Tanzania Review* toleo namba 7. Aidha, chuo kimefanya vikao viwili vya Baraza la Chuo, vitatu vya Kamati ya Taaluma na viwili Kamati ya Uendeshaji kwa lengo moja tuu la kuimarisha shughuli za chuo.

Mhe. Mwenyekiti, katika uratibu na uendelezaji wa shughuli za michezo Idara ya Utamaduni na Michezo imesaidia timu ya wabeba vyuma vizito kushiriki katika mashindano nchini Jordan ambapo Makamu wa Pili wa Rais amekwenda kutembea, na walipata nafasi ya tisa wanaume, *Zanzibar Queen* katika mashindano ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika Mashariki na Kati hongereni sana *Zanzibar Queen* kwa kutuwakilisha. Mashindano ambayo yamefanyika nchini Uganda, timu ya watu wenye ulemavu wa kusikia nchini Kenya nao wamefanya mashindano wamepata nafasi ya pili wanaume, mashindano ya 11 ya mchezo wa judo Afrika Mashariki nayo yalifanyika 2017 kwa upande wa Zanzibar wamepata nafasi ya tatu hongereni wanamasubwi. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 3 inaonyesha taarifa hizo).

Mhe. Mwenyekiti, juhudi za kukiimarisha kiwanja cha Amaan kwa kukizungushia ukuta wa matofali zinaendelezwa. Pia, Idara kwa kushirikiana na BTMZ wameweza kufanya matayarisho ya ujenzi wa uwanja wa Kitogani Mkoa wa Kusini Unguja kwa kutia kifusi na udongo wa kuoteshea nyasi za kisasa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa kulitaarifu Baraza lako Tukufu kuwa Shirikisho la Soka la Afrika (CAF) limeridhia kuipa uwanachama wa kudumu Zanzibar, ambapo ombi la uanachama limeridhiwa na Mkutano Mkuu wa CAF uliofanyika Addis Ababa nchini Ethiopia. Zanzibar sasa ni mwanachama wa 55 wa CAF Barani Afrika. Hatua hii ya Zanzibar kupata uanachama wa kudumu wa CAF inapelekea mafanikio yafuatayo:

1. Zanzibar sasa itaweza kushiriki mashindano yanayoandaliwa na CAF katika Mataifa ya Afrika ambayo yanaitwa (AFCON),

2. Vile vile itashiriki fainali za Afrika Wanawake ambayo yanaitwa (AWCON),
3. Vile vile watashiriki katika fainali za Vijana (AFCON U17 na AFCON U 20). Pia, itakuwa na uhalali wa kuhudhuria mikutano mbali mbali sambamba na kupokea na kusimamia kozi mbali mbali na kupata fursa ya kupiga kura katika masuala muhimu ya CAF.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar kufikia kujiunga na uanachama wa kudumu wa CAF kunaashiria wazi kwamba uwezekano mkubwa usioshaka wa kupata

uanachama wa FIFA hali ambayo itapelekea vijana wetu kucheza mashindano ya kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti Baraza la Taifa la Michezo limefanikiwa kuvisaidia vyama 10 vya michezo kushiriki na kuandaa mashindano mbali mbali ya ndani vikiwemo chama cha mpira wa pete mashindano ya Klabu Bingwa ya Zanzibar, Chama cha Judo mashindano ya Zanzibar Judo na chama cha mpira wa wavu mashindano ya Klabu Bingwa ya Mpira wa Wavu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mafunzo Baraza limeweza kutoa mafunzo kwa vyama vitano vya michezo. Mafunzo yenyewe ni mafunzo ya ualimu na uamuzi wa michezo ya Mpira wa Pete, Mpira wa Kikapu, Mpira wa Wavu, Karati, Wanyanyua vitu vizito na pamoja na Kuogelea. Aidha, Baraza limeweza kutoa jezi kwa timu ya Taifa ya Vijana chini ya umri wa miaka 17 na vikombe kwa ajili ya mashindano ya michezo ya Polisi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika kusimamia utekelezaji wa Sheria namba 5 ya Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar ya mwaka 2010, Baraza limesimamia marekebisho ya katiba kwa vyama vinne vya michezo ya Mpira wa Pete, Mpira wa Kikapu, Mpira wa Mikono na Mchezo wa Baskeli.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 653,194,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2017 imefanikiwa kupata shilingi 523,812,615/= sawa na asilimia 80 na kutakiwa kukusanya jumla ya shilingi 530,000,000/= lakini hadi kufikia Machi 2017 jumla ya shilingi 297,930,509/= zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 56. kiambatisho namba 1D na 1E kinaonyesha).

Mhe. Mwenyekiti, katika kufikia zaidi ya nusu niendelee na Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii.

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la programu hii ni kuongeza tija ya Sekta ya Utalii kwa kuongeza ajira kwa jamii, idadi ya watalii na thamani yao. Programu hii inayotekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi ili Zanzibar itambulike zaidi kuwa ni miongoni mwa vivutio bora vya utalii duniani.

Mhe. Mwenyekiti huduma inayotolewa katika programu hii ni kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi yetu.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ya Utalii ilishiriki maonesho ya kimataifa ya utalii, ikiwemo onesho la *International Tourism Borse* (ITB-Ujerumani), *World Travel Market* (WTM-Uingereza), Arabian *Travel Market* (ATM-Dubai) na *International Russian Travel Market* (IRTM-Urusi). Lengo la kushiriki maonesho hayo ni kuitangaza Zanzibar na kuwavutia watalii wengi zaidi kutembelea nchini petu. Vile vile, Kamisheni ya Utalii iliweza kushiriki katika Tamasha la Biashara wakati wa Sherehe za kutimiza miaka 53 ya Mapinduzi. Katika maonesho hayo, Kamisheni ya Utalii ilishirikiana na wadau kutoka Taasisi za Umma na Sekta Binafsi katika kutangaza vivutio vya utalii Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mafanikio ya maonesho hayo ni kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaotembelea Zanzibar. Kwa mujibu wa takwimu zilizokusanywa na Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar imepokea wageni wa kimataifa wapatao 376,242 ambao ni sawa na asilimia 104.5 ya makadirio yaliyopangwa kwa mwaka. Kwa mwaka wa fedha 2016/17 mkazo mkubwa uliwekwa katika kuvutia wageni kutoka masoko mapya ikiwemo Ukraine, Poland, Urusi, China, India na Israel.

Mhe. Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa idadi ya wageni kutoka nchi hizo imeongezeka kwa kasi kubwa kutoka 29,248 mwaka 2015 hadi wageni 56,666 mwaka huu mmoja 2016 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 103.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar imeweza kuwaalika waandishi wa habari wa vyombo tofauti vya kimataifa kwa lengo la kutoa taarifa za vivutio vya Zanzibar katika vyombo vya habari, magazeti na majarida ya masoko husika. Kutokana na ziara hizo Zanzibar imeendelea kuandikwa na majarida tofauti kama vile BizTravel.

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ya Utalii ilifanya misafara nchini Dubai na Morocco ili kuhamasisha watalii kuja kutembelea vivutio vya utalii nchini. Kwenye ziara hizo ujumbe wa Tanzania ulifanya mazungumzo na taasisi mbali mbali za kiutalii juu ya mambo bora ya nchi zetu zinavyoweza kutangaza utalii kwa pamoja. Miongoni mwa faida zilizopatikana kupitia ziara hizo ni pamoja na mji wa Marrakesh kuonesha nia ya kutaka kushirikiana na Manispaa ya Zanzibar katika kuhifadhi maeneo ya urithi. Mji wa Marrakesh una maeneo mengi ya urithi ambayo yamehifadhiwa vizuri hivyo mji wa Zanzibar utapata fursa nzuri sana ya kujifunza namna bora ya kuendeleza mji wetu wa Zanzibar, Mamlaka ya Elimu nchini Morocco nayo imekubali kushirikiana na Mamlaka

za elimu za Tanzania katika kutoa mafunzo kwa vijana katika sekta ya utalii, Mamlaka ya Utalii ya Dubai nayo imekubali kutoa fursa kwa maofisa wetu kwenda kujifunza namna bora ya kutangaza utalii kwa kutumia mitandao ya kisasa ikiwemo mitandao ya kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na wadau imetayarisha na kusambaza nakala 6,500 za vielelezo mbali mbali vya utalii kwa ajili ya kutoa taarifa sahihi za Utalii kwa mujibu wa soko husika. Aidha, Kamisheni ya Utalii imeandaa CD, DVD na video za muda mfupi kwa ajili ya kutangaza utalii kwa njia ya mabango ya matangazo na mitandao ya kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, wizara iliingia makubaliano na Kampuni ya China *Intercontinental Press*. Kupitia makubaliano hayo vipindi maalum vinavyohusu utalii wa Zanzibar vitaandaliwa na kurushwa hewani nchini China. Vile vile, Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Bodi ya Utalii ya Tanzania na Ubalozi wa Tanzania nchini China inaendelea na matayarisho ya ujio ambao wageni hawa wamefika tayari na mimi mwenyewe nimewapokea kwa waandaaji wa *documentary* za utalii kutoka China. *Documentary* hizo zinatarajiwa kurushwa hewani kupitia kituo cha televisheni za Anhui cha China. Televisheni zenye watazamaji wasiopungua milioni 500 duniani kote.

Mhe. Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kuimarisha utangazaji wa bidhaa na huduma za utalii, Kamisheni ya Utalii imeunda kamati shirikishi ya kuitangaza Zanzibar ndani na nje ya nchi. Kamati hiyo inajumuisha wajumbe kutoka Sekta za Umma na Sekta Binafsi zikiwemo Jumuiya ya Wawekezaji wa Sekta ya Utalii (*ZATI*) na Jumuiya ya Waandaaji wa Misafara ya Watalii (*ZATO*).

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kamisheni ya Utalii iliratibu safari ya kutembelea vivutio vya utalii kwa watu 45 ambayo iliwahusisha waandishi wa habari na watu wenye ulemavu. Hatua hiyo ni miongoni mwa mikakati ya kuhamasisha jamii kushiriki katika kufanya utalii wetu wa ndani.

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ya Utalii imeiwezesha Ofisi ya Utangazaji Utalii iliyopo nchini India kufanya kazi za utangazaji kikamilifu kwa kuipatia vielelezo vya utangazaji na kulipa gharama za uendeshaji. Kupitia ofisi hizo, Zanzibar imeweza kujitangaza vizuri nchini India kwa kushiriki maonesho, matamasha, mikutano na makongamano yanayoandaliwa nchini humo. Aidha, ofisi hii iko katika matayarisho ya kuleta wamiliki wa makampuni ya utalii ya India kwa ajili ya kufanya mkutano wa jumuiya yao.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, programu hii ilipangiwa jumla ya shilingi 208,505,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2017 imefanikiwa kupata shilingi 196,130,578/= sawa na asilimia 95.

PROGRAMU YA KURATIBU NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la programu ni kuwa na mazingira na rasilimali watu bora katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya utalii. Programu inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Mipango na Sera, yenye jukumu la kuratibu na kuendeleza utalii pamoja na kujenga uwezo wa mazingira mazuri kwa wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, huduma ambazo zinazotolewa na programu hii ni uratibu na uendelezaji wa utalii na kuwajengea uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ya Utalii imezifanyia marekebisho kanuni za kuendesha biashara za utalii nchini kwa kuzingatia maoni ya wadau yaliyopatikana kwenye warsha mbali mbali zilizofanyika. Aidha, iliendesha zoezi la ukaguzi wa wakala wa biashara za utalii katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar. Zoezi hilo liliwezesha uimarishaji wa huduma za malazi. Vile vile, ushauri wa kitaalamu katika utalii wa viungo uliotolewa kwa watoa huduma 25 katika mashamba ya kilimo cha viungo yaliyopo Kizimbani, Dole na Kianga. Kadhalika, vikundi 27 vya wanawake kutoka katika Wilaya ya Mkoani, Chake Chake, Wete na Micheweni vimepatiwa mafunzo ya utoaji bora wa huduma kwa wateja wao.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa wananchi wanaielewa Sekta ya Utalii na wanashiriki kikamilifu katika shughuli za utalii, Kamisheni ya Utalii imeandaa na kurusha jumla ya vipindi 72 kupitia vyombo vya habari vya Redio na Televisheni. Aidha, Kamisheni ya Utalii imewalipia gharama za mafunzo wafanyakazi wanne ambao wanasoma katika vyuo vya ndani katika fani za Utalii, Masoko na Sheria.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, programu hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 904,395,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2017 imefanikiwa kupata shilingi 682,343,858/= sawa na asilimia 75 na kutakiwa kukusanya jumla ya shilingi 2,000,000,000/= na hadi

kufikia Machi, 2017 jumla ya shilingi 2,058,936,094/= zimekusanywa ambazo ni sawa na uvukaji wa malengo kwa asilimia 103. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E)

PROGRAMU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Mhe. Mwenyekiti, programu ina jukumu la kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti pamoja na usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika wizara. Programu imeundwa na programu ndogo tatu, programu ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Habari, Utalii, Utamaduni, na Michezo, kuratibu na kusimamia mipango mikuu ya wizara na kuratibu na kusimamia utawala, uendeshaji na mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo ya utawala na uendeshaji katika Sekta za Habari, Utalii, Utamaduni, na Michezo inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Mhe. Mwenyekiti, huduma zinazotolewa katika programu ndogo hii, ni kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi na utayarishaji wa ripoti za fedha na ukaguzi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, katika kusimamia majukumu yake ya kiutendaji Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanya ziara za kikazi katika taasisi zilizopo chini ya Ofisi Kuu Pemba na Dar es Saalam kwa ajili ya kuelewa utendaji kazi na changamoto ambazo zimejitokeza. Aidha, idara imeimarisha mashirikiano na wadau wa ndani na nje ya wizara katika sekta zote nne zinazosimamiwa na wizara. Pia, viongozi na watendaji wameshiriki katika makongamano, mikutano na warsha tofauti nchini Ujerumani, Iran, China, Dubai, Ethiopia, Uganda na Kenya.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya wafanyakazi 42 katika ngazi na fani tofauti wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu ikiwemo ngazi ya Shahada ya Pili wafanyakazi tisa, Shahada ya Kwanza wafanyakazi tisa, Stashahada wafanyakazi 19 na Cheti wafanyakazi watano ambapo mafunzo hayo yana lengo la kukuza, kuongeza ufanisi na utendaji mzuri wa majukumu yao ya kila siku wanapokuwa wizarani. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 2).

Mhe. Mwenyekiti, idara katika kuimarisha mazingira mazuri ya kazi imeweza kuzipatia ofisi zake vitendea kazi na vifaa mbali mbali kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika kazi. Aidha, Kitengo cha Ukaguzi wa Fedha za Ndani

kimetayarisha ripoti za fedha na ukaguzi kwa lengo la kuhakiki matumizi sahihi ya fedha za serikali. Pia, Kitengo cha Ugavi na Manunuzi kimetayarisha Mpango wa Utekelezaji wa Manunuzi wa mwaka pamoja na Mpango wa Matumizi ya Fedha kwa ajili ya kuwa na utaratibu wa manunuzi ambao utafatwa na taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, idara imeweza kutayarisha na kusimamia vikao vya Kamati ya Uongozi na Kamati Tendaji ya wizara kwa ajili ya kujadili rasimu ya Sera ya Michezo, Sera ya Utalii, Sera ya Urithi wa Mambo ya Kale, Kanuni na Sheria ya Tume ya Utangazaji, Waraka wa mauzo wa vitabu vya BAKIZA, Taarifa ya Zanzibar kujiunga na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (*CAF*) na Bajeti ya Wizara ya mwaka wa fedha 2017/18 huu ambao tunaiwasilisha leo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,645,735,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2017 imefanikiwa kupata shilingi 1,099,185,200/= sawa na asilimia 67. (Tafadhali angalia kiambatanisho nambari 1D)

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo ya kuratibu na kusimamia mipango mikuu ya wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la kupanga, kutayarisha, kufuatilia na kutathmini mipango, sera, tafiti na miradi ya maendeleo ya wizara.

Mhe. Mwenyekiti, huduma ambazo zinatolewa na uratibu wa sera na tafiti, kuandaa na kuwasilisha bajeti ya wizara, kuandaa na kusimamia mipango na miradi ya maendeleo ya wizara.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, katika kukamilisha Sera ya Michezo na Sera ya Utalii za mwaka 2017 zinazopendekezwa, idara ipo katika hatua za kuwasilisha rasimu hizo katika kikao cha Makatibu Wakuu kwa ajili ya kujadiliwa na baadae kupelekwa BLM. Aidha, katika hatua za awali idara imetayarisha Rasimu ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Michezo ya mwaka 2017 ambao kwa sasa unajadiliwa na wataalamu wa Wizara. Mkakati huo unatarajiwa kuwasilishwa kwa wadau wakuu wa utekelezaji wa sera ili wapate kujadili na kutoa michango katika kurahisisha utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, idara imefanya utafiti kuhusu usahihi wa maelezo katika maeneo ya kihistoria Unguja na Pemba yakiwemo Mkamandume, Ras Mkumbuu, Kichokochwe, Banani, Makutani -Tumbatu, Msikiti wa Kizimkazi, Bi Khole na Mwinyi Mkuu-Dunga. Ripoti ya awali juu ya usahihi wa maelezo ya maeneo ya kihistoria kwa Unguja na Pemba imekamilika na imewasilishwa kwa wadau kwa lengo la kutoa maoni na michango juu ya taarifa hiyo. Kwa sasa ripoti hii amekabidhiwa mtaalamu kwa lengo la kufanya uhakiki wa mwisho kabla ya kuwasilishwa katika ngazi kuu za utendaji. Aidha, idara imefanya utafiti wa ukusanyaji wa maoni ya wadau wa filamu juu ya uanzishwaji wa Sera ya Taifa ya Filamu na shughuli hii imekamilika kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, idara kupitia Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini imetembelea na kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa na wizara ikiwemo Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Michezo cha Mao-Tse-Tung kilichopo Kikwajuni, Mradi wa Kutengeneza Njia ya Kukimbilia katika Uwanja wa Gombani Pemba, Mradi wa Uhifadhi na Uendelezaji wa Maeneo ya Kihistoria uliopo eneo la Kuumbi-Jambiani na Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Uandishi wa Habari Kilimani, lengo ni kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa ufanisi mkubwa na serikali.

Mhe. Mwenyekiti, idara imeandaa taarifa za utekelezaji wa shughuli za wizara pamoja na miradi ya maendeleo na kuwasilishwa Tume ya Mipango. Aidha, idara imeaandaa ripoti za utekelezaji katika kikao cha pamoja kati ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein na watendaji wa wizara. Vile vile, imeandaa ripoti kwa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, programu hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 136,505,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2017 imefanikiwa kupata shilingi 102,214,450/= sawa na asilimia 75. Kwa miradi ya maendeleo iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,000,000,000/= ambapo shilingi 400,000,000/= ni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa uwanja wa Mao-Tse-Tung Studium na shilingi 600,000,000/= ni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Maabara ya Utalii, hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya shilingi 689,535,000/= sawa na asilimia 69 zimepatikana, ambapo shilingi 315,750,000/= sawa na asilimia 79 ni kwa ajili ya mradi wa Mao-Tse-Tung na shilingi 373,785,000/= sawa na asilimia 62 ni kwa ajili ya mradi wa Maabara ya Utalii. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D kinaonesha urefu wa maelezo hayo).

Mhe. Mwenyekiti, programu ya kuratibu na kusimamia utawala, uendeshaji na mipango ya Ofisi Kuu Pemba inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, huduma ambazo zinatolewa ni uratibu wa sera, tafiti na mipango mikuu ya Ofisi Kuu Pemba, kuratibu miradi ya maendeleo na kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya wafanyakazi wanne wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi tafauti ikiwemo Stashahada wawili na Shahada wawili katika fani ya Manunuzi na Ugavi, Uwekaji kumbukumbu, Uchumi na Urithi wa Utamaduni na Utembezaji wageni ambapo mafunzo hayo yana lengo la kukuza na kuendeleza utendaji mzuri wa majukumu ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi Kuu Pemba imefanya utayarishaji wa *documentary* katika maeneo ya kihistoria kwa ajili ya kuhifadhi na kuendeleza maeneo hayo. Aidha, shughuli hii inaendelea katika maeneo 10. Pia, jumla ya vipindi vinane vimetayarishwa na kurushwa hewani kupitia *ZBC TV* pamoja na kuratibu kazi za kutafuta vivutio vya utalii ndani ya msitu wa Ngezi na taarifa zake kwa kushirikiana na Idara ya Misitu na Mali Asili zisizorejesheka.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuufanya uwanja wa Gombani Pemba kuwa wa kisasa na wenye hadhi ya kimataifa, Ofisi Kuu Pemba imekamilisha uwekaji wa mpira katika njia za kukimbilia Tatan na kufanya matengenezo ya ukumbi wa mikutano. Aidha, katika kuweka mazingira bora ya kazi, Ofisi Kuu Pemba imefanya matengenezo madogo ya jengo la ofisi Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, programu hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 963,328,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2017 imefanikiwa kupata shilingi 645,944,450/= sawa na asilimia 67. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D).

MAENEO YA VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, wizara imejipangia maeneo muhimu ya utekelezaji kuwa ni vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Vipaumbele hivyo ni vitavyotekelezeka na vitavyosimamiwa vizuri ni kama vifuatavyo:-

i. Kuimarisha miundombinu ya Habari.

ii. Kuimarisha eneo la kihistoria la Bi Khole, Fukuchani na maeneo mengine.
iii. Kutayarisha Sera ya Taifa ya Filamu.
iv. Kujenga viwanja vya Michezo vya Wilaya Unguja na Pemba.
v. Kuongeza ubora na wingi wa huduma za utalii na kuzitangaza ndani na nje ya nchi.

MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo imepangiwa jumla ya shilingi 19,376,020,000/=. Kati ya fedha hizo shilingi 12,278,520,000/= kwa matumizi ya kawaida na shilingi 7,097,500,000/= kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, katika fedha za miradi ya maendeleo wizara imepangiwa jumla ya shilingi 1,500,000,000/= ikiwa ni mchango kutoka serikalini kati ya hizo shilingi 1,000,000,000/= kwa mradi wa Maabara ya Utalii, shilingi 500,000,000/= ni kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa viwanja vya Wilaya. Aidha, shilingi 5,597,500,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Mao-Tse-Tung ikiwa ni mchango kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1F).

KUWASILISHA BAJETI YA MFUMO WA PROGRAMU (*PROGRAM BASED BUDGET - PBB*) KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo itatumia jumla ya shilingi 19,376,020,000/= kwa ajili ya kutekeleza programu kuu tano ambazo ni:-

1. Programu ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji. (Shilingi 4,814,166,000/=)
2. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni na Michezo. (Shilingi 2,733,006,000/=)
3. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii. (Shilingi 425,293,000/=)
4. Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii. (Shilingi 1,152,507,000/=)
5. Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. (Shilingi 10,251,048,000/=) (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1G, 1H na 1I)

Programu ya 1: Maendeleo ya Habari na Utangazaji

Mhe. Mwenyekiti, programu ina jukumu la kuhakikisha kuwa na jamii iliyoimarika katika maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kupitia habari. Aidha, matokeo ya muda mrefu katika programu hii ni wananchi kupata na kutumia habari zenye kiwango cha juu na zenye ubora. Programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 4,818,910,000/= na imepangiwa kusimamia programu ndogo mbili:-

- Upatikanaji na Usambazaji wa Habari. (Shilingi 4,599,766,000/=)
- Usimamizi wa Vyombo vya Habari na Utangazaji.(Shilingi 214,400,000/=)

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo ya upatikanaji na usambazaji wa habari inatekelezwa na Taasisi na Idara tofauti nazo ni, Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*), Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Magazeti ya Serikali, Chuo cha Uandishi wa Habari na Kampuni ya Usambazaji Maudhui (*ZMUX*), jukumu la msingi katika Programu ndogo ni kuarifu, kuelimisha na kuburudisha jamii, kuratibu uchapishaji wa magazeti ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kutoa mafunzo ya taaluma ya uandishi wa habari na mawasiliano. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni urushaji wa vipindi kupitia TV na Redio, utoaji wa taarifa picha, makala, filamu na sinema, utoaji wa magazeti, utoaji wa mafunzo ya habari na mawasiliano na usambazaji wa maudhui ya utangazaji. Mhe. Mwenyekiti, ili programu ndogo hii iweze kutekelezeka katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 naliomba Baraza lako tukufu kwa heshima na unyenyekevu kuidhinisha jumla ya shilingi 4,599,766,000/= kwa kazi za kawaida na makusanyo ya Shilingi 1,748,600,000/= kwa kuzikusanya kwa ajili ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo ya pili ni usimamizi wa vyombo vya habari na utangazaji ambayo inatekelezwa na Taasisi na Idara zifuatazo:

Idara ya Habari Maelezo na Tume ya Utangazaji Zanzibar na jukumu la msingi katika programu ndogo hii ni kusimamia vyombo vya utangazaji vya serikali na vya binafsi vinavyoanzishwa nchini ili kwenda sambamba na Sheria ya Habari na Utangazaji. Huduma ambayo inatarajiwa kutolewa ni udhibiti na usimamizi wa shughuli za habari na utangazaji kupitia Sera na Sheria za Habari na Utangazaji.

Mhe. Mwenyekiti, ili programu ndogo hii nayo iweze kutekelezwa vizuri katika mwaka huu wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kupitia wajumbe wako kuidhinisha jumla ya shilingi 214,400,000/= kwa kazi za kawaida lakini pia na majukumu ya kukusanya shilingi 100,000,000/=

Programu ya 2: Maendeleo ya Utamaduni na Michezo

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa utamaduni wa Zanzibar unawaendeleza wasanii kiuchumi na kupunguza umasikini pamoja na kuifanya michezo kuwa ni sehemu ya kujenga afya na ajira kwa jamii. Aidha, matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa soko la kazi za sanaa, uhifadhi wa utamaduni na kukuza michezo. Programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 2,733,006,000/= na itakuwa na programu ndogo mbili.

- Uimarishaji wa Utamaduni na Maeneo ya Kihistoria. (shilingi 2,369,486,000/=)
- Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo. (shilingi 363,520,000/=)

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo ya uimarishaji wa utamaduni na maeneo ya kihistoria inatekelezwa na Taasisi na Idara zifuatazo:

Idara ya Utamaduni na Michezo; Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni; Baraza la Kiswahili na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale. Jukumu la msingi katika programu ndogo hii ni kusimamia, kuratibu, kuimarisha, kuendeleza na kudumisha shughuli zote za utamaduni hapa Zanzibar. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uendelezaji na ukuzaji wa shughuli za utamaduni kwa wananchi, kurikodi kazi za sanaa kupitia studio ya filamu na muziki, uratibu wa kazi za sanaa na wasanii, ukaguzi wa filamu na sanaa za maonesho, utoaji wa elimu kuhusu mafunzo fasaha ya Kiswahili, uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya kihistoria, uelimishaji na ushirikishaji wa jamii katika uhifadhi wa maeneo ya kihistoria na urithi wa utamaduni.

Mhe. Mwenyekiti, ili programu ndogo iweze kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinishiwa jumla ya shilingi 2,369,486,000/= kwa kazi za kawaida na pia tunachukua jukumu la kukusanya shilingi 297,553,000/=

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo ya uendelezaji na ukuzaji wa michezo inatekelezwa na Taasisi na Idara zifuatazo:

Idara ya Utamaduni na Michezo na Baraza la Taifa la Michezo. Jukumu la msingi katika programu ndogo hii ni kusimamia maendeleo ya michezo yote iliyosajiliwa nchini. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uratibu na uendelezaji wa shughuli za michezo, uendelezaji wa miundombinu ya michezo na usimamizi wa shughuli za vyama vya michezo kupitia Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, ili programu hii ndogo iweze kufanya kazi zake katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 363,520,000/= kwa kazi za kawaida.

Programu ya 3: Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi ili kuleta tija kwa maslahi ya Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la programu hii ni kuongeza tija ya Sekta ya Utalii kwa kuongeza ajira kwa jamii, idadi ya watalii na thamani yao wanayokuja nayo. Matokeo ya muda mrefu katika programu hii ni kuifanya Zanzibar kuwa kituo bora cha utalii chenye kukidhi mahitaji ya jamii na watalii wake. Huduma inayotarajiwa kutolewa ni kuitangaza Zanzibar ndani na nje ya nchi ili watalii wengi waongezeke kuja hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, ili programu hii iweze kutekelezeka kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 425,293,000/= kwa kazi za kawaida.

Programu ya 4: Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Mipango na Sera, ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kuendeleza utalii pamoja na kuwajengea uwezo na mazingira mazuri ya kazi wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri samahani kidogo, kwa mujibu wa kanuni zetu ya 96(2) unatakiwa utoe hotuba yako kwa muda wa saa moja na nusu na sasa hivi umebakisha dakika tano.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, namaliza.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa kama unamaliza itakuwa vizuri na kama hujamaliza basi nilikuwa naomba useme tu kama iingie katika uwasilishaji wako...

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, namaliza.

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la programu hii ni kuwa na mazingira na rasilimali watu nzuri katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya utalii. Matokeo ya muda mrefu katika programu hii ni kuwepo kwa utalii endelevu na wenye kuhimili ushindani. Huduma ambazo zinazotarajiwa kutolewa ni uratibu na uendelezaji wa utalii na kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, ili programu hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 1,152,507,000/= kwa kazi za kawaida na makusanyo ya shilingi 4,000,000,000/=.

Programu ya 5: Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu mipango katika wizara ya matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa kusimamia usimamizi bora wa mipango na uendeshaji. Programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 10,251,048,000/= na itasimamia programu ndogo tatu.

- Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. (Shilingi 1.9 bilioni)
- Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara. (shilingi 7.2 bilioni=)
- Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba. (Shilingi 1.019 bilioni)

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ndogo ya utawala na uendeshaji katika Sekta za Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo itatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi ambayo ina jukumu la kusimamia shughuli zote za utawala, utumishi, maendeleo, wajibu na maslahi ya wafanyakazi wa wizara.

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la programu ndogo hii ni usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu wa Wizara. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi na utayarishaji wa ripoti za fedha na ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, ili programu hii ndogo iweze kufanikiwa kwa ufanisi zaidi katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 1,972,352,000/= kwa kazi za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo ya kuratibu na kusimamia mipango mikuu ya wizara ambayo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la kupanga, kutayarisha, kuratibu, kufuatilia na kutathmini mipango, sera, tafiti na miradi ya maendeleo ya wizara.

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la programu ndogo ni kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti za Wizara. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uratibu wa sera na tafiti, kuratibu na kuandaa bajeti ya Wizara na kuratibu mipango na miradi ya maendeleo.
Mhe. Mwenyekiti, ili programu ndogo iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 7,258,700,000/=**,** kati ya hizo shilingi 161,200,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 7,097,500,000/= kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo ambapo shilingi 1,000,000,000/= kwa ajili ya Programu ya Maabara ya Utalii na shilingi 500,000,000/= kwa Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya na shilingi 5,597,500,000/= kwa ajili ya Ujenzi wa Uwanja wa *Mao-Tse-Tung* ambazo ni mchango kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo ya kuratibu na kusimamia utawala, uendeshaji na mipango inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba, ambayo ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za Wizara Pemba. Programu ndogo hii ina jukumu la kuhakikisha mipango, malengo na shughuli zote za Wizara zilizopangwa zinatekelezwa kwa ufanisi kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la programu ndogo ni kusimamia na kuratibu shughuli za Utawala, Uendeshaji na Mipango Mikuu ya Wizara katika Ofisi Kuu-Pemba. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uratibu wa sera, tafiti na mipango mikuu ya Ofisi Kuu-Pemba, kuratibu miradi ya maendeleo na kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 1,019,996,000/= kwa kazi za kawaida.

SHUKRANI

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumaliza hotuba yangu naomba kuwashukuru wote waliochangia katika kutayarisha hotuba hii. Shukurani maalumu ziwaendee Mhe. Naibu Waziri Bi. Choum Kombo Khamis, Mshauri wa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Mhe. Abdalla Mwinyi Khamis, Katibu Mkuu

Nd. Omar Hassan Omar (King), Naibu Katibu Mkuu Dkt. Amina Ameir Issa, Naibu Katibu Mkuu Habari Nd. Hassan A. Mitawi, Makatibu Watendaji, Afisa Mdhamini Pemba, Wakurugenzi, Wakuu wengine wa Taasisi za Wizara na wasaidizi kwa wote pamoja na wafanyakazi wote kwa ujumla kwa juhudi, maarifa, uadilifu na umakini mkubwa. Kwa kweli wamekuwa wakinisaidia sana kutekeleza majukumu yangu. Pia, nawashukuru Wenyeviti wa Kamati na Bodi mbali mbali kwa kusimamia vyema taasisi zetu na kunishauri kwa hekima na busara.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwashukuru wafanyakazi, wanamichezo, wasanii, washirika wa utalii na wananchi wote wa Unguja na Pemba kwa michango yao katika kufanikisha shughuli za wizara yangu. Pia shukurani za pekee ziende kwa Vyombo vya Habari vya Serikali na Binafsi, kwa kufanikisha kurusha vipindi mbali mbali vya kuelimisha jamii kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuishukuru Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano mkubwa waliotupa kwa mahitaji ya fedha na ushauri, pamoja na kuishukuru vizuri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu nizishukuru nchi mbali mbali za Mashirika kadhaa ikiwemo Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Misri, Ujerumani, Oman, Iran, Kenya, Uganda, Ethiopia, Shirika la *UNESCO*, Shirika la Urithi wa Dunia na Shirika la Utangazaji la Ujerumani (*DW*) tuliyoshirikiana nao katika utekelezaji wa majukumu ya wizara.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naomba kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote akiwemo Mwenyekiti wa Kamati hii na Wajumbe wake pamoja na Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu, kwa umakini na kwa kina kabisa kuielezea bajeti hii.

MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa naliomba Baraza lako tukufu kujadili kwa kina matumizi ya jumla ya shilingi 19,376,020,000/=**.** Kati ya hizo shilingi 12,117,320,000/= kwa kazi za kawaida, shilingi 5,597,500,000/= ni mchango kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa ajili ya Ujenzi wa Uwanja wa *Mao-Tse-Tung* na shilingi 1,000,000,000/= kwa utekelezaji wa Programu ya Maabara ya Utalii na shilingi 500,000,000/= kwa ujenzi wa viwanja vya Wilaya. Aidha, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe makusanyo mazito ya kuyakusanya ya shilingi 4,468,303,000/= kwa fedha zinazoingia katika Mfuko

Mkuu wa Serikali. Pia, makusanyo ya shilingi 1,710,000,000/= ambazo hukusanywa na taasisi zilizoruhusiwa kutumia makusanyo na kutumiwa na taasisi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba nimshukuru sana mke wangu mpenzi, habibi aliyenisababisha kuwa na *speed* ya kusoma hotuba hii kuanzia nilipoanza na nikawa na utulivu hadi nilipomaliza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ahsante sana. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

VIAMBATISHO
KIAMBATISHO NAMBA 1 A
FEDHA ZILIZOINGIZWA KUANZIA JULAI 2016 HADI MACHI 2017
KWA MATUMIZI YA KAWAIDA
TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU

NO.	TAASISI	MAELEZO	BAJETI 2016/2017	FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI - MACHI 2016/2017	ASILIMIA
1	Ofisi Kuu Pemba	Mishahara	428,539,000	333,138,450	78%
		Matumizi Mengineyo	534,789,000	312,806,000	58%
	JUMLA		**963,328,000**	**645,944,450**	**67%**
2	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	Mishahara	-	-	
		Matumizi Mengineyo	136,505,000	102,214,450	75%
	JUMLA		**136,505,000**	**102,214,450**	**75%**
3	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	Mishahara	1,050,682,000	782,927,900	75%
		Matumizi Mengineyo	595,053,000	316,257,300	53%

	JUMLA		**1,645,735,000**	**1,099,185,200**	**67%**
4	Idara ya Habari Maelezo	Mishahara	208,219,000	158,136,550	76%
		Matumizi Mengineyo	112,170,000	98,336,120	88%
	JUMLA		**320,389,000**	**256,472,670**	**80%**
5	Idara ya Utamaduni na Michezo	Mishahara	618,519,000	490,541,450	79%
		Matumizi Mengineyo	290,201,000	212,154,046	73%
	JUMLA		**908,720,000**	**702,695,496**	**77%**
6	Idara ya Makumbusho na Mambo ya kale	Mishahara	418,941,000	276,626,850	66%
		Matumizi Mengineyo	219,282,000	147,786,650	67%
	JUMLA		**638,223,000**	**424,413,500**	**67%**
7	Kamisheni ya Utalii	Mishahara	576,100,000	398,864,660	**69%**
		Matumizi Mengineyo	536,800,000	479,609,776	**89%**
	JUMLA		**1,112,900,000**	**878,474,436**	**79%**
	JUMLA YA MISHAHARA		**3,301,000,000**	**2,440,235,860**	**74%**
	JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO		**2,424,800,000**	**1,669,164,242**	**69%**
	JUMLA KUU KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU		**5,725,800,000**	**4,109,400,102**	**72%**

TAASISI ZA RUZUKU

NO.	TAASISI	MAELEZO	BAJETI 2016/2017	FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI -MACHI 2016/2017	ASILIMIA
1	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Mishahara	1,463,327,000	1,127,250,650	77%
		Matumizi Mengineyo	392,000,000	308,926,301	79%
	JUMLA		**1,855,327,000**	**1,436,176,951**	77%
2	Shirika la Magazeti ya Serikali	Mishahara	287,592,000	215,586,500	75%
		Matumizi Mengineyo	238,000,000	202,500,000	85%
	JUMLA		**525,592,000**	**418,086,500**	**80%**
3	Chuo cha Uandishi wa Habari	Mishahara	278,343,000	306,184,600	110%
		Matumizi Mengineyo	56,000,000	56,000,000	100%
	JUMLA		**334,343,000**	**362,184,600**	**108%**
4	Tume ya Utangazaji	Mishahara	163,144,000	102,754,600	63%
		Matumizi Mengineyo	56,000,000	48,620,135	87%
	JUMLA		**219,144,000**	**151,374,735**	**69%**
5	Chuo cha Maendeleo ya Utalii	Mishahara	366,194,000	279,006,350	76%
		Matumizi Mengineyo	42,000,000	42,000,000	100%

	JUMLA		**408,194,000**	**321,006,350**	**79%**
6	Baraza la Kiswahili	Mishahara	-		
		Matumizi Mengineyo	42,000,000	37,153,400	88%
	JUMLA		**42,000,000**	**37,153,400**	**88%**
7	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	Mishahara			
		Matumizi Mengineyo	84,000,000	63,317,074	75%
	JUMLA		**84,000,000**	**63,317,074**	**75%**
8	Baraza la Michezo	Mishahara	-		
		Matumizi Mengineyo	84,000,000	84,000,000	100%
	JUMLA		**84,000,000**	**84,000,000**	**100%**
9	Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX)	Mishahara			
		Matumizi Mengineyo	406,000,000	323,740,800	80%
	JUMLA		**406,000,000**	**323,740,800**	**80%**
	JUMLA YA MISHAHARA YA RUZUKU		**2,558,600,000**	**2,030,782,700**	**79%**
	JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO YA		**1,400,000,000**	**1,166,257,710**	**83%**

	RUZUKU				
	JUMLA KUU YA RUZUKU		**3,958,600,000**	**3,197,040,410**	**81%**
	JUMLA YA MISHAHARA KWA WIZARA		**5,859,600,000**	**4,471,018,560**	**76%**
	JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO YA WIZARA		**3,824,800,000**	**2,835,422,052**	**74%**
	JUMLA KUU YA WIZARA (MATUMIZI YA KAWAIDA)A		**9,684,400,000**	**7,306,440,612**	**75%**
MIRADI YA MAENDELEO					
1	Maabara ya Utalii		600,000,000	315,750,000	53%
2	Ujenzi wa Uwanja wa Mao Tse Tung (SMZ)		400,000,000	373,785,000	93%
3	Ujenzi wa Uwanja wa Mao Tse Tung (Washirika wa Maendeleo_		5,597,500,000	-	-
	JUMLA KUU YA WIZARA (MIRADI		6,597,500,000	**689,535,000**	**10.5%**

	YA MAENDELEO) B				
	JUMLA KUU YA WIZARA (A+B)		**16,281,900,000**	**7,995,975,612**	**49%**

KIAMBATISHO NAMBA 1B
MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2016 HADI MACHI 2017
MAPATO YANAYOINGIA HAZINA

NO.	TAASISI	BAJETI	MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI HADI MACHI 2016/17	ASILIMIA
1	Idara ya Habari Maelezo	55,000,000	26,676,750	49%
2	Tume ya Utangazaji	100,000,000	51,188,000	51%
3	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale	250,000,000	109,914,202	44%
4	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	120,000,000	56,760,000	47%
5	Baraza la Kiswahili	22,268,000	3,436,000	15%
6	Kamisheni ya Utalii	2,000,000,000	2,058,936,094	103%
	JUMLA	**2,547,268,000**	**2,306,911,046**	**91%**

KIAMBATISHO NAMBA 1C
MAPATO YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA

NO.	TAASISI	BAJETI 2016/2017	MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI HADI HADI MACHI 2017	ASILIMIA
1	Chuo cha Uandishi wa Habari	200,000,000	125,797,671	63%
2	Chuo cha Maendeleo ya Utaliii	530,000,000	297,930,509	56%
3	Shirika la Magazeti ya Serikali	550,000,000	509,852,546	93%
4	Shirika la Utangazaji (ZBC)	500,000,000	434,575,347	87%
5	Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX)	230,000,000	62,658,000	27%
	JUMLA	**2,010,000,000**	**1,430,814,073**	**71%**

KIAMBATISHO NAMBA 1D
FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2016 HADI MACHI 2017 KWA KILA PROGRAMU NDOGO
Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2016 HADI MACHI 2017	ASILIMIA
1	Shirika la Utangazaji Zanzibar	1,855,327,000	1,436,176,951	77%
2	Idara ya Habari Maelezo	320,389,000	256,472,670	80%

3	Shirika la Magazeti ya Serikali	525,592,000	418,086,000	80%
4	Chuo cha Uandishi wa Habari	334,144,000	362,184,600	108%
5	Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX)	406,000,000	323,740,800	80%
	JUMLA	**3,441,452,000**	**2,796,661,021**	**81%**

Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari na Utanagzaji

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2016 HADI MACHI 2017	ASILIMIA
	Tume ya Utangazaji Zanzibar	219,144,000	151,374,735	69%
	JUMLA	**219,144,000**	**151,374,735**	**69%**

Programu ndogo ya Uimarishaji wa Utamaduni na Maeneo ya Kihistoria

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2016 HADI MACHI 2017	ASILIMIA
1	Idara ya Utamaduni na Michezo	744,720,000	583,889,231	78%
2	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	84,000,000	63,317,074	75%
3	Baraza la Kiswahili	42,000,000	37,153,400	88%
4	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale	638,223,000	424,413,500	67%
	JUMLA	**1,508,943,000**	**1,108,773,205**	**73%**

Programu ndogo ya Uendelezaji wa Utalii na Ukuzaji wa Michezo

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2016 HADI MACHI 2017	ASILIMIA
1	Chuo cha Maendeleo ya Utalii	408,194,000	321,006,350	79%
2	Idara ya Utamaduni na Michezo	164,000,000	118,806,265	72%
3	Baraza la Michezo	84,000,000	84,000,000	100%
	JUMLA	**656,194,000**	**523,812,615**	**80%**

Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2016 HADI MACHI 2017	ASILIMIA
	Kamisheni ya Utalii	208,505,000	196,130,578	95%
	JUMLA	**208,505,000**	**196,130,578**	**95%**

Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2016 HADI MACHI 2017	ASILIMIA
	Kamisheni ya Utalii	904,395,000	682,343,858	75%
	JUMLA	**904,395,000**	**682,343,858**	**75%**

Programu ndogo ya Uendeshaji Na Usimamizi wa Sekta za Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2016 HADI MACHI 2017	ASILIMIA
1	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	1,645,735,000	1,099, 185,200	67%
	JUMLA	1,645,735,000	**1,099, 185,200**	**67%**

Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2016 HADI MACHI 2017	ASILIMIA
	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	136,505,000	102,214,450	75%
	JUMLA	**136,505,000**	**102,214,450**	**75%**
	Mradi wa Maabara ya Utalii	600,000,000	373,785,000	62%
1	Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Mao Tse Tung	400,000,000	315,750,000	79%
	JUMLA KUU	**1,000,000,000**	**689,535,000**	**69%**

Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2016 HADI MACHI 2017	ASILIMIA
	Ofisi Kuu Pemba	963,328,000	645,944,450	67%
	JUMLA	963,328,000	645,944,450	**67%**

KIAMBATISHO NAMBA 1E
FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2016 HADI MACHI 2017 KWA KILA PROGRAMU NDOGO
Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari

	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2016 HADI MACHI 2017	ASILIMIA
1.	Shirika la Utangazaji Zanzibar	500,000,000	434,575,347	87%
2	Idara ya Habari Maelezo	55,000,000	26,676,750	49%
3	Shirika la Magazeti ya Serikali	550,000,000	509,852,546	93%
4	Chuo cha Uandishi wa Habari	200,000,000	125,797,671	63%
5	Kampuni ya Usambazaji wa Maudhui (ZMUX)	230,000,000	62,658,000	27%
	JUMLA	**1,535,000,000**	**1,159,560,314**	**75%**

Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari na Utanagzaji

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULY 2016 HADI MARCH 2017	ASILIMIA
	Tume ya Utangazaji Zanzibar	100,000,000	51,188,000	51%
	JUMLA	100,000,000	51,188,000	**51%**

Programu ndogo ya Uimarishaji wa Utamaduni na Maeneo ya Kihistoria

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2016 HADI MACHI 2017	ASILIMIA
1	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	120,000,000	56,760,000	47%
2	Baraza la Kiswahili	22,268,000	3,436,000	15%
3	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale	250,000,000	109,914,202	44%
	JUMLA	**392,368,000**	**170,110,202**	**43%**

Programu ndogo ya Uendelezaji wa Utalii na Ukuzaji wa Michezo

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2016 HADI MACHI 2017	ASILIMIA
	Chuo cha Maendeleo ya Utalii	530,000,000	297,930,509	56%
	JUMLA	**530,000,000**	**297,930,509**	**56%**

Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2016 HADI MACHI 2017	ASILIMIA
	Kamisheni ya Utalii	2,000,000,000	**2,058,936,094**	**103%**
	JUMLA	**2,000,000,000**	**2,058,936,094**	**103%**

KIAMBATISHO NAMBA 1F

BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA HABARI, UTALII, UTAMADUNI NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU

NO.	TAASISI	MAELEZO	BAJETI 2017/2018
1	Ofisi Kuu Pemba	Mishahara	654,996,000
		Matumizi Mengineyo	365,000,000
	JUMLA		**1,019,996,000**
2	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	Mishahara	-
		Matumizi Mengineyo	161,200,000
	JUMLA		**161,200,000**
3	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	Mishahara	1,277,352,000
		Matumizi Mengineyo	695,000,000
	JUMLA		**1,972,352,000**
4	Idara ya Habari Maelezo	Mishahara	317,466,000
		Matumizi Mengineyo	150,000,000
	JUMLA		**467,466,000**

5	Idara ya Utamaduni na Michezo	Mishahara	1,028,652,000
		Matumizi Mengineyo	450,000,000
	JUMLA		**1,478,652,000**
6	Idara ya Makumbusho na Mambo ya kale	Mishahara	680,454,000
		Matumizi Mengineyo	400,000,000
	JUMLA		**1,080,454,000**
7	Kamisheni ya Utalii	Mishahara	677,800,000
		Matumizi Mengineyo	900,000,000
	JUMLA		**1,577,800,000**
	JUMLA YA MISHAHARA		**4,636,720,000**
	JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO		**3,121,200,000**
	JUMLA KUU KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU		**7,757,920,000**

TAASISI ZA RUZUKU

NO.	TAASISI	MAELEZO	BAJETI 2017/2018
1	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Mishahara	2,200,500,000
		Matumizi Mengineyo	369,400,000
	JUMLA		**2,569,900,000**
2	Shirika la Magazeti ya Serikali	Mishahara	422,100,000
		Matumizi Mengineyo	196,600,000
	JUMLA		**618,700,000**
3	Chuo cha Uandishi wa Habari	Mishahara	496,100,000
		Matumizi Mengineyo	111,300,000
	JUMLA		**607,400,000**
4	Tume ya Utangazaji	Mishahara	171,100,000
		Matumizi Mengineyo	43,300,000
	JUMLA		**214,400,000**
5	Chuo cha Maendeleo ya Utalii	Mishahara	-
		Matumizi Mengineyo	-
	JUMLA		**-**
6	Baraza la Kiswahili	Mishahara	-
		Matumizi Mengineyo	32,100,000
	JUMLA		**32,100,000**
7	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	Mishahara	-
		Matumizi Mengineyo	70,900,000

	JUMLA		**70,900,000**
8	Baraza la Michezo	Mishahara	-
		Matumizi Mengineyo	70,900,000
	JUMLA		**70,900,000**
9	Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX)	Mishahara	-
		Matumizi Mengineyo	336,300,000
	JUMLA		**336,300,000**
	JUMLA YA MISHAHARA YA RUZUKU		**3,289,800,000**
	JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO YA RUZUKU		**1,230,800,000**
	JUMLA KUU YA RUZUKU		**4,520,600,000**
	JUMLA YA MISHAHARA KWA WIZARA		**7,926,520,000**
	JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO YA WIZARA		**4,352,000,000**
	JUMLA KUU YA WIZARA (MATUMIZI YA KAWAIDA) A		**12,278,520,000**
MIRADI YA MAENDELEO			
1	Maabara ya Utalii SMZ		1,000,000,000
2	Ujenzi wa viwanja vya Wilaya SMZ		500,000,000
3	Ujenzi wa uwanja wa Mao Tsu Tung (Ruzuku Nje Chaina)		5,597,500,000
	JUMLA KUU YA WIZARA (MIRADI YA MAENDELEO) B		**7,097,500,000**
	JUMLA KUU YA WIZARA (A+B)		**19,376,020,000**

KIAMBATISHO NAMBA 1G
BAJETI INAYOOMBWA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 KWA KILA PROGRAMU NDOGO
Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari

NO.	TAASISI	BAJETI 2017/2018 MATUMIZI	BAJETI 2017/2018 MAPATO
1	Shirika la Utangazaji Zanzibar	2,569,900,000	600,000,000
2	Idara ya Habari Maelezo	467,466,000	38,600,000
3	Shirika la Magazeti ya Serikali	618,700,000	650,000,000
4	Chuo cha Uandishi wa Habari	607,400,000	210,000,000
5	Kampuni ya Usambazaji wa Maudhui (ZMUX)	336,300,000	250,000,000
	JUMLA	**4,599,766,000**	**1,748,600,000**

Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari na Utangazaji

NO.	TAASISI	BAJETI 2017/2018 MATUMIZI	BAJETI 2017/2018 MAPATO
	Tume ya Utangazaji Zanzibar	214,400,000	100,000,000
	JUMLA	**214,400,000**	**100,000,000**

Programu ndogo ya Uimarishaji wa Utamaduni na Maeneo ya Kihistoria

NO.	TAASISI	BAJETI 2017/2018 MATUMIZI
1	Idara ya Utamaduni na Michezo	1,186,032,000
2	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	70,900,000
3	Baraza la Kiswahili	32,100,000
4	Idara ya Makumbusho	1,080,454,000
	JUMLA	**2,369,486,000**

Programu ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo

NO.	TAASISI	BAJETI 2017/2018 MATUMIZI	BAJETI 2017/2018 MAPATO
1	Idara ya Utamaduni na Michezo	292,620,000	-
2	Baraza la Michezo	70,900,000	-
	JUMLA	**363,520,000**	-

Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii

NO.	TAASISI	BAJETI 2017/2018 MATUMIZI	BAJETI 2017/2018 MAPATO
	Kamisheni ya Utalii (Idara ya Masoko)	**425,293,000**	-
	JUMLA	**425,293,000**	-

Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii

NO.	TAASISI	BAJETI 2017/2018 MATUMIZI	BAJETI 2017/2018 MAPATO
	Kamisheni ya Utalii (Idara ya Mipango)	**1,152,507,000**	**4,000,000,000**
	JUMLA	**1,152,507,000**	**4,000,000,000**

Programu ndogo ya Uendeshaji naUsimamizi wa Sekta za Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

NO.	TAASISI	BAJETI 2017/2018 MATUMIZI	BAJETI 2017/2018 MAPATO
	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	1,972,352,000	-
	JUMLA	**1,972,352,000**	**-**

Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara

NO.	TAASISI	BAJETI 2017/2018 MATUMIZI	BAJETI 2017/2018 MAPATO
1.	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	161,200,000	
2.	Mradi wa Maabara ya Utalii Zanzibar (SMZ)	1,000,000,000	
3.	Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Mao-tse- Tung (CHINA)	5,597,500,000	-
4.	Mradi wa Ujenzi wa viwanja vya Wilaya (SMZ)	500,000,000	-
	JUMLA	**7,258,700,000**	**-**

Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba

NO.	TAASISI	BAJETI 2017/2018 MATUMIZI	BAJETI 2017/2018 MAPATO
	Ofisi Kuu Pemba	1,019,996,000	32,150,000
	JUMLA	**1,019,996,000**	**32,150,000**

KIAMBATISHI NAMBA 1H
MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018
MAPATO YANAYOINGIA HAZINA

NO.	TAASISI	BAJETI 2017/20
1	Idara ya Habari Maelezo	
2	Tume ya Utangazaji	
3.	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale	
4	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	
5	Baraza la Kiswahili	
6	Ofisi Kuu Pemba	
	JUMLA NDOGO	
	Kamisheni ya Utalii	
	JUMLA NDOGO	
	JUMLA	

KIAMBATISHO NAMBA 1I
MAPATO YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA

NO.	TAASISI	BAJETI 2017/2018
1	Chuo cha Uandishi wa Habari	210,000,000
2	Shirika la Magazeti ya Serikali	650,000,000
3	Shirika la Utangazaji (ZBC)	600,000,000
4	Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX)	250,000,000
	JUMLA	**1,710,000,000**

KIAMBATISHO NAMBA 2

WAFANYAKAZI WA WIZARA YA HABARI, UTALII, UTAMADUNI NA MICHEZO AMBAO WAMEKWENDA MASOMONI MWAKA 2016/2017

	Jina Kamili	Jinsia	Taasisi	Fani	Kiwango	Muda	Chuo
1	Nd. Khamisuu Hamid Moh'd	M/ke	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	Public Administration	Shahada ya Pili	Miaka 2	Zanzibar University
2	Nd. Ali Mohammed Ali	M/me	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	Public Administration	Stashahada	Miaka 2	Bishop Barham University Kabale Uganda
3	Nd. Mwanajuma Muki Makame	M/ke	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	Record Management	Stashahada	Miaka 2	ICPS
4	Nd. Naomi Kurwa	M/ke	Idara ya Uendeshaji na	Record Management	Cheti	Mwaka 1	ICPS
5	Nd. Saada Suleiman	M/ke	Idara ya Mipango,	Development Policy	Shahada ya	Miaka 2	Mzumbe Universit
6	Nd. Khalfan	M/me	Kamisheni ya	Business Administra	Shahada ya Pili	Miaka 2	Zanzibar Universit
7	Nd. Maulid Hassan Chum	M/me	Chuo cha Uandishi wa Habari	Record Management	Stashahada	Miaka 2	ICPS
8	Nd. Iddi Haji Issa	M/me	Idara ya Habari Maelezo	Mass Communication	Shahada ya Kwanza	Miaka 2	Christian University Uganda
9	Nd. Mwantanga Juma Khamis	M/ke	Idara ya Habari Maelezo	Arts in Mass Communication	Shahada ya Kwanza	Miaka 2	Bishop Barham University Kabale Uganda
1	Nd. Fatma Fundi	M/ke	Idara ya Habari	Information	Stashahada	Miaka 2	ICPS

	Salum		Maelezo	Technology			
1	Nd. Shinuna	M/ke	BASSFU	Human Resource	Stashahada	Miaka 2	IPA
1	Nd. Ilyasa Mzee Juma	M/ke	BASSFU	Human Resource Mgt	Stashahada	Miaka 2	IPA
1	Nd. Mourtala Moh'd Ali	M/me	BASSFU	Information Technology	Stashahada	Miaka 2	Karume Collage
1	Nd. Abdul-Aziz Salim Abdul-Aziz	M/me	ZITOD	Tourism	Shahada ya Pili	Miaka 2	The Cyuprus of Marketing Institute
1	Nd. Fatma Ali Juma	M/ke	ZITOD	Air Fair and Ticketing	Stashahada	Miaka 2	Mark Air Travel Academy
1	Nd. Hassan	M/me	ZITOD	IT and Manageme	Shahada ya	Miaka 2	IFM
1	Nd. Issa Mussa Ali	M/me	ZITOD	Air Fair and Ticketing	Stashahada	Miaka 2	Mark Air Travel Academy
1	Nd. Amina	M/ke	ZITOD	Economics	Shahada ya	Miaka 3	Zanzibar Universit
1	Nd. Safia Ujudi	M/ke	ZITOD	Tourism	Shahada ya	Miaka 2	Iringa Universit
2	Nd. Zaituni Mussa Ali	M/ke	ZITOD	Tourism Management &	Shahada ya Pili	Mwaka 1	Bournemouth Universit
2	Nd. Nafla Seif	M/ke	ZITOD	Secretary	Cheti	Mwaka 1	IPA
2	Nd. Msena	M/me	ZITOD	Procurement &	Shahada ya	Miaka 3	ICPS

2	Nd. Hamed Abdalla Abdalla	M/me	ZIToD	Tourism Management & Marketing	Shahada ya Pili	Miaka 2	Makerere University (Uganda)
2	Nd. Suleiman	M/me	ZIToD	Ufundi	Cheti	Mwaka 1	Chuo cha Ufundi
2	Nd. Muhamm	M/me	ZIToD	Ufundi	Cheti	Mwaka 1	Chuo cha Ufundi
2	Nd. Halima Juma Omari	M/ke	Makumbusho na Mambo ya Kale	Project Planing & Management	Shahada ya Pili	Miaka 2	Chuo Kikuu Kabale Uganda
2	Nd. Kei Mohammed Abdalla	M/ke	Makumbusho na Mambo ya Kale	Tourism Management & Marketing	Shahada ya Kwanza	Miaka 3	SUZA
2	Nd. Faida Ramadhani Senga	M/me	Makumbusho na Mambo ya Kale	Tourism Management and Marketing	Shahada ya Kwanza	Miaka 3	SUZA
2	Nd. Ibrahim Ali Sharifu	M/me	Makumbusho na Mambo ya Kale	Tourism Management & Marketing	Shahada ya Kwaza	Miaka 3	SUZA
3	Nd. Zuhura A. Juma	M/ke	Makumbusho na Mambo ya Kale	Tourism Management & Marketing	Shahada ya Kwanza	Miaka 3	SUZA
3	Nd. Mjaka Bakari Ali	M/me	Makumbusho na Mambo	Electricty	Cheti	Miaka 2	Elimu Mbadala Forodhan
3	Nd. Aisha Mohd Khamis	M/ke	Shirika la Utangazaji (ZBC)	A/C Islamic Banking	Shahada ya Kwanza	Miaka 3	ICPU
3	Nd. Mwanakhamis Sosi Ameir	M/ke	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Journalism	Stashahada	Miaka 2	Royal Collage
3	Nd. Hadia Kombo Hussein	M/ke	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Journalism	Stashahada	Miaka 2	Royal Collage

3	Nd. Saada Janabi Amour	M/ke	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Journalism	Stashahada	Miaka 2	Royal Collage
3	Nd. Zuhura Mgeni	M/ke	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Journalism	Stashahada	Miaka 2	Open Royal Collage
3	Nd. Fatma Mussa Moh'd	M/ke	Shirika la Utangazaji (ZBC)	ICT	Stashahada	Miaka 2	ZIToD
3	Nd. Hidaya Abdalla Salum	M/ke	Shirika la Utangazaji (ZBC)	ICT	Stashahada	Miaka 2	ZIToD
3	Nd. Rajab Khamis Rashid	M/me	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Information Technolog-	Stashahada	Miaka 2	ZIToD
4	Nd. Saada Hassan Chande	M/ke	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Secretary	Stashahada	Miaka 2	IPA
4	Nd. Amina Moh'd	M/ke	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Journalism	Stashahada	Miaka 2	Royal Collage
4	Nd. Khadija Mussa Ali	M/ke	Ofisi Kuu Pemba	Information Technolog-	Stashahada	Miaka 2	Dar Collage

KIAMBATISHO NAMBA 3
MASHINDANO MBALI MBALI AMBAYO ZANZIBAR ZILISHIRIKI KWA MWAKA 2016/2017

S/NO.	CHAMA	MASHINDANO	PAHALA	MAELEZO
1.	Chama cha Netiboli	Mashindano ya Afrika Mashariki ya mchezo wa Netiboli	Nairobi-Kenya, 2017	Timu mbili zimeshiriki lakini hazikufanya vizuri.
		Mashindano ya Klabu Bingwa ya Zanzibar	Zanzibar, 2017	Kwa upande wa wanaume timu ya JKU ilipata nafasi ya kwanza na Polisi wa pili na kwa wanawake timu Mafunzo ilapata nafasi ya kwanza na JKU nafasi ya pili.
2.	Chama cha Mchezo wa Kuogelea	Mashindano ya Klabu Bingwa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mchezo wa kuogelea	Dar-es-salaam, Machi, 2017	Timu ya KMKM ilipata ushindi wa tisa wa jumla katika timu 15 na kupata medali nne za fedha na nne za shaba na Timu ya WAHOO ilipata ushindi wa sita jumla.
3.	Chama cha Mpira wa Wavu	Mashindano ya Klabu bingwa ya Volleyball	Pemba, 2016	Kwa upande wa wanaume timu ya Polisi ilapata nafasi ya kwanza na Polisi wa pili na kwa wanawake timu Wete Stars ilapata nafasi ya kwanza na Makoongwe nafasi ya pili.
		Mashindano ya ligi kuu ya Muungano	Dar es salaam,	Timu ya mafunzo ilitolewa katika

			2017	hatua ya nusu fainali na timu ya Polisi ilitolewa katika ngazi ya makundi.
4.	Chama cha mpira wa Miguu	Mashindano ya kimataifa ya Kombe la Mapinduzi	Zanzibar, Januari, 2017	Timu ya Azam kutoka Dar es salaam ilipata mshindi wa kwanza
		Mashindano ya CECAFA	Uganda, 2016	Timu ya wanawake ya Zanzibar wameshiriki katika mashindano hayo.
5.	Chama cha Mpira wa Vikapu	Mashindano ya Klabu Bingwa ya Zanzibar	Pemba, 2016	Timu ya Polisi ilipata ushindi wa kwanza na Timu ya Nyuki walipata ushindi wa pili.
		Mashindano ya ligi kuu ya Muungano	Zanzibar, 2017	Timu ya Nyuki wanaume ya Zanzibar walipata mshindi wa kwanza na JKT Star wanawake wamepata mshindi wa kwanza
6.	Chama cha JUDO	Mashindano ya 11 ya Afrika Mashariki	Zanzibar, Machi, 2017	Zanzibar ilipata mshindi wa tatu kwa kupata Medali moja ya dhahabu, nne fedha na nne shaba kwa upande wa wanaume na wanawake walipata ushindi wa tatu kwa

				kupata medali moja ya dhahabu, moja ya fedha, na moja shaba.
		Mashindano ya "Zanzibar Budokan Cup"	Zanzibar, Disemba, 2016	Vilabu mbali mbali kutoka Unguja, Pemba na Tanzania Bara vilishiriki mashindano hayo
7.	Chama cha Riadha	Mashindano ya Vilabu	Zanzibar, 2016	Timu ya KMKM ilipata nafasi ya kwanza na JKU nafasi ya pili
		Mashindano ya Kimataifa ya Kilimanjaro Marathon	March, 2017	Mchezaji wa Zanzibar alipata nafasi ya kwanza na amechaguliwa kujiunga na timu ya Taifa ya Tanzania amabayo itashiriki Mashindano ya Riadha ya Afrika.
		Mashindano ya mbio za Nyika	Moshi, 2017	Wachezaji wa Zanzibar walichaguliwa kujiunga na timu ya Taifa ya Tanzania ambao walishiriki mashindano ya Kili Marathon.
		Mashindano ya mbio za Nyika	Zanzibar, 2017	Jumla Wachezaji 12 kati ya hao sita wanaume na sita wanawake walichaguliwa kuunda timu ya Taifa ya Zanzibar ambao walishiriki

				mashindano ya Mbio za nyika huko Moshi.
8.	Zanzibar Weight lifting Association	Mashindano ya Afro-Asia Weightlifting Championship	Jordan, 2016	Zanzibar wamepata nafasi ya tisa kwa upande wa wanaume
9.	Chama cha Mpira wa Mikono	Mashindano ya Kombe la Challenge	Uganda, 2016	Timu za Zanzibar hazikufanya vizuri
10.	Chama cha Michezo ya Viziwi Zanzibar	Mashindano ya mpira wa miguu ya michezo ya Viziwi	Kisumu Kenya, 2016	Timu ya Zanzibar ilipata nafasi ya pili.
11.	Chama cha Baskeli	Mashindano ya kuhamasisha mchezo wa Baskeli	Pemba, 2016	Vilabu mbali mbali kutoka Unguja na Pemba vilishiriki
12.	Chama cha Mazoezi ya viungo Zanzibar	Maadhimisho ya kitaifa ya Tamasha la siku ya mazoezi ya viungo Zanzibar	Zanzibar, 2017	Vilabu mbali mbali kutoka Unguja na Pemba na Dar es salaam vilishiriki

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa uwasilishaji wako mzuri. Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kumwita Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii naomba tuwatambue wageni wetu wa leo ambao ni wageni wa Mhe. Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mhe. Mgeni Hassan Juma nao ni wasanii wa Filamu na Muziki. Wasanii wa muziki wa kwanza ni Sultan King, pili Joseph (King Poza) na wa tatu msanii Abdul (Pozi Adimu). Kwa upande wa wasanii wa Filamu Zanzibar ni Josephine Fina, mwengine Khamis Ferouz. Wasanii wa Filamu Dar es Salaam wa kwanza Hidaya Njaidi na wa pili Ester, huyu ni *photographer*. Wasimamizi wao wa kwanza ni Khamis H. K (Kaka Meneja), wa pili Ima Minane (*Producer Music*).

Wageni wengine ni wa Mhe. Rashid Ali Juma, Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ambao ni Wenyeviti wa Bodi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Wa kwanza Bibi Sabahi Saleh Ali, Mwenyekiti

Kamisheni ya Utalii huyo; wa pili Bibi Mariam Hamdani, Mwenyekiti Baraza la Sanaa na Sensa; wa tatu Bwana Bakari Is-haka kwa niaba ya Mwenyekiti *ZBC*, mwengine ni Bibi Jamila Borafia (ni Mtu mwenye Mahitaji Maalum).

Wageni wengine wa Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, Choum Kombo Khamis ambaye ni Time Bakar Sharif - Mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu Tunguu (*Zanzibar University*). Karibuni sana wageni wetu.

Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kwa maoni ya hotuba.

Mhe. Ali Suleiman Ali: (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu na kutoa Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kuhusiana na Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kwa mara nyengine tena kukutana hapa katika Mkutano huu wa Bajeti ukiwa ni Mkutano wa Bajeti wa Pili kwa Baraza hili la Tisa la Wawakilishi. Aidha, namshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kuijaalia nchi yetu kuendelea kuwa katika hali ya amani, utulivu, usalama na mshikamano; mambo ambayo ni muhimu kwa ustawi wa maendeleo ya jamii ya nchi yetu.

Pili, napenda kuendeleza shukurani zangu za dhati kwako binafsi kwa kuniruhusu kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha mchango wangu kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu na kufuata sheria hali inayopelekea wananchi kuzidi kujenga imani dhidi yake na nchi yetu kuendelea kuwa na amani na utulivu wa kila siku.

Aidha, tunazidi kumpongeza kwa kutekeleza ahadi yake kwa kuongeza mishahara ya Watumishi wa Umma kwa asilimia mia moja. Mhe Rais tunakupongeza hongera sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sina budi pia kumshukuru Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na naibu wake, watendaji wake wakiongozwa na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa mashirikiano waliyotupa wakati wa kupitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii.

Lakini pia nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu kwa kutoa mashirikiano na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisishia kazi yangu ya kuongoza kikao kuwa nyepesi zaidi, kwa hakika ni wajumbe mahiri wenye uwezo wa kuchambua na kutoa mawazo mazuri na ya kujenga.

Pia, wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha kwa wizara hii zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa pamoja na kuleta tija.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima ya hali ya juu napenda kuwatambua Wajumbe hao kama hivi ifuatavyo:

1.	Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	Mwenyekiti
2.	Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Hassan Khamis Hafidh	Mjumbe
4.	Mhe. Maryam Thani Juma	Mjumbe
5.	Mhe. Zaina Abdalla Salum	Mjumbe
6.	Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
7.	Mhe. Mussa Foum Mussa	Mjumbe
8.	Ndugu Himidi Haji Choko	Katibu
9.	Ndugu Haji Jecha Salum	Katibu
10.	Ndugu Amina Abeid Hemed	Mkalimani

Mhe. Mwenyekiti, Miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati yangu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka katika wizara husika kama ilivyoelezwa katika kanuni zetu na leo hii kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati nawasilisha maoni ya Kamati yangu kuhusiana na Bajeti hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Baada ya kutoa utangulizi huo mfupi, naomba nichukue fursa hii adhimu kutekeleza jukumu la msingi lililonileta hapa mbele ya Baraza lako tukufu kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ina mafungu *vote* mawili (2) ambayo ni J01 Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na J02 Kamisheni ya Utalii.

Fungu J01 limejumuisha Programu kuu tatu (3) zenye Programu ndogo saba (7). Fedha iliyoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa fungu hili ni Tshs. 17,807,832,000

Mhe. Mwenyekiti, Programu kuu za fungu hili ni hizi zifuatazo:

1. Programu kuu ya Maendeleo ya habari na Utangazaji.
2. Programu kuu ya Maendeleo ya Utamaduni, Utalii na Michezo.
3. Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Habari, Utalii na Michezo.

Programu Kuu ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji

Mhe. Mwenyekiti, hotuba ya Mhe. Waziri iliyomalizika hivi punde imeelezea kwamba Programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwa na jamii iliyoimarika katika maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kupitia habari.

Mhe. Mwenyekiti, sekta ya Habari ni moja kati ya sekta muhimu sana katika jamii yoyote kwani hutumika kuuhabarisha umma kuhusu mambo mbalimbali yanayoendelea yakiwemo ya kisiasa, kiafya, kielimu na hata kiuchumi. Habari ina nafasi kubwa katika jamii kwani inawezesha watu katika jamii husika kupata taarifa, habari na maarifa na hatimae kuzitumia kwa kudadisi na kuhoji, kufikiri zaidi na kupembua na hatimae kuwa na maoni yatakayomuwezesha kufanya maamuzi sahihi juu ya kile ambacho kinawagusa au kuwahusu.

Mhe. Mwenyekiti, Taifa lenye watu wenye kupata habari sahihi na kwa wakati sahihi linakua vizuri katika nyanja mbalimbali kama vile kiuchumi, kisiasa na hata kiutamaduni. Hapa tunaiomba Wizara na Serikali kwa ujumla kuhakikisha kwamba vyombo vyetu vya habari vinakwenda na wakati kwa kutoa habari haraka iwezekanavyo baada ya kuzifanyia utafiti wa kina.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba bado wananchi wetu wanavipenda, kuviamini na kuvithamini zaidi vyombo vyetu vya *ZBC* Redio na *TV* pamoja na Gazeti letu la Zanzibar leo, hivyo ni vyema kuviimarisha zaidi kwa kuongezewa bajeti pamoja na kuimarishwa kwa rasilimali watu na vifaa ili vizidi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuvishukuru vyombo vyetu hasa kutokana na mfumo wao wa habari na matukio, kwa kweli hivi sasa tunashuhudia mabadiliko makubwa ambapo wananchi wa kawaida mijini na vijijini, wamekuwa wakipewa fursa kubwa kujieleza na kutoa maoni yao katika habari na mijadala mbali mbali. Hii ni hatua nzuri hasa kwa nchi zinazotoa uhuru mpana wa kidemekrasia na zinazofuata Utawala Bora pamoja na Utawala wa Sheria. Hata hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kamati inaitaka wizara kuimarisha zaidi upatikanaji na usikivu bora wa *ZBC TV* na Redio katika sehemu zote za Zanzibar na kwa wakati unaofaa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu pia inazidi kutoa wito kwa Taasisi mbali mbali za Serikali na watu binafsi wanaopata huduma za kutolewa Matangazo kutoka vyombo hivyo kusaidia gharama za hudumu hiyo kwa kulipia matangazo yao, ili hatimae lengo la serikali la kuazisha mashirika ya *ZBC* na Magazeti ya SMZ iweze kufikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, wakati Serikali inaendelea kutafuta mbinu mbali mbali za kuimarisha vyombo vyake , Kamati yangu inaishauri wizara kufuatilia na kuzungumza na Mamlaka ya Mawasiliano ya Serikali ya Mapinduzi ya Tanzania ili kuhakikisha kwamba *ZBC TV* inaonekana kupitia ving'amuzi vyote viliopo hapa nchini bila ya kuingizwa katika mpango wa malipo wa kila mwezi ili wananchi wengi zaidi wazidi kufaidika na matangazo ya *ZBC*.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu pia inatambua mchango wa watu binafsi katika kuinua sekta ya habari hapa nchini, vyombo vya habari vinazidi kuongezeka siku hadi siku na kwa kweli vinatoa mchango mkubwa katika kusaidia ajira kwa vijana wetu, kuinua vipaji mbali mbali, kukuza taaluma na upashanaji wa habari pamoja na burudani. Tunaiomba serikali nayo ithamini mchango wa ndugu zetu hawa hasa kwa kuangalia uwezekano wa kuwapunguzia baadhi ya kodi za vifaa vyao, minara na umeme pamoja na waandishi wa vyombo hivyo kushirikishwa japo kwa zamu wakati viongozi wetu wa kitaifa wanapofanya ziara mbali mbali za kikazi ndani na nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Programu Kuu ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imepangiwa jumla ya Tshs. 4,814,166,000. Hivyo, Kamati yangu inaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha fedha hizo kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya programu hii.

Programu Ndogo ya Usimamizi Wa Vyombo vya Habari na Utangazaji

Mhe. Mwenyekiti, Programu ndogo ya usimamizi wa vyombo vya habari na Utangazaji imelenga kuwa na vyombo vya habari vinavyozingatia sheria, kanuni na maadili ya habari. Kamati inatoa pongezi kwa wizara kwa kutekeleza vizuri majukumu yake chini ya programu hii katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Tume ya utangazaji Zanzibar, Idara ya Habari Maelezo na Baraza la Habari Zanzibar kuhakikisha kwamba inasimamia kwa ukamilifu sheria, kanuni na maadili ya habari ili vyombo vya habari visipate fursa ya kukiuka miongozo hiyo. Kamati yangu inaamini kwamba iwapo misingi na maadili ya Utangazaji na Upashanaji wa habari itafuatwa Taifa na jamii kwa ujumla linaweza kupiga hatua kubwa za kimaendeleo pamoja na kuishi katika hali ya amani na utulivu na endapo misingi hiyo na maadili hayo yatakiukwa, Taifa linaweza kuingia katika taharuki na mfarakano mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaona ni nyema kwa Waheshimiwa Wajumbe tukaruhusu kutekelezwa kwa Programu hii kwa kukubaliana na fedha zote zilizotengwa kwa ajili hiyo.

Programu ndogo ya Uimarishaji wa Utamaduni na Maeneo ya Kihistoria

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu bado hairidhiki kabisa na utendaji hasa katika ukusanyaji wa Mapato yanayotokana na wasimamizi wa Programu hii ambao ni Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni, Baraza la Kiswahili na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale.

Kama alivyosema Mhe. Waziri, programu hii ilitakiwa kukusanya jumla la Tshs. 392,268,000 na hadi kufikia Machi 2017 jumla ya Tshs. 170,110,202 zilikusanywa sawa na asilimia 43**.** Hii inaonesha dhahiri kwamba bado panatakiwa mkakati wa kuhakikisha kwamba fedha zinakusanywa kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, makusanyo hayo ni madogo kabisa hivyo, Kamati inaitaka Wizara kujidhatiti na kusimamia vizuri mipango waliyotueleza ya kuyatambua, kuyahifadhi na kuyaendeleza kwa kuweka miundombinu yote muhimu na hatimae kuyatangaza ipasanyo maeneo ya kihistoria yaliyopo Zanzibar. Na pia kutafuta vianzio vipya vya mapato kwa taasisi zote zinazohusika na programu hii.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu pia inawataka wasimamizi wote wa program hii, kusimamia vizuri ukusanyaji wa mapato na kudhibiti mianya yote ya uvujaji wa mapato hayo ili kufikia malengo ya ukusanyaji yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2017/20118.

Programu ndogo ya Uendelezaji wa Rasilimali watu katika Utalii na Ukuzaji wa Michezo

Mhe. Mwenyekiti, Programu ndogo ya pili ya uendelezaji wa rasilimali watu katika utalii na kukuza michezo inakusudia kuwa na rasilimali watu wenye ujuzi na ustadi wa kukuza utalii nchini na kuifanya michezo kuwa ni sehemu ya kujenga afya na ajira kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inatoa pongezi za dhati kwa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa kufanikisha azma ya Zanzibar kuwa mwanachama wa Shirikisho la Mpira wa Miguu barani Afrika *CAF*. (*Makofi*)

Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa furaha waliyonayo Wazanzibari kwa Zanzibar kupata uanachama wa *CAF* inaendelea kwa wizara kuchukua hatua za kukamilisha masharti yaliyotolewa na *CAF* baada ya kukabidhiwa uanachama huo wa 55.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hatua hiyo iliyofikiwa kwa Zanzibar, Kamati yangu bado inasononeshwa na hairidhishwi kabisa na hali ya nidhamu iliyopo katika michezo hivi sasa . Migogoro ya kila siku katika vyama vyetu na taasisi zinazosimamia michezo hapa Zanzibar pamoja na kesi zinazoendelea mahakamani kuhusiana na sekta ya michezo, kwa kweli ni vitendo vya aibu na vinachangia kwa kiasi kikubwa kudumaza michezo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inatoa wito wa kumalizwa migogoro hiyo na kufungua ukurasa mpya ili nidhamu itawale michezoni na hatimae tufikie malengo na maendeleo tunayoyakusudia katika sekta ya michezo, huku ikitiliwa maanani kwamba michezo ni afya, ajira na inaongeza upendo katika jamii na taifa kwa ujumla.

Kamati yangu inaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 362,520,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Program hii mwaka huu wa fedha wa 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukuwe fursa hii mimi nikiwa Mwenyekiti wa Wizara hii niipongeze klabu ya Yanga kuwa bingwa kwa mwaka 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, hii nasema kwa dhati kutoka kwenye moyo wangu mchezo ni faida, mchezo ni hasara, mchezo ni udugu. Kwa hivyo, anaeshinda apewe hongera na aliekuwa hakushinda tujiandae mwakani ili tufanye vizuri.

Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya utangazaji na uhamasishaji wa utalii imekadiriwa kutekelezwa kwa Tshs. 425,293,000 ambazo zitatumika katika kuitangaza Zanzibar ndani na nje ya nchi yetu.

Kamati yangu inachukua fursa hii kuiomba Wizara kuimarisha Utalii wa ndani kwani nchi yetu imebahatika kuwa na maeneo mengi ambayo yakiendelezwa na kuimarisha yataongeza vivutio vya utalii tulivyonanvyo kama vile magofu, mapango na chumba cha chini kwa chini kule Makangale. Utafiti unaonyesha kuwa nchi nyingi duniani zimekua zikifaidika na mapato yanayotokana na Utalii wa ndani. Kamati yangu inazidi kutoa wito kwa wajumbe wenzetu kukubaliana na maombi ya Kamisheni ili *program* hii iweze kutekelezeka kwa ufanisi zaidi.

Programu ndogo ya Utawala na Usimamizi wa Kamisheni ya Utalii

Mhe. Mwenyekiti, Hotuba ya Mhe. Waziri inaonyesha kwamba Programu hii ina lengo la kuongeza tija ya sekta ya utalii na kuweka mazingira na rasilimali watu bora katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya utalii.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu imebaini kwamba Kamisheni ya Utalii imeweza kuvuka malengo ya ukusanyanji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo ilipangiwa kukusanya shilingi 2,000,000,000. Wakati hadi kufikia Mwezi Machi mwaka huu Kamisheni imefanikiwa kukusanya shilingi 2,058,936,094 asilimia 103 ni asilimia nzuri ambayo inaonesha dhahiri kwamba bado wana uwezo wa kukusanya uwezo wa zaidi na zaidi kutokana na malengo haya waliyoyafikia. Tunapenda kuikumbusha Kamisheni kwamba mafanikio hayo yachukuliwe kwamba ni chachu ya kukusanya zaidi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu pia hairidhiki na mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za Watalii katika vituo vyetu vya Uwanja wa Ndege Kisauni na Bandarini Malindi. Kwa kweli, Kamati yangu ina wasiwasi wa mfumo uliopo sasa ambapo takwimu hizo zinategemea taarifa watakazozipata kutoka Idara ya Uhamiaji. Kamati inaiomba Kamisheni kukaa na taasisi zote mbili

zinazohusika katika vituo hivyo ili kuhakikisha kwamba tunapata takwimu za uhakika ili kulinda maslahi ya mapato yetu.

Mhe. Mwenyekiti, *Program* ndogo hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imekadiriwa kutumia Tshs. 985,967,000 ambapo tunaliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha fedha hizo...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwenyekiti, samahani kidogo kabla ya kuendelea naomba nimpishe Mhe. Naibu Spika aendelee na shughuli zetu

(Hapa Mhe. Naibu Spika alikalia Kiti)

Mhe. Naibu Spika: Haya Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Ali Suleiman Ali: (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, mwisho, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu na kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza. Sasa niwaombe Wajumbe wa Baraza lako waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii ili wamuwezeshe Mhe. Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka huu wa Fedha.

Aidha, navipongeza Vyombo vya Habari vyote kwa kazi zao nzuri wanazozifanya na wananchi wanapata habari bila ya matatizo. Naomba waongeze bidii na serikali inawaangalie kutokana na kazi zao nzuri na nzito wanazozifanya ili faraja iwafikie zaidi na waweze kufanya kazi yao.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati inayohusiana na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Waheshimiwa Wajumbe tunaanza na michango, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mhe. Abdalla Maulid Diwani akimaliza atafuata Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ajitayarishe pia Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis. Mhe. Abdalla Diwani karibu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii adhimu kuwa mchangiaji wa mwanzo katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, salama na kuweza kukutana siku hii ya Jumamosi ya leo hapa, baada ya shukrani hizo na nimshukuru sana na nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri wa madaha uliomfanya kila mmoja kusisimkwa bila kusinzia hata kidogo, Mhe. Waziri hongera sana kwa uwasilishaji wako mzuri.

Vile vile niipongeze wizara yake kwa jumla. Kuanzia yeye mwenyewe Mhe. Waziri, Naibu Waziri wake, kaka yangu Katibu na uongozi mzima wa wizara hii kwa namna thabiti waliyokuwanayo ya kuweza kuona kwamba Zanzibar kwa upande wa habari, utalii na michezo inaondoka hapa ilipo na kusogea mbele zaidi hongereni sana na Mwenyezi Mungu akutieni nguvu kwa hilo.

Vile vile nimpongeze Mhe. Rais kwa dhati kabisa kumuona namna gani jinsi anavyosimamia kuona michezo Zanzibar inapata nafasi yake, nimpongeze sana kwa dhati ya moyo wangu, kwa kuona kwamba Zanzibar tuondoke kule kwenye michezo ya zamani ya riadha na mingine na kuingia katika michezo ya mbele.

Vile vile nimpongeze kwa dhati kabisa Rais wa Chama cha Mpira Zanzibar Ravia Idarus, Katibu wake Maalim Teddy na wengineo kwa kuona Zanzibar sasa tunapata bendera kwa wanachama katika shirikisho la mpira Barani Afrika *CAF*, sio wale wenzetu wengine, *CAF* sasa kuona kwamba tayari tumepata nafasi na imetupa mwanga kwamba mtoto akishazaliwa sasa tumlee mtoto huyu ili akuwe baadae basi mtoto Chino atupe nafasi tuingie katika *CAF*. Nia ipo, sababu ipo na uwezo upo.

Mhe. Naibu Spika, nilisema niseme hayo kwanza kuona kwamba namna gani tumeshapata uanachama wa *CAF*. Mtoto tayari keshazaliwa lakini tatizo kumlea mtoto kuona kwamba tunapata nafasi ya kusogea mbele zaidi katika *FIFA*. Tunajua migogoro kwenye vyama vyetu vya michezo hususan kuanzia Baraza na Chama cha Mpira kuanzia ngazi ya Wilaya na Taifa. Kwa hivyo, ningekuomba sana Mhe .Waziri hili ulisimamie kwa dhati kabisa. Migogoro bado ipo misuguano hususan kutoka kwenye Baraza la Michezo kwenda katika vyama vya chini.

Mhe. Naibu Spika, nathubutu kusema hayo kwa sababu ni shahidi katika Chama cha Mpira Wilaya ya Mjini na uongozi wa *BTMZ* ni paka na chui au

ardhi na mbingu hatuwezi kwenda. Tukumbuke kwamba Wilaya ya Mjini ni mlezi, analelewa na *ZFA* ya taifa lakini hawa wote mlezi wao ni Baraza la Michezo la Taifa. Ziondoke hizi tofauti ili tuone ni namna gani tunacheza mpira wetu. Mpira sasa hivi sio starehe tena bali ni ajira. Wachezaji mpira wengi sana wanafaidika na michezo mbali mbali ya mpira. Kwa hivyo, tuone kule tulikotoka zamani kuona vipaji vya soka katika nchi hii kama vilivyokuwa vya kina Abdul Wakati na kina Karume Mussa virudi. Nakipongeza sana Chama cha Mpira cha Zanzibar kwa dhati kabisa wa kuwa na mpango kabambe wa kupunguza utitiri wa vilabu katika *league* kuu ya Zanzibar, ili kuweza kutafuta wachezaji wenye uwezo katika vilabu 12 vitakavyoshiriki *league* ya Zanzibar kwa mwakani. Hakuna sababu lisobudi hutendwa, japo inaipa wakati mgumu vilabu vyetu, vilabu vyetu ni vya ridhaa havina udhamini tunapata shida. Lakini kwa nia hii tungeomba sana Mhe. Waziri uwaambie watustahamilie ili tucheze *league* yetu ndogo hii kwa kutafuta vilabu 12. Vilabu 6 Unguja na 6 Pemba tucheze *league* yetu ya Zanzibar yenye mvuto na kila mtu kuipenda *league* ile.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri ili mpira wetu tuucheze vizuri zaidi, tupange mpango maalum kuzipunguza timu za vikosi. Nimesema kwa nia safi kwamba timu za vikosi zimekuwa nyingi katika *league* yetu. Kuna timu za vikosi zisizopungua 6 au 7 ambapo ni nafasi yao kucheza mpira, lakini watafute mbinu angalau ya kuona angalau kikosi chao kimoja iwe timu *strong* ya kushindana na timu za mitaani. Tumeona muda mdogo tu jinsi mpira sasa hivi ulivyoshika hatamu katika nchi hii kwa kupitia timu zetu za Jang'ombe Boys na Taifa ya Jang'ombe, tumeona namna gani mpira unavyokua. Tunaona sasa hivi mpira wa Gulioni na Mlandege, tungetamani zaidi tuzione timu za Mwembeladu, Ujamaa, Small Simba na Kikwajuni katika *league* yetu ile tujuwe kweli zile timu za mitaani ambazo ndio timu pekee zenye washabiki na kusisimua katika mpira wetu, tofauti na timu za vikosi.

Mhe. Naibu Spika, timu za vikosi vyengine ni timu za ajira wamekwenda kule watu, kwa hivyo kama wamelazimishwa kucheza timu ile. Lakini mapenzi ya dhati zinatoka katika vilabu vya mitaani. Nakuomba sana Mhe. Waziri katika hilo uliangalie ili tuone ni utaratibu gani tunaweza kuvipunguza timu za vikosi, na kuziacha timu zetu za uraiani na kuona ni kwa namna gani mpira unachezwa. Nilisema niogelee hapo kidogo katika michezo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile niende katika suala zima la kumpongeza tena Rais au Serikali ya Zanzibar, kwa kuona dhana kamili ya kuturudishia uwanja wetu wa shimoni pale Uwanja wa Mau. Ni ukweli usiofichika japo umechelewa kwa miaka miwili au mwaka mmoja na nusu. Sasa hivi tunaona harakati zimeanza

za ujenzi hongereni sana katika hilo. Nafikiri baada ya mwaka mmoja na nusu tu basi Uwanja wa Mau unarudi kuliko vile ulivyokua na kuwa uwanja mzuri zaidi kwa kupotezea muda katika fani zetu za michezo. Nakupongeza sana Mhe. Waziri kwa kusimamia hilo. Najua wewe ni jembe uwezo unao, nguvu unazo Zanzibar itapiga hatua katika michezo hongera sana Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, nije katika Chama cha Wanyanya vitu vizito, Zanzibar *Weight Lifting*. Hiki chama ni chama pekee cha Zanzibar au kwa Tanzania kilichopata usajili katika Shirika la Kimataifa. Lakini chama hiki kimekuwa na kilio kukosa ruzuku, kinakosa ruzuku kinashindwa hata kushiriki katika vikao mbali mbali ambapo kinapaswa kushiriki chama hiki cha wanaonyanyua vitu vizito, pamoja na kusaidiwa kushiriki katika michezo, lakini ruzuku hakipatiwi fedha ili kuweza kulipa ada mbali mbali za shirikisho lile.

Kwa hivyo, ningekuomba sana Mhe. Naibu Spika, sana tume- *focus* kwenye *football*, kwenye natball na riadha. Lakini hiki chama cha wanaonyanyua vitu vizito kimeshatuletea sifa nyingi sana hapa Zanzibar. Ushahidi usiopingika walikuwepo hapa kina Hizdori na kina Marwa walikuwa wakinyanyua vyuma tumepata sifa nchi hii. Sasa hivi kile chama kipo na ni cha muda mrefu lakini ushiriki wake ni wa magomashi, hata kupata pesa za ada kulipa katika shirikisho lile limekuwa tatizo. Kwa hivyo, ningekuomba sana mheshimiwa na huku ukutupie jicho, kwa sababu kuna watu wengi sana katika chama hiki cha wanyanyua vitu vizito, ningekuomba sana mheshimiwa katika hili uliangalie kidhati *lillah* tuone kwamba michezo yetu tunaigawa angalau watu wengi sana wanaingia katika fani hiyo.

Mhe. Naibu Spika, niende katika suala la magazeti, naipongeza sana serikali kwa kuona kwamba kuanzia tarehe 9 kuamkia 10 gazeti la Zanzibar leo limeanza kutoka rasmi Zanzibar, kuchapishwa na Kiwanda chetu cha Uchapaji cha Serikali na kuingia Zanzibar. Lakini kumekuwa na changamoto, gazeti lile linachelewa au halifiki katika Mikoa ya Tanzania Bara, kama ilivyokua zamani inachapishwa Tanzania Bara. Tatizo ni nini najua utaniambia usafiri, maana yake magazeti yanachapishwa usiku yanamalizika pengine saa 10 au saa 9 huko, kuondosha usafiri kutoka hapa kupeleka mapema kufika katika soko imekuwa tatizo.

Kwa hivyo, nakuomba sana badala ya kutanua wigo wa kuchapisha Zanzibar, tuone kwamba hata katika soko tunaingia ili tuongeze kipato chetu sisi wenyewe Wazanzibari tofauti na pale ilipokuwa likichapishwa kule *TSJ* Dar es Salaam, lakini inaingia kwenye soko na sisi tunabakisha deni Tanzania Bara zaidi kubwa kuliko tukichapisha hapa. Mhe. Waziri ufanye rai kabisa katika

hilo ili tuone kwamba gazetu lile la Zanzibar linaendelea katika mfumo wake ule ule. Hata katika magazeti asubuhi katika redio Zanzibar, gazeti lile kwa upande wa Tanzania Bara halisomwi tokea tarehe 10 lilipoanza kuchapishwa Zanzibar limekuwa linasomwa hapa, na sio utaratibu kama lilivyokua. Anasoma mtangazaji wa Bara kule magazeti na lile linakuwemo, na Waswahili wanasema 'mcheza kwao hutunzwa' anaanza na gazeti la kwetu. Lakini leo hii Redio Zanzibar wanasoma magazeti gazeti lile halisomwi mwanzo katika Redio Zanzibar, na sio tu hata katika uandishi wa magazeti yetu yale, tujuwe kwa upande wa michezo, sisi bado tuna timu zetu za Zanzibar ambazo zinawavuta watu wengi sana.

Kwa mfano, Jang'ombe Boys na Taifa ya Jang'ombe wanakuwa na michezo mizuri kila siku. Basi inapokuwa kipindi chao kimefika basi tuzipe nafasi katika kurasa zetu za mbele, tusing'ang'anie Simba na Yanga tu, twende tukitukuze kilicho chetu tuwaone watu namna gani wanavutiwa na timu zetu za Zanzibar. Lakini leo hii gazeti lile anaandikwa zaidi Simba na Yanga zaidi kuliko timu zetu za Zanzibar ambazo sasa hivi zimetokezea kufanyakazi vizuri. Kwa hivyo, ningekuomba sana Mhe. Waziri uwaambie basi watu wako lazima wakitunze cha kwetu kionekane na chetu ni hicho. Jang'ombe Boys, Taifa ya Jang'ombe, Mlandege, Gulioni na vilabu vyengine ambavyo vinafanya vizuri. Kwa *page* ya michezo ni lazima tuziandike habari za Zanzibar kwa wingi, ili watu waweze kusoma kwamba kweli sasa hivi Zanzibar wamejidhatiti kufanyakazi katika mpira na kuona kwamba inapiga hatua ili kusogea mbele.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele nizungumzie juu ya suala la mjenzi wa *ZBC* Pemba *Ayoub Building Company*, imekuwa kilio cha muda mrefu sana anadai wizara yako. Kwa hivyo, ningeomba sana hicho kilichobakia alipwe. Nasikia imetokea tatizo sasa hivi anaambiwa kwamba hana mkataba sijui vipi. Aliweza kulipwa vipi mwanzo na sasa hivi iwe vigumu aambiwe hana mkataba, hilo haliingii akilini katika hicho. Ningekuomba sana ile *balance* yao iliyobakia hao watu wa *Ayoub Company* waliofanyiwa ukarabati kule Pemba wapatiwe pesa zao. Siku zote tunahimizana jasho la mnyonge lisifike kukauka mtu apate malipo yake. Kwa hivyo, ningekuomba sana Mhe. Waziri, najua waziri uwezo unao ni mweleweshaji mzuri, maalim Rashid mwalimu wangu, utajitahidi ili tuone tunapiga hatua katika suala hilo ili kumaliza migogoro midogo midogo isiyokuwa ya lazima.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele katika suala hilo hilo, kuna kilio cha muda mrefu nililia sana na nitaendelea kulia sitonyamaza katika kilio chetu. Viwanja vyetu vya Mnazi Mmoja, naipongeza sana serikali kwa namna ilivyokarabati ule uwanja haukai maji, sawa vizuri. Lakini bado baadhi ya

sehemu haziwezi kusibika tena na mipira, kwa hivyo ule ujenzi uliofanyika pale na *ZUSP* bado wakarabati juu ya ile mifiniko ya ma- *chamber* yale, ili iwe kama zamani vichezwe mpira viwanja vile. Uwanja wa Jeshi umekufa kabisa pale kwa sababu ya ule mtaro uliopita pale nyuma yao imekuwa hata vile viwanja haviwezi kutumika tena. Kwa hivyo, ningeomba najua ujenzi bado haujakamilika vizuri, lakini najua serikali yangu sikivu na italifanyia kazi suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, sio hilo tu, hata kuondoa maguzo ya umeme katika viwanja. Mhe. Waziri suala la nguzo za umeme kwangu mimi ni changamoto kubwa, kwa sababu ukumbuke viwanja vile vilikuwa vitupu havikuwa na hata kipande kimoja cha nguzo zaidi ya magoli. Leo hii badala ya kucheza mpira mtu na mtu basi anacheza mpira mtu na nguzo, pembeni ukipigwa mpira mara unaweza kujigonga na nguzo, hatuendi huko na nyinyi mmesema kwamba tunaelekea katika *FIFA*. Kwa hivyo, ningekuomba sana utumie ueledi wako, najua tulihangaika sana mimi na wewe pamoja kuona zile nguzo tunaziondoa, lakini imeshindikana sijui tatizo liko wapi. Nimeshauliza swali mara nyingi sana, tumeambiwa inaharibu mazingira, sasa kuharibu mazingira kuondoshwa nguzo au kuwekwa nguzo katika viwanja ambavyo havistahiki kuwekwa nguzo. Ingekuwa ni mpira wa *rugby* ningekubali kwa sababu ndio magoli yale, lakini kwa sababu sio mpira wa *rugby football*, magoli yake hayana urefu ule, ningekuomba sana tuchukuwe jitihada tusikae tukachekwa na kila mtu, wanakuja watu wanatushangaa katika viwanja vizuri kama hivi tulivyokuwanavyo, leo hii vinakuwa na maguzo ya umeme.

Mhe. Naibu Spika, najua serikali imefanya kwa nia safi kabisa, lakini zile nguzo pale sio pahala pake, zingewezekana hata zikang'olewa zikawekwa juu zaidi barabarani ingekuwa vizuri zaidi kuliko kwenye viwanja. Tulisema na tukapiga kelele sana lakini imeondoshwa nguzo moja katika uwanja wa *black fighter* hiyo ndio iliyoonekana inakera, lakini nguzo zote zilizokuwemo mule zinakera na zinasumbua. Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Naibu Spika, ili michezo hii iendelee basi miundombinu ya michezo iheshimiwe, tuiheshimu miundombinu ya michezo nguzo katika viwanja vya Mnazi Mmoja, viwanja vya Evaton kuna Stonvilla huko pembeni ya Gofu, vile viwanja sasa hivi vimekufa imekuwa ni darasa la kufundishiana magari badala ya viwanja vya mpira. Viwanja vile vimetoa wachezaji wazuri katika nchi hii, lakini leo hii vile viwanja vimekuwa vinapangwa maringi na kuwekwa maguzo watu wanafundishiana magari. Tunapoteza lego zima la uboreshaji wa michezo hususan kwa mpira wa miguu katika viwanja vyetu.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana viheshimiwe viwanja vya mpira ili tuweze kufufua vipaji zaidi Zanzibar sasa hivi tunaingia kwenye shirikisho la mpira wa Afrika ili tuone kwamba tunatoa vipaji kweli. Naishukuru na naipongeza sana timu yetu ya Serengeti Boys kule Gabon ilikokuweko, najua mule muna Wazanzibari wawili wanashiriki unaona namna gani jinsi Zanzibar walivyopiga hatua katika fani ya mpira. Wako vijana wawili wanashiriki mmoja wapo ni wa Jang'ombe Boys yuko kule na mwengine sijui wa timu gani. Kwa hivyo, ningeomba nafasi ile viwanja vile viheshimike ili tuweze kutoa wachezaji wengi zaidi katika mashindano mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika suala la mapato. Nimepitia kidogo tu hili suala nimepata mkanganyiko nikiangalia bajeti ya 2016/2017 na 2017/2018. Kwa hivyo, nimepata ukakasi kidogo kuona kwamba Baraza la Michezo kwa wakati ule 2016/2017 ilitengewa karibuni milioni 84, 000,000/-lakini sasa hivi imetengewa milioni 70,900,000/-. Jaribu kuangalia je, tuna dhama ya kweli ya kuibua michezo, badala ya maisha kwenda mbele sisi tunarudi nyuma. Sasa haiwezekani mtu ukapungua umri badala ya kuongezeka umri. Tuone makusudi mazima, labda ukija nifahamishe imekuwaje Baraza hili la Michezo limetengewa milioni 84,000,000/- katika mwaka 2016/2017, lakini katika mwaka 2017/2018 imetengewa milioni 70,900,000/-. Kwa kweli naona kama kidogo hapa sifahamu, kwa sababu gharama kila siku zinaongezeka, lakini katika matumizi ya bajeti hii imepunguzwa. Je, ni kweli tunataka tushiriki katika michezo mbali mbali au tunakwenda katika mambo yetu tunayoyapenda sisi katika siasa. Nilitaka niseme hayo machache katika suala hilo la michezo.

Lakini vile vile naona kama narudia nyuma kwa sababu imeshikwa sana hii na suala la michezo, wasi wasi wangu mkubwa sisi kama viongozi, tunaomba basi tuheshimu michezo hususan mpira wa miguu. Mpira wa miguu siku zote hauongozwi kwa busara na hekima, mpira wa miguu unaongozwa na kanuni na sheria. Hapa nyuma wakati bado hatujapata nafasi ya kuingia katika *CAF* ilikuwa inafika wakati vilabu vya upande mmoja vikishuka daraja, tunakwenda kupitisha siasa zetu hivi tutakosa kura namna gani tuombeni sasa hivi kule tuondoke, kule tuondoke tuwachie sheria na kanuni zichukuwe nafasi yake katika mpira ili mpira uchezwe na nafasi tayari tumeshaianza hiyo ya kwenda zetu *CAF*, basi tuheshimu sana ili tuone tunafanikiwa katika hilo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilitaka niseme hayo machache tu, sina mengine ya kuongeza isipokuwa nasema kwamba naunga mkono hoja ofisi hii. Lakini la mwisho kidogo mheshimiwa samahani. Suala la *ZBC2*, nataka kujua Mhe. Waziri utakapokuja unijibu *ZBC2* nini tatizo lake, ile inaoneshwa katika channel ya Azam TV kule. Je. tumemuuzia, tumemkodisha au tumemgaia

tujuwe. Au pengine kwa ihisani yake watasema tukusaidieni kwa sababu hamuonekani katika *satellite*, pia inawezekana unifahamishe kama tumemuuzia tumefaidika vipi kama serikali kwa upande wa *ZBC2*, na kama tumemkodisha tu basi mje mtuambie ili tuone angalau mikataba yake, mkataba huu umekuwa vipi.

Lakini hapo hapo kusema kwamba *ZBC* ni *domestic television,* inakuwaje katika king'amuzi kile inapomalizika pesa yako kishindwe kuonekana *free*. Kwa sababu katika sheria zenu nyinyi za *broadcasting* mnaamua kwamba *domestic* televisheni zote zitapatikana *free*.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, una dakika moja kumalizia.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante namalizia. *Domestic* televisheni zote zinapatikana *free*. Iweje *ZBC* unapomaliza *package* yako tu pale inakatika unakuwa huoni. Nilitaka niseme hayo Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii, naunga mkono kwa asilimia 99 hotuba hii na inabakia asilimia moja, Mhe. Waziri najua utanijibu vizuri ili niweze kukuachia. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ajitayarishe Mhe. Mwantatu Mbaraka na baadae atafuata Mhe. Suleiman Sarahan.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subuhanahu Wataala* Muumba Mbingu na Ardhi, na aliyeniwezesha kusimama hapa kwa uwezo wake wala sio akili zangu wala ujanja wangu ni neema zake Mwenyezi Mungu, natakiwa kushukuru kwa kusema *Alhamdulillah*.

Mhe. Naibu Spika, wengine sasa hivi wanakata roho, wengine wanazaliwa, wengine wanavua na wengine wako katika kutafuta riziki ndio neema zake *Allah Subhanahu Wataala.*

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa sijakutendea haki kama sijakushukuru wewe uliyenipa ruhusa hii ya kuchangia na ungeweza hata kunikatalia wewe ndio mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kumshukuru sana Dk. Ali Mohammed Shein tena na tena, kwa uteuzi alioufanya kwa Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Mhe. maalim Rashid niseme hakukosea, kwa upande wangu. Kila

mmoja anasimamia analoliona, niombe ku-*declare interest* Mhe. Naibu Spika, mimi ni mjumbe wa kamati hii halali, mengi nimeyaona katika kamati hii.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kuwashukuru sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa wizara hii, katika kamati hii ilivyofanya kazi kwa mashirikiano makubwa waliotuonesha.

Mhe. Spika, niendelee kumpongeza Waziri kwa kutekeleza kwa asilimia kubwa ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi na sio kwa mdomo kwa vitendo, Mhe. Waziri hongera sana na nimuombe Mhe. Waziri Salama Aboud anayesimamia ilani lakini aendelee kuisimamia vile vile kwa vitendo nasema kwa nini? Wananchi wa Michamvi mpaka leo wanasikia tu ilani ya Chama cha Mapinduzi kwenye vyombo vya habari, kwenye Redio lakini kwa vitendo hawajaiona tokea dunia ilipoanzwa hadi leo hii imo humu ndani maji Michamvi hawajapata. Ukitizama kule kuna wawekezaji wa mahoteli makubwa. Kwa hivyo nikuombe tu Waziri Mhe. Salama Aboud jitahidi angalau wananchi kule waione ilani hii ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo baada ya kusikia tu kwenye vyombo vya habari wanahitaji maji na ukizingatia wakati huu wa mvua, kipindu hatari kubwa na vile vile tumpe heshima Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Ikulu ndio anakotokea kule.

Mhe. Spika, baada ya hapo nizungumze mafanikio ya kipindi kifupi tu alichokamata Mhe. Waziri. Kwanza uwanja wa Gombani Mhe. Waziri nikuopongeze kwa dhati kabisa kazi uliyofanya sisi tumeiona, umetandika nyasi mle ambapo naamini uwanja wa Amani hazipo nyasi zile jambo la kupongezwa sana Mhe. Waziri, tofauti na hapo nyuma Serikali imekula hasara katika Uwanja wa Gombani umetandika *tartan* ya kimataifa Mhe. Waziri.

La pili hatua kubwa uliiyoifanya na kwa mujibu wa ilani ya Chama cha Mapinduzi wajumbe mkipata nafasi au mkipata siku Kigogani Mhe. Waziri anajenga uwanja wa kileo wa Wilaya ya Kusini Kitogani, ni jambo la kupongeza sana. Ndio nikasema ukimchukua mtu mchukue na sababu, ukimpenda mtu tuwe na sababu umpendea vipi haya ndio anayofanya Waziri. Nimshukuru Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein anafuatilia suala hili kwa umakini wa hali ya juu mimi nalijua kwa hivyo Mhe. Waziri jitihada unazofanya tunaziona, leo kuna uwanja pale unakwenda kwa *speed* ya hali ya juu na usije ukarudi nyuma haya ndio mafanikio yako Mhe. Waziri.

La tatu ulisema ndani ya Baraza humu kuhusu uwanja wa Mao leo tupite tukaone hali ya Uwanja wa Mao uko vipi? Waziri umefanya kazi wewe kwa kipindi kifupi sana, mimi nafikiri hata ofisini hukai unapiga kazi tu nje uko,

kazi kubwa uwanja ule pale umezungumza ndani ya Baraza humu na uongozi ndio huu tusiseme kwa mdomo tu vitendo vinataka vifanyike, kwa hivyo nakupongeza sana.

Jengine Waheshimiwa Wajumbe na wananchi *Academy* nafikiri imo katika ilani tayari tunaiona sasa hivi inaendelea vizuri jengine kubwa zaidi niwashukuru wote Serikali ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzbar, kwa uanachama wa *CAF* na hapa niendelee kumshukuru sana Ndugu yangu Nape Nnauye sana tena sana. Naijua hii siri ya kufika wanachama mengine mwalimu hawezi kuyajua ninavyojua mimi kupata uanachama huu wa mpira wa miguu wa *CAF*. Maalim tulikuwa tukihangaika kwa muda mrefu sifa hizi itabidi uzipate wewe tu maalim Rashid kunwa Mwalimu na maalim tofauti. Waziri umefanya kazi kubwa hapa sifa kubwa umeifanya hapa watu miaka na miaka wanahangaika na uanachama huu jitihada zako zimeonekana pamoja na wote walioshiriki kazi kubwa sana sana Mwalimu umeifanya.

Baada ya hapo kulikuwa kuna kilio cha muda mrefu cha wafanyakazi wetu *wa ZBC* kila mwaka huja wakitwita mimi ni mmoja wao wanaoniita sijasikia manung'uniko hayo inaonekana kungali salama. Kwa hivyo Waziri umefanya jitihada kubwa Mhe. Waziri mimi sijasikia ikifika wakati wa bajeti hii huwa tunaitwa wanatueleza matatizo yao mimi sijakisikia kwa hivyo inaonekana kungali salama, nafikiri likizo zao wanazipata kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije katika ukurasa huu sijui hapa niseme Waziri umejitakia mwenyewe au vipi maana yake hapa mimi nimeona umekusaya pesa nyingi katika Kamisheni ya Utalii umevuka lengo, sasa inaonekana kama unataka kutiwa adabu sasa kutokana na jitihada zako ulizofanya. Ukarasa wa 57 nafikiri kama hivi umekusanya bilioni ngapi katika Kamisheni ya Utalii, sasa hivi unatakiwa ukakusanye bilioni nne hii watakuonea Mhe. Waziri hii *speed* kubwa wanataka kukupelekesha. Ndio wanakuona mchapa kazi na hii kutokana na jitihada zako ndio maana wakaona aa huyu ni Waziri makini kweli kweli tumuongezee mzigo huu ukurasa wa 59 ulipoambia ukusanye bilioni nne kitu kama hivi nilivyofahamu mimi.

Hii niwaombe wahusika akiwemo Waziri wa fedha aa mtamuumiza mapema Mhe. Waziri huyu msione kazi yote anayopiga ni kubwa ni kweli kubwa tunaiona na huyu uzuri wenyewe katokea kunako pesa alikuwa *ZRB* Mhe. Waziri. Sasa mapato haya yote yanakwenda *ZRB*, kwa mlipaji ikiwa Mhe. Ali Suleiman itabidi amtafute Mhe. Ali Suleiman wa pili au wa tatu mlipaji ndio yule yule, ng'ombe ni yule yule mmoja unakamua lita tatu za maziwa utamlazimisha lita sita tutakuja kuua. Kwa hapa sina nia ya kutaka kuja kuzuia

kifungu, mimi nilizungumza kabisa ni mjumbe wa kamati hii mengi nimezungumza kwenye kamati, lakini hili nitalihoji na nikipata maelezo nitaliachia.

Mhe. Waziri hii kazi unayofanya kuliko Jet 540 tofauti na kupanda ndege yaCostal yenye injini moja kazi kubwa anayofanya Mhe. Waziri. Leo ukakusanye bilioni nne mlipaji ndio yule yule mtu mmoja au kesho uende kule kule *ZRB* wanataka kule kula aaa, hili nitalihoji Mhe. Waziri, wala sina nia ya kutaka kuja kuzuia fungu lakini nikipata maelezo nitaliachia.

Mhe. Waziri kuna migogoro ya *ZFA* na *BMZ* hapa pana mtihani na huu tukija tukiteleza uanachama huu utakuja kupotea tuwe makini na nataka nikuombe Mhe. Waziri kwa niaba ya kamati lazima ipatikane elimu ya kutosha kwa wajumbe wa Baraza hili ufanye siku utoe semina. Lakini mgogoro huu na nafasi hii tuliyoipata tukija tukiichezea itakuwa mtihani Mhe. Waziri ifike wakati tuelimishe hii migogoro ya Mahakama hii itatuathiri sana, tufike itolewe elimu ya kutosha tumepata kwa shida uanachama huu. Leo nchi kama Sudan, Nigeria, Angola ni fedha nyingi zinazopatikana katika mchezo wanachama, Tanzania Bara, Kenya ni jambo la kupongeza tu tusije tukaifanyia dharau hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilisema zamani nitakuwa sina mchango mkubwa kutokana na Wizara hii kwa vile ni Mjumbe wa Kamati hii nikupongeze sana Mhe. Waziri, na niombe Mhe. Naibu Spika, kutokana na wajumbe kutokuwa kidogo tutumie kanuni ya 147 tumpitishie waziri mapema bajeti yake mapema leo hii, tuwekeni kanuni kando, hamna wachangiaji. Hiyo nikuombe sana Mhe. Naibu Spika, wachangiaji wakishamalizika tusiweke zege hailali Mhe. Naibu Spika, Wajumbe tuliokuwemo tunajiona humu tumpitishie leo ili akampuzike na watendaji wake. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Jaku, lakini hayo maamuzi yanaweza kufanywa na Mhe. Spika, pamoja na Baraza lenyewe, kwa hivyo tumuachie Mhe. Spika, maamuzi hayo. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Mwantatu, baada ya Mhe. Mwantatu atafuata Mhe. Suleiman Sarahan na ajitayarishe Mhe. Hidaya. Mhe. Mwantatu.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia machache hotuba hii ya Waziri wa Habari, Utalii Utamaduni na Michezo. Kabla ya kuanza na mchango wangu kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote wa Wizara hii kwa kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu vile vile kuweza kufikia malengo makubwa kama

alivyotangulia kusema Mhe. Jaku kwamba kwa kweli Mhe. Waziri na watendaji wake wanajitahidi sana na mtu sifa yake apewe.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia niipongeze kamati kwa kuweza kuwasilisha ripoti ambayo itatusaidia sisi wachangiaji kuweza kupata uwelewa mpana na kuweza kuchangia kwa ufanisi zaidi, baada ya pongezi hizo Mhe. Nabu Spika, naomba nianze mchango wangu ukurasa wa 9 kifungu cha 19. Mhe. Naibu Spika, naomba ninukuu:

Kifungu cha 19 kinasema:

> "Katika kuhakikisha maeneo yaliyoainishwa katika program ya kuendeleza utalii yanatekelezwa kwa ufanisi Wizara imelipia gharama ya mabanda ya maonyesho ya Zanzibar yaliyokuwepo Dubai na Ujerumani kwa lengo la kutoa fursa kwa Wazanzibari kuendelea kutangaza bidhaa na huduma za utalii".

Mhe. Naibu Spika, mimi hapa ningelimuomba tu Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho atueleze ni kiasi gani cha fedha kilicholipiwa gharama hizi za mabanda yaliyoko Dubai na Ujerumani, lakini vile vile itakuwa ni vyema na faraja kwa wajumbe pamoja na wananchi kwa jumla akatueleza faida gani inapatikana kutokana na mabanda hayo.

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 12 kifungu cha 26, kifungu hichi Mhe. Naibu Spika, kinaelezea Shirika la Utangazaji limefanikiwa kurusha hewani vipindi mbali mbali vikiwemo vya unyanyasaji wa kijinsia, rushwa, ijue sheria pamoja na masuala mengine, lakini vile vile Shirika la Utangazaji huwa linatoa matangazo mbalimbali ambayo yanaelimisha umma juu ya mambo ambayo yanawahusu jamii kwa ujumla. Lakini matangazo yale naamini huwa kuna watu ambao wanayapima na kuyachuja.

Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi nimesikitishwa na tangazo moja kwa vile sisi huwa tunapinga huu udhalilishaji kuna tangazo ambalo linaendelea katika *ZBC* tangazo hili kwa upande wangu mimi kama mwanamke nahisi kidogo limemdhalilisha mwanamke, tangazo lenyewe anaonyeshwa mwanamke anatoa mishumaa anampa mtoto aweke mle ndani wakati wazazi wanaondoka. Kiasi cha kwamba anaonekana mwanamke hana akili na hiyo si kweli mwanamke ni mtu ambaye anachukua tahadhari kubwa katika familia. Hivyo kwa mtizamo wangu mimi nahisi tangazo lile halikumtendea haki mwanamke. Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe.Waziri pamoja na watendaji wake wote kuangalia kwa

kina yale matangazo ambayo yatawasilisha pamoja na kuchuja ni athari gani itapatikana ili isiweze kumkwaza mtu mwengine.

Nikiendelea niende ukurasa wa 14 kifungu cha 29 kifungu hichi kinaelezea kuwa Idara imeweza kusajili vijarida wamevitaja hapo, aidha imechapisha na kusambaza vitambulisho vya waandishi wa habari. Lakini vile vile kwa kutumia gari la sinema Idara imeweza kufikia vijiji kuonesha filamu tofauti tofauti wakavitaja vijiji vilivyokuwemo hapa, baada ya kuangalia mimi nikaona kwamba hawakuweza kufika katika maeneo yote ya Zanzibar. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri akija atueleze kuna mpango gani kwa yale maeneo ambayo hayajaanza kufikiwa kwa sababu haya yote yaliyoelezwa yaliyoenda kuoneshwa kule ni muhimu kwa jamii.

Lakini vile vile naona ni busara kwa Mhe. Waziri nimshauri kwamba katika yale maonyesho ambayo wanakwenda kuelimisha kule kwa jamii watumie fursa hii kuonesha filamu ambazo zitaonyesha athari za udhalilishaji kwa jamii. Kwa vile wao moja kwa moja wanakwenda kukutana na jamii itakuwa ni busara sana wakifika katika jamii, kwa sababu udhalilishaji unafanyika zaidi kule chini ndani ya jamii husika kwa hivyo itakuwa ni vyema kutumia fursa hii. Lakini vile vile tutumie fursa hii kuelimisha jamii juu ya athari za utumiaji wa madawa ya kulevya ili kuokoa jamii yetu na kupunguza ongezeko la vitendo hivi ambavyo vinaleta shida sana katika jamii zetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuendelea niende ukurasa wa 23 kifungu cha 50, kifungu hichi kinaelezea jinsi Wizara ilivyojipanga kutoa mafunzo yaliyohusiana na ujengaji wa maadili kwa wanafunzi wa skuli za msingi na namna bora ya kuibua vipaji vya sanaa kwa wanafunzi hao. Mimi nimuulize tu Mhe. Waziri suala dogo aje atueleweshe. Je, Wizara ina mpango gani wa kutoa elimu hiyo kwa mikoa mingine kwa sababu inaonekana fika kwamba kuna mikoa mingine kama Mkoa wa Mjini Magharibi ambao una idaidi kubwa ya watu haujafikiwa. Lakini vile vile itakuwa ni vyema kama atatueleza kupitia program hii Wizara iliweza kutumia kiadi gani.

Mhe. Naibu Spika, nirudi ukurasa wa 21 katika uendelezaji wa ukuzaji wa shughuli za utamaduni kwa wananchi, hapa nimshauri tu Mhe. Waziri kwamba tunaelewa huko vijijini kuna tamaduni mbali mbali zikiwemo ngoma mbali mbali na masuala mengine ya utamaduni katika maeneo yetu. Hivyo ni busara kuimarisha zile tamaduni zilizomo katika maeneo yetu ikiwemo ngoma za asili ambazo huwa zinachezwa katika vijiji mbali mbali kama vile Nungwi na maeneo mengine Makunduchi na maeneo mengine. Kwa hivyo tuweze kudumisha ule utamaduni ili wasije wakaona kama ule utamaduni wao hauna

maana au zile ngoma zao hazitambuliki. Wakati mwengine ikitokea hata katika zile sherehe zetu tuweze kuchukua watu wenyewe ambao wanacheza ile ngoma na kuacha kuchukua wale ambao waigizaji, kwa sababu kuna kikundi chetu cha sanaa naamini ndio kinakuwa mara nyingi kinaigiza zile ngoma, lakini tuwachukue wale wenyewe hasa ili waweze na wao kujisikia kwamba ule utamaduni wao unaimarika.

Mhe. Naibu Spika, nije ukurasa wa 53 katika utekelezaji wa 2017/2018 Mhe. Naibu Spika, kuna *program* namba moja maendeleo ya habari na utangazaji, pamoja na jitihada za Mhe. Waziri ambazo amezichukua pamoja na kazi nzuri ambayo inafanywa na Wizara hii lakini bado kuna changamoto na kwa upande wangu mie changamoto hii naiona ni kubwa sana, Mhe. Waziri kama utakumbuka bajeti ya 2016/2017 nilizungumza hapa nikakwambia kwamba kuna haja ya kuajiriwa wakalimani wa lugha ya alama katika vyombo vyetu. Mhe. Waziri nikazungumzia vifungu vya mkataba wa kimataifa ambao umeridhiwa huu hapa na Tanzania naomba ninukuu ibara ya 8(1).

Kifungu kinasema:

> "Ili kuwawezesha watu wenye ulemavu waishi kwa uhuru na kushiriki kikamilifu katika hali zote za maisha nchi zilizoridhia mkataba huu zitachukua hatua zinazofaa kuhakikisha watu wenye ulemavu wanafika pahala au kupata kitu kwa misingi sawa na wengine kutokana na ulemavu wao wanawekewa mazingira ya kufika pahala kusafiri, kupata habari na kuwasiliana pamoja na teklonojia ya habari na mawasiliano na vifaa vya huduma vyengine zilizokuwa wazi au zinazotelewa kwa umma".

Mhe. Waziri kwa kweli hapa watu wenye ulemavu bado hawajatendea haki ya kutosha. Kwa sababu ni kweli jitihada mmechukua ya kuweka wakalimani, lakini wakalimani wale wanakuwepo pale wakati wa taarifa ya habari tu, kuna masuala mbali mbali ya umma kuna elimu mbali mbali za zinatolewa na wao wanatakiwa wazijue hawawezi kuzipata. Hadi sasa Wizara yako imeshindwa kuajiri wakalimani wa lugha ya alama jambo ambalo linapelekea kumkosesha haki mtu mwenye ulemavu, haki ya mawasiliano. Kwa maantiki hiyo Mhe. Waziri, nazuia shilingi kwa kifungu hichi mpaka utakaponipa majibu ambayo yataniridhisha, kwa sababu nitakuwa sijawatendea haki watu wenye ulemavu. Kifungu hiki kikipita bila ya kujua maslahi yao hasa katika upatikanaji haki ya habari, hasa ukizingatia Baraza hili lilipitisha Sheria Nam. 9 ya Mwaka 2006 inayosema haki na fursa kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Lakini vile vile, Sheria hii kifungu cha 15(1) kimesisitiza vituo vyote vya televisheni, vilivyosajiliwa Zanzibar vitatumia lugha ya alama au maelezo ya maandishi katika Taarifa zote za habari, vipindi vya elimu na vipindi vya matukio ya kitaifa. Mhe. Waziri, bado watu wenye walemavu hawajatendewa haki katika hapa. Taarifa ya Habari wapo na tunawaona lakini kwa nini labda uje utwambie, ni changamoto gani au kikwazo gani kinachopelekea watu wakalimani wa lugha ya alama wasiajiriwe, wakati wafanyakazi wengine watangazaji wanaajiriwa.

Mhe Naibu Spika, baada ya maelezo haya machache naunga mkono hoja hii kwa asilimia 90 na zilizobakia baada ya majibu ya Mhe. Waziri, yakiniridhisha basi sina matatizo nayo. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mwantatu, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Suleiman Sarahan baadae ajitayarishe Mhe. Hidaya na baada ya hapo atafuata Mhe. Abdalla Ali Kombo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru, Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia nafasi ya kuchangia Hotuba ya Wizara ya Habari, nataka nianze na Uwanja wa *Mao Tse Tung.* Mhe. Naibu Spika, mimi namzungumzia na Waziri kutoa angalizo tu, Uwanja wa *Mao Tse Tung*, Mheshimiwa mikataba mingi hii tumeiona wakati wa kuanza tunaanza na kasi na mbwembwe nyingi, lakini jahazi likizama tunamtafuta aliyerukia paka wa uso hajulikani. Mimi nilikuwa namwambia Mhe. Waziri katika ukurasa wake wa 5 katika kifungu cha 11 amelizungumzia suala la Uwanja wa Mao Tse Tung na amezungumza mengi kwamba mambo yameshaanza sawa, lakini pale uwanjani sijaona kama mambo yameanza zaidi ya kukatwa majani, sasa nimeona pesa ambazo amezungumza humu karibu pesa za wahisani karibu milioni 5.597 na pesa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo ni karibu milioni 400 lakini sasa najaribu kutafuta ufumbuzi wa uwanja atakapokuja Waziri atupe hesabu kamili ambayo uwanja huu utagharimu na pesa ambazo tayari ameshazipata ambazo zinataanza na huo ujenzi na vipi atuelezee uwanja huo utamalizika kwa muda gani ambao umepangwa.

Kwa hivyo, natoa angalizo kwamba uwanja huu usije kuwa kama uwanja wa ndege ukaja ukaombewa pesa mara tatu, kwa hivyo kama alivyo kuwa nnavyomuamini kwa mbwembwe zake, kwa hivyo mimi nilikuwa namtahadharisha na uwanja huu. Kwa sababu tusiwe kila mwaka tukaja kuwa na bajeti ya Uwanja wa *Mao Tse Tung* ulikuwa haumaliziki. Kwa hivyo atakapokuja atupe hesabu kamili ya Uwanja huu utamalizika vipi na muda gani ambao utamalizika na vipi amejitayarisha katika ukaguzi wa hatua kwa hatua,

kwa hivyo hapo nilikuwa na muomba Mhe. Waziri hilo lilikuwa suala ambalo lilikuwa nimshituwe kidogo.

Lakini nije katika suala la Ofisi Kuu ya Pemba Mhe. Wizara ya Habari Pemba bado nzito na nikisema nzito namaanisha kwamba siizungumzii zaidi, lakini sijaonapo tangazo la *ZBC* au matangazo zaidi ya uwelewa tu wa kichwani kwamba tuna *Channel* ya *ZBC*, lakini utangazaji wa majukumu hasa ya *ZBC* hatuyaoni, lakini jengine ni kwamba waandishi wake wa habari wa *ZBC* hawajukani.

Labda tunamjua mtu kwa jina kwa kuwa tunakaa Chake Chake, lakini hata vile viguo vya kuvaa vya *ZBC* pia hawana, sasa mji kama ule wa Chake Chake, ambao mji unakuwa na vitongoji vyake na Pemba kwa ujumla *ZBC* ikiwa ndo chombo tunachokiamini chenye habari za ukweli. Lakini unakuta habari zinazotoka pale anazichukua mtu *ITV* utaziona kwenye *ITV, ZBC* hawapo ukenda ukiuliza utaambiwa kamera imekwenda kwa Mhe. nani na tuna kamera moja. Mheshimiwa utakapokuja hapa hebu tueleze ukweli hawa wafanyakazi wako wa *ZBC* wana kamera ngapi na vyombo vya kupandia kufuata habari wanavyo vingapi, maana hapa hatujui tumkamate nani? Ukimkapata mtu wa *ZBC* akwambia sina usafiri, ukikamata Wizara nimepeleka pikipiki, nimepeleka makamera, bila ya kamera haiwezi kufanya kazi.

Sasa Mheshimiwa na wafanyakazi inaonekana kwanza ni kidogo hawatoshi, na inaonekana hasa kwamba kutokana na sababu zenyewe matukio yanayotokea Pemba hayaoneshwi. Matokeo haya yote yaliyokuwa yamepata maafa mpaka mtu *special* akachukuliwe wakati *ZBC* ni kazi yenu kutokana na kwamba ni chombo cha Serikali. Lazima tutangaze tu sio tupeleke harusi tu. Kwa hivyo nnachokiomba Mheshimiwa ukija utueleze hii Pemba umeipangia vipi kuhusu zana zake, ambazo usafiri pamoja na zana za kutendea kazi zinapatikana vizuri sana pamoja na magari wenyewe, lile gari lenyewe ambalo hili ni la *ZBC* Mheshimiwa kwa nini halibandiki matangazo anaogopewa nani? Au hamna gani hatuyaoni yale yakibandikwa *ZBC* ndio tunajua kama hii ndo *ZBC* lakini hamna kwa hivyo ningekuomba hebu ukija utueleze kidogo una mpango gani wa kule Pemba kuiboresha, maana hii hali kidogo haijakuwa ya kutosha kabisa.

Nyengine Mheshimiwa nilikuwa naulizia kuhusu habari ya Uwanja wa Gombani, Mhe. Uwanja kama ule wa Gombani si rahisi kuujenga tena kwa pesa zake ni uwanja mkubwa sana, lakini ule uwanja kila kukicha unachuka hadhi, hata ile milango yake haifunguliwi ile milango ambayo inakwenda kwa kufunguliwa watu labda ni mmoja au miwili mengine yote haifunguki tena.

Mheshimiwa ule uwanja si wakufanyiwa mas-hara unatakiwa ule uwanja uwe *services* ya kutosha, kitu chake kimoja kikiharibika ni nusu bajeti ya wizara yako. Ningekushauri sana ule uwanja ukaweza kutizamwa kwa hali ya juu ili visiachwe vitu mpaka vikawa havifunguki, baadae ikaja ikawa hatari mlango mmoja tu lile gati lake sijui limegharimu milioni ngapi? Kwa hivyo ningeshauri Uwanja wa Gombani na vile vile ningeshauri kwa nini uwanja huu haufanyiwi biashara, biashara ni mpira, biashara ni kodi ndogo ndogo lakini hautii tija kama tija mimi sioni.

Uwanja wa Gombani ni kitu kikubwa sana, sio rahisi kuwa na kitu kama kile ukashindwa kuona bajeti ndogo, ule uwanja unatakiwa utangazwe, unatakiwa ufanyiwe biashara lakini sasa sioni kama una biashara zaidi ya kucheza mpira timu ndogo ndogo na hamna chengine cha ziada. Ningeomba sana Uwanja wa Gombani Mheshimiwa ukautizama kwa jicho jengine, ukaufanyia biashara ya kutosha usije ukafikia kama hoteli zetu za kitalii mwisho tena zikaanguka kwa sababu hazivutii, ningeshauri sana Uwanja wa Gombani ukautangaza una kila aina *facility* kwa hivyo nahitaji matangazo. Lakini pia Mheshimiwa nikupongeze kwanza kwa kupata nafasi ya kuingia katika mashindano ya Kimataifa CAF hili lazma nikupongeze, niipongeze na Serikali nimpongeze na Rais Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa jitihada zake zote mpaka tukavikia hapa. *(Makofi)*

Malengo na mustakbali kabisa Mheshimiwa sio mlango tulioingilia tuje tutokee, bado malalamiko ya watu katika sehemu ya mpira wa miguu Mheshimiwa bado hatujajipanga. Maelekezo kabisa kuna watu wanatumia nafasi zao kwa kujinufaisha wenyewe. Huu mpira na nafasi hii ni ya kupigiwa mfano, tumehangaika nayo miaka mingi. Tusije tukafika wakati tumeshaipata nafasi kama ulompa mtu mkono ukenda ukampa mtu mkono wa pole, unampa unaacha ndio unatoka, lazima ukae na Kamati yao ambayo inachughulikia na mpira iache matatizo yake ya ubinafsi. Nafasi tuliokwisha ipata hii tuitumie vya kutosha na tuone faida yake. Lakini mimi nataka utakapokuja hapa, uje unieleze hizi ngoma za utamaduni zilizoko Zanzibar ni ngapi na zipi ambazo unazo katika mikakati yako, ambayo unazisaidia katika kufikisha lengo la utamaduni, maana kila mtu mwenye jadi yake ana ngoma lakini ni mpaka siku ya mavuno au siku ya harusi, lakini hazikuwekwa hizi ngoma au hizi tamaduni katika nafasi yake ya Uzanzibari.

Sasa ningeomba utakapokuja uje uniambie una ngoma za kiasili ambazo unakwenda nazo sambamba, ili wakati wowote wanapozihitaji ngoma hizi unazipata, lakini kitu cha pekee nataka kuulize huu mchezo wa ng'ombe umefikia wapi, huu ni mchezo wa asili ni mchezo unaotajikana na mchezo wa

kihistoria. Zanzibar sioni kwamba mchezo huu wa ng'ombe hupo si wakitaifa wala kimataifa wala wa Pemba, wala Mchanga Mdogo wala wa Pujini. Ningeomba Wizara hii ina mchezo huu wa ng'ombe wapi ambao umeutayarisha kama wa Wizara wanapouhitaji mchezo huu unapatikana. Kwa sababu huu mchezo, una ng'ombe, ng'ombe hawa wanatengenezwa na hawa wanaokuwa wanafunga ng'ombe ni wataalamu maalum sasa Serikali inawasaidiaje hawa, ng'ombe hawa wanapatikanaje, sasa wewe huwezi tu ukaja leo unataka mchezo wa ng'ombe ukaupata sio kama dume wa gari anachezwa ng'ombe.

Ng'ombe huyu anachezwa ana mbinu zake maalumu ana mchezo wake wa kumbaya ana kila kitu huyu ndio anachezwa. Kwa hivyo Serikali inawasaidiaje hawa, ukawaweka ukajua nina ng'ombe wangu kipolo, mashetani yake haya mbwembwe zake hizi, ukimtandika uwanjani unajua kama sasa ng'ombe kipolo anakuja, lakini hachukuliwi dume wa gari tu. Kwa hivyo ningekushauri Mheshimiwa, utakapokuja hapa una kikundi gani umekitayarisha. Na kama huna una mpango gani, kwa hivyo nikitaka kujua sababu mchezo wa ng'ombe Mheshimiwa ukiuwacha ukipotea huu halafu wale watu waliobakia wakifa, itakuwa mchezo umepotea. Kwa hivyo Mheshimiwa, ningeomba sana utakapokuja kidogo uwezo kutuambia habari nyengine, lakini nataka niseme kwamba kila siku tunapigia kelele kwamba Zanzibar ni nchi ya utalii Mheshimiwa, utalii Zanzibar mimi siufahamu kwamba tunaukuzaje. Kwa bahati njema na sisi tumeenda nchi za watu wenye watalii kila siku kwenye nchi ya utalii haitakiwi *week end*, nchi ya utalii haina habari ya *week end* siku zote ni *week end*.

Kwa mfano, tumekwenda Cuba, Cuba ni nchi ambayo ya kitalii na inategemea utalii na niliwahi kuongea na Waziri wa Habari kama wewe, anasema sasa hivi anategemea kuchukua watalii milioni tano kwa mwaka, wakati sisi mpaka sasa hivi tuna 100% tunachukua watu laki tatu sijui na ngapi watalii, wao wana milioni tano. Kwa hivyo tuangalie tuko wapi lakini utalii wao kila siku ule utamaduni wao, wanapiga mizinga yao, wanacheza ngoma zao kwa kila siku kwa hivyo sisi hapa tunaweka *disco week end*, hapa Mheshimiwa duu, samahani Mhe. Naibu Spika, nilikuwa sioni kidogo. Sasa nilikuwa nazungumza kwamba Waziri wa Habari, mimi ninachokuomba chukua ngoma zetu za utamaduni tuna Ngome Kongwe ambayo ile ni *indoor games* mambo ya ndani yale si mambo ya kukaa viwanjani, kila siku utalii wetu ukuzwe pale watalii wanapokuja wasiende Forodhani kula pweza, tuwatilie ngoma mule kila siku. *(Makofi)*

Ili tupate kujua kwamba utalii wetu, sasa utalii si kuja kuzunguka tu angalie na ngoma zetu . Sasa sisi, mtalii ni Forodhani akale pweza, lazima kila kwetu sisi iwe sikukuu kwa sababu hii ndio sasa hivi tumeifanya ndio pato letu kubwa. Kwa hivyo ningeshauri kwamba utalii wetu kuukuza ni kuhakikisha kwamba sisi hatuna wikiendi Zanzibar, jumatatu wikiendi, jumaane wikiendi, kutokana na starehe zenyewe zilivyo kwa hio lazima tukubaliane na hali ambayo tunakuza utalii wetu. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nilikuwa na mimi natoa wazo kwamba twataka kukuza utalii hebu tuukuze utalii ili tuweze kufikia malengo ambayo yapo.

Lakini, chengine Mhe. Naibu Spika, kidogo nilikuwa nasema kwenye ukurasa wa 19 kuna suala la kuhakikisha maeneo yaliyoainishwa katika programu ya kuendeleza utalii yanatekelezwa kwa ufanisi. Wizara imelipia gharama ya mabanda ya maonyesho ya Zanzibar yalikuwepo Dubai na Ujerumani, kwa lengo la kutoa fursa kwa Zanzibar kuendeleza kutangaza bidhaa za huduma za utalii, ili kuvutia watalii kutoka nje ya nchi kutembelea na kuongeza idadi ya watalii.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea ni kwamba hapa kuna mabanda umelipia lakini sikuona gharama za mabanda haya ambayo umelipia lakini pia nilikuwa nizungumzie kwamba kuna nchi nyingi ambazo, ulizitaja kwenye Kamisheni ya Utalii ilishiriki maonesho ya kimataifa ya utalii ikiwemo la *International Toursim Mass Both* la ITB la Ujerumani, *Would Travel Market* WTM Uingereza, *Arabian Travel Market* Dubai, *Interantional Rash* Urusi na nchi nyengine. Lakini mafanikio uliosema katika hapa, ulisema kwamba mafanikio hayo yameongezeka kwa idadi ya watalii waliokwenda Zanzibar kwa asilimia mia moja na nne, ambayo ina watalii 3,376,242 lakini Mheshimiwa, watalii waliokuja ni kutoka *Ukrain, Polland, Urusi, China, India* na *Israel.*

Wakati huku utalii tuliufanya Uingereza, Ujerumani, Dubai na Urusi, lakini watalii waliokuja ni wa aina yengine, ningekuomba uje ukija uniambie hata umewapata utafiti wa aina gani, mpaka ukawapata ukasema hawa wamekuja wakati sisi wageni wanaoingia hapa bado takwimu zao sio sahihi. Sasa sijui huku tulikwenda kujipeleka kwenda kutoa ushirikiano huu na hawa wageni waliokuja vipi hapa, kwa hivyo nilikuwa nikuombe. Lakini pia nikuulize utakapokuja kwamba jana niliona *clip* moja kule Uingereza katika mabasi fulani ya ndege ya Uturuki ikitangaza Zanzibar. Sijui na wewe umo mle katika *share* au wale wenzako wanakutangazia tu kwamba Zanzibar ina utalii utakapokuja unaweza ukasema kwamba na mimi nimo mle au mimi simo. Basi wenzako Waturuki wanakusaidia kukutangazia Zanzibar utalii wako.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niseme jengine kwamba wachezaji wetu tunaowaandaa kuendelea katika mashindani makubwa ya kimataifa pamoja na michezo yetu ya ndani, una kipimo cha kumpima mtu madawa ya kulevya kabla ya kumuandaa au tunampeleka hata akifike mbele ataonekana anatumia madawa ya kuleta itakuwa sisi keshatupotezea watu wetu, ameshatupoteza pesa zetu.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nikuombe hata timu zetu za mpira ambazo zinaingia ligi kuu vipi baada ya usajili wa wachezaji, je unavipimo vya kuwapima kama huna ununue kabisa. Ligi yetu ya hapa Zanzibar kunawachezaji wanavuta bangi, kuna wachezaji wanakula unga. Hawa nao wazuiwe hata ligi yetu ndogo wasicheze, hawana faida kwa sababu mtu kama huyo hata ukim-*promote* kitu gani haendi mbele asitupotezee muda. Kwa hivyo sasa hivi ningekuomba wachezaji wote watakaosajiliwa katika timu zetu zote za ligi Kuu ya Zanzibar wapimwe kama wanavuta unga wasiingie. Nakuomba sana utakapokuja uje unipe muelekeo wa hali hiyo.

Mhe. Naibu Spika, niongeze kwamba Wizara yako ni Wizara ambayo kukwambia kweli inasaidia pato kubwa la serikali yetu hata Waziri wa Fedha unamsaidia sana kupata pesa kupitia kwako. Lakini wewe kama Waziri pamoja na Wizara yako una maeneo mengi ya utalii, maeneo ya Mahoteli, maeneo ya wanamuziki, maeneo ya ngoma za asili. Hawa wenye Mahoteli wewe unawasidiaje kwenda kuwaongezea nguvu, kuwataka ushauri na wale waliokwama pengine imemshinda hoteli kuimaliza, wewe unamsaidiaje ukamwambia umekwama wapi nikusaidie ili hoteli hii ikiendelea na wewe upate faida na yeye apate faida, unafanyaje hapa. Kwa sababu wewe ni mdau mkubwa sio lazima uende pale mtu kumkamata kwa kodi, unatakiwa na wewe umsaidie sio uchukuwe kodi tu. Kama amekwama hoteli yake umeifunga unamfuataje huyo mtu ili kuweza kujua amekwama wapi, ili uweze kuisaidia kwamba hii sekta ndiyo ukuwaji wenyewe kama kuna hoteli kumi kesho kutwa kuwe na hoteli ishirini.

Mhe. Naibu Spika, ningekushauri pamoja na ngoma, pamoja na Mahoteli uwe unawafatilia hawa watu ili kujua kwamba wamekwama wapi na kama mara hii unaweza kusema utalii wangu umepungua vipi ili ukiulizwa ni kwa nini hoteli zimefungwa uweze kujua ni sababu gani, ujue kama hana maji, hana kitu gani au ameshindwa na nini, uweze kumsaidia. Ningeshauri kwa mkakati uliopo wa kuweza kukuza utalii zaidi unawasaidiaje hawa wafanyabiashara ili na wao waweze kufanikiwa katika mipangilio.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilitaka nije kwenye huu ugatuzi wa Chuo cha Utalii. Chuo cha Utalii umempa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Najua serikali imechukua hatua na maelekezo mengi ambayo tumesifia kutoka ugatuzi huu wa utalii kuupeleka katika lengo la mafunzo ya Amali. Lakini mimi ninachoona kwamba sifikirii kwamba suala la Chuo cha Utalii kiingia kwenye elimu ya mafunzo ya amali sijui kama inaendana pamoja. Sasa tusije tukafika pahala tukaweza kuchanganya mambo mawili ambayo ugatuzi wake ukaja ukawa haulingani na elimu yetu, ikawa sisi tunampandisha mtu renki ya kusoma elimu ya amali lakini Utalii ukawa sijui ukawa umefikia wapi. Nilikuwa nakuomba ulitizame kwa kina ingawa umeshamkabidhi masuala ambayo Mhe. Waziri atayazungumzia.

Mhe. Naibu Spika, mimi nizungumzie gazeti la Zanzibar Leo. Hili gazeti lilikuwa likichapishwa Bara. Mimi nataka utakapokuja uje unieleze kwamba hili gazeti likichapishwa Bara na likichapishwa Zanzibar gharama kubwa ni wapi. Wanapochapishwa Zanzibar ni rahisi au wanapochapishwa Bara ni rahisi. Mimi nataka nikwambie hili gazeti kama linaendeshwa kama gazeti la kibiashara kwa mfano nilionao mimi kwenye kichwa changu kwamba gazeti hili likichapishwa Bara ndio kwenye soko la watu wanaosoma magazeti, likitoka Alfajiri pale hata saa 3:00 asubuhi saa 4:00 liko Mikoa yote ya Bara ambalo linasomwa.

Mhe. Naibu Spika, Gazeti hili likichapishwa Zanzibar, litoke hapa na Boti ya asubuhi, saa 1:00 liingie Dar-es-Salaam, kule lichambuliwe liondoke saa 5:00 likifika huko litafika usiku au siku ya pili. Gazeti hili likiwa linataka kusimama kwa miguu yake ukija hapa unieleze gazeti hili litasimama vipi. Biashara ni watu na Zanzibar tunajua kwamba gazeti moja tunasoma watu 10, wala hatuna utamaduni wa kununua magazeti, tunajifunza. Lakini gazeti hili kama utali *promote* Zanzibar ukaliacha Bara kwamba lifanye kazi au lijiendeshe kibiashara, baada ya madeni unayodaiwa yataongezeka tena na mwisho utalifunga.

Mhe. Naibu Spika, ningeshauri ulitizame sio lazima ulichapishe Zanzibar wakati unafuata biashara. Utakapokuja hapa njoo unieleze hili gazeti likichapishwa Bara linaingia hasara au lina faida na likichapishwa Zanzibar lina hasara gani na faida gani. Sifikirii kwamba mpaka gazeti tulifunge ndio tuje tuone hasara. Kabla gazeti halijafungwa ulitizame hasara yake, gazeti likiuzwa Bara na wewe ukili-*print* hapa mpaka likifika Bara ni siku mbili halina litakuwa halina maana tena, hata zile *front page* ambazo zina maana zitakuwa zimeshachukuliwa na magazeti mengine.

Mhe. Naibu Spika, ningeshauri utakapokuja hapa uweze kutueleza kwamba hili gazeti lako wapi lina faida ili kama lina faida Bara mimi nitakushauri usiliondoe Bara kuchapishwa ili liendelee na faida ikiwa kama faida ipo Zanzibar basi lilete. Kwa hivyo nitakachokusihi utakapokuja uweze kutuelekeza nini habari itatuletea tija.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye maelezo uliyosema kuhusu habari ya maeneo ya kihistoria. Ukurasa wa 58 Mhe. Mwenyekiti, ulikuwa umesema kwamba katika kuhifadhi uenezaji maeneo ya kihistoria ya Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale umefanya matengenezo katika maeneo saba ya kihistoria ikiwemo Kijichi, ujenzi wa vyoo Mangapwani, kibanda cha kuuzia tiketi dunga, kuweka milango ya matengenezo na madirisha, kuliwekea uzio jengo la kihistoria la Chuini. Aidha matengenezo ya Makumbusho ya Pete kwa awamu ya Pili yamekamilika, uchimbaji wa kisima, kutia milango madirisha, kuwekeza bati, umeme umetaja vitu vingi. Kuna maeneo humu ambayo mimi sijayaona na hayo nayo yanakuongezea tija na wewe umesema umeshafanya utafiti.

Kuna kisima cha chini kwa chini cha Mangapwani sijakiona. Maeneo haya hayatangazwi, mtu wa Zanzibar ukimwambia kuna kisima cha chini kwa chini hakijui, Je, mtalii atakijua, kuna Mkamandume ana sifa zake alikuwa ana mguu mkubwa, ana kitanda hivi sijaona. Kuna kaburi la mwanamwari, sijaona, kuna msitu wa ngezi waliozama wale mashekhe, mamufti, sijaona. Sasa ningekushauri Mheshimiwa vyanzo vya kupatia pesa na vyanzo vya kuweza kuileta juu hii Zanzibar katika yale mambo ya kale hasa hujayataka.

Mhe. Naibu Spika, huyu Mkamandume anahistoria kubwa, katafute watu wakupeleke. Mheshimiwa njoo Pujini tukuonyeshe Mkamandume alivyokuwa katika historia yake. Twende kwenye kaburi la Mwanamwari. Kuna mwanamwari hapa amezikwa na mjauzito, yuko ndagoni twende tukakuoneshe. Msitu wa Ngezi kuna mashekhe wamedidimia, zile nafasi twendeni tukazi-*promote*, tusikae tu tukisema Beit-al-Ajaab halipo tena linavunjika, yapo haya mengine njooni. Sasa ningekushauri Mheshimiwa katika hali ambayo nakuona una *speed* nzuri ya kuweza kutaka kuleta hamasa kubwa njoo tukuonyeshe hizi historia nyengine zijengewe, watu watakuja Pemba watakuja kufata kuja kuangalia mwana mwari kazikwa vipi Mheshimiwa ninakuomba sana.

Mhe, Naibu Spika, kwa hivyo ningekushauri katika makadirio yako yaweze kutoa mwangaza ambao ungetusaidia katika mambo haya uliyoyataja humu yote. Lakini na haya yana kipaumbele sana mpaka pale tunaita katika baina ya Konde hata hujafika hapa kuna historia kubwa pale. Kuna msikiti wa chooko,

kuna kitu gani, lakini makumbusho haya yote hayapo. Sasa ningekushauri Mheshimiwa haya maeneo ukayaona na yakawekewa mabango makubwa na yakatangazwa katika maeneo mengi hata ukitunga katika kitabu chako ukitia mtu atataka kukuuliza yako wapi haya. Ningekushauri sana Mheshimiwa tukaweza kuendeleza hivyo.

Mhe. Naibu Spika, la ziada zaidi mimi nataka niangalie kwamba katika ukurasa wa kwanza kabisa ..

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa una dakika mbili za kumalizia.

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Usitie wasiwasi Mheshimiwa ikikaribia nambie tu. Baada ya shukurani mimi nataka nisema kwa kweli lazima niseme kitu kwamba Mhe. Waziri watu wanakusifu sana mpaka wafanyakazi wako wanakusifu sana. Hili dogo tu nataka nilisemee kwa upande wako. Wanakusifu uko hodari, msikivu, unafatilia, lakini bado wafanyakazi wako wanalalamika watendaji wako wengine wanawapiga pini kwa mambo tofauti. Sasa kwa sababu wamekusifu wewe nataka nikuombe uyafatilie haya masuala sina haja ya kukubagulia kwamba kuna nini.

Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi wa Idara ya Habari ndiyo wanaotutangaza sisi, wanayoitangaza Zanzibar, na niwaaminifu sana na serikali yao. Asiwe mtu wa Idara ya Habari anachukua mambo ya nje anavaa koti anainjoi ITV wakati yeye ni wa ZBC kila siku yuko hivi kwa nini wao ndio mwenye serikali. Hawa watanue vifua mbele na mwanamke wa ZBC avae vilivyondivyo sio avae mashungi tu, ajulikane huyu Mwandishi wa Habari wa ZBC. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nikupongeze kwa hilo wewe na Naibu wako Waziri mnaambiwa ni watu safi. Hawa waandishi wetu wa habari kila ukiwatizama unaona siku zote wamefunga, wanaonekana hawali sikukuu. Hawa wafanye siku zote iwe ni sikukuu, sasa hivi wanaringa na serikali yao. Kwa hivyo Mheshimiwa hawa wape kipaumbele, wapeleke Pemba kidogo waende warudi, wapandishe ndege warudi, ndio utalii wa mwandishi wa habari.

Mheshimiwa nakushukuru sana na naunga mkono hoja asilimia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Suleiman Sarahan, Waheshimiwa Wajumbe upande huu mnahangaika sana na hizo microphone zenu mara nyingi mkitajwa majina inabidi muanze kwenda ukizunguka huku na huku. Kwa sababu

mnazipiga sana meza na watu wa *control room* wameshasema tatizo ni kwamba mnapiga sana meza matokeo yake mnazi *disturb* hizo *system* za *microphone*. Sasa piga kofi moja dogo tu linatosha, tunaendelea.

Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Hidaya Ali Makame na baada ya hapo Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) ameniomba dakika tano, nitakuomba uzitumie hizo hizo dakika tano kwa sababu ya dharura yako halafu baadaye nitampisha Mhe. Abdalla Ali Kombo. Mhe. Hidaya karibu.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa na mimi kuweza kuchangia machache juu ya hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia leo kukutana tena katika Ukumbi wetu huu tukiwa katika hali ya uzima na afya. Tumuombe Mwenyezi Mungu atujaalie kila la kheri katika kazi zetu hizi ili tuweze kumaliza kwa salama na amani.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile leo tunachangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, nafikiri pia katika sisi wachangiaji itakuwa itakuwa kuna haja ya kuziingiza zile lahaja za kwenye utamaduni wetu hasa kule tunakotokea. Kwa hivyo leo kiingia kile kilugha msishangae ndiyo utamaduni.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanzia mimi nianze moja kwa moja kwenye suala la kukuza lugha yetu ya kiswahili ikiwa ni moja ya utamaduni wetu. Lugha yetu ya kiswahili kuna haja sana ya kuipa kipaumbele na kuitangaza ulimwenguni kote kwa kupitia vyombo vyetu vya habari pia kwa kupitia midomo yetu lakini pia kupitia utamaduni wetu wa kivazi.

Mhe. Naibu Spika, lugha yetu ya kiswahili ulimwenguni kote imewekwa kipaumbele kwa sababu kiswahili ni mama wa lugha nyingi kwani imeiba kila aina ya lugha. Kiswahili ni lugha yetu lakini tunapokitumia kiswahili wengi wao tunakuwa tunakipotosha kwa kutumia baadhi ya lugha lakini kwa kutumia pia baadhi ya maneno tukachanganya kwenye kiswahili chetu. Kwa hivyo ningemuomba sana Mhe, Waziri tuweke utamaduni wa kuitumia hii lugha yetu kikamilifu ili iweze kufahamika nje na ndani na kwa wale wageni ambao wanakuja kujifunza lugha hii basi waonekane wanafundishwa lugha hii ya kiswahili ili na wao waweze kukizungumza hichi kiswahili.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia kwenye mitandao mingi utaona kuna nchi tofauti zinafundisha hichi kiswahili, lakini kwa kweli kiswahili hichi ambacho utakikuta mle kinafundishwa ni tofauti na kile Kiswahili ambacho wenyewe

waswahili tunakijua. Ningemuomba sana Mhe. Waziri tukaipa kipaumbele hii lugha yetu ya kiswahili, ndani ya vyombo vyetu vya habari lakini pia kwenye mitandao ya jamii tukaweza kukizungumza hichi kiswahili halisi, sanifu na tukaweza kukitumia ipasavyo na hawa wageni ambao wanakuja kujifunza na wao wakaweza kukitumia vile inavyotakiwa na vile kiliyo kwa kupewa kiswahili ambacho hakifahamiki na watu wengine kutoka sehemu za nchi mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, pia niende kwenye ukurasa wa 17 Mhe. Waziri katika hotuba yake hii ametwambia kwamba Chuo cha Uwandishi wa Habari katika mwaka wa masomo huu wa 2016/17, kimepata udahili wa wanafunzi 248. Mhe. Waziri katika wanafunzi hawa ambao wamepata udahili huo hujatufafanulia kama kunawanawake wangapi na wanaume wangapi. Ningekuomba sana utakapokuja kwenye maelezo yako utufafanulie ili tuweze kufahamu kwamba hawa wanafunzi waliodahiliwa hapo wanawake wangapi na wanaume wangapi. Pia ukitoa hiyo utwambie ni wazalendo wangapi ambao ndani ya mwaka huu 2016/17 wameingia kwenye chuo hicho cha uwandishi wa habari na kuweza kupata mafunzo kama haya uliyoyataja hapa yakiwemo hasa ya vitendo.

Mhe. Naibu Spika, nikimaliza hapo niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa 23 Mhe. Waziri ametwambia kwamba Baraza limetoa leseni 68. Mhe. Waziri mimi kwa kweli hapa ulinifurahisha sana ulipokitaja kikundi cha Mchikicho Nungwi. Katika vikundi vya sanaa ambavyo vimepatiwa vibali au leseni na kikundi changu kiwamo. Kwa vile kikundi changu kiwamo umanifurahisha asilimia mia moja. Mhe. Waziri Kikundi hichi kwa kweli ulimwengu huu wa Unguja na Pemba hakuna hata mtu mmoja ambaye hakiji au hakijui. Kwa sababu Kikundi cha Mchikicho tunakijua sote na tunakiona katika shughuli zetu mbali mbali kinatumiliwa na kinafanya kazi ipasavyo kwa kweli kinanufaisha Wazanzibari wengi yaani kulipa jina la umarufu gani mkubwa kwa kupitia kikundi hiki cha Michikicho la kweli Mhe. Waziri kikundi hiki kinasitisha ingawa ndio kushaandika hapa kuwa nacho kimepatiwa leseni lakini hiyo leseni haijawa kuwa ndio jambo maana leseni ndo leseni tu. *(Makofi)*

Sasa ikiwa leseni itabidi ishughulikiwe hii leseni ili hichi kikundi kiwe na miguu na mikono na vidole viweze kufanya kazi maana leseni itakuwa ni kipande tu cha karatasi, lakini ili vikundi hivi vifanye kazi inavyopaswa basi Mhe. Waziri kuna haja kubwa sana hapa uvitizame vikundi hivi vya utamaduni vinavyofanyia kazi Zanzibar yetu hii vikaleta nuru, vikaleta umaarufu katika nchi yetu hii, vionekane. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa ufahamu wangu mimi hivi vikundi si cha Mchikicho tu maana hiki cha Mchikikicho kina ngoma mbili nikwambie kwamba kina ngoma ya Mchikicho, lakini pia kina ngoma ya Mkurungo ambayo ni maarufu sana nayo, kila mtu ngoma hii nayo kaijua ngoma ya Mkurungu, kwa hivyo Mchikicho ikawekwa na Mkurungu mambo hufana na yakishafana kila mtu anajua. Kwa hiyo leseni tayari zishatoka lakini kuna mambo mengine pia mambo yanastahiki kupatiwa hivi vikundi.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka kulikuwa kuna vikundi vingi kikiwemo kikundi cha Imarisha kilikuwa Amali pale kuna wale kina mama walokuwa wanaimba zile ngoma za utamaduni. Lakini pia kulikuwa kuna kikundi huko Makunduchi kile kikundi kwa kweli kilikuwa kizuri sana nacho kilikuwa kinaimba nyimbo zake, wao hawataki ngoma za nini hiyo midomo yao pia ilikuwa inatosha. Lakini vikundi hivi tulikuwa tunaviona vinavyotumbuiza na sote tukafurahika kwenye redio zetu Zanzibar na redio nyengine pia walikuwa wanatuiga kwa kupitia vikundi hivi hivi na ngoma zetu hizi hizi.

Lakini hivi vikundi vyengine baadhi vimeshakufa kutokana na kwamba huu ushuhulikiaji au huu utunzaji haupo unakufa. Kwa hivyo kama unakufa na hivi vyengine ambavyo vishapewa hizo leseni kama havikushughulikiwa baba yangu navyo vitakwenda na maji. Maana waswahili wanasema, mchamago hanyele kwa vile mchamago hanyeje, huenda akarudia papo baadaye. *(Makofi)*

Kwa hivyo tuvitizame hivi vikundi vinavyokufa vifufuliwe vilivyokuwa havijafa viimarishwe vipewe kipa umbele ili viweze kulinda utamaduni wetu wa Mzanzibari, viweze kuimarisha Zanzibar yetu. Lakini pia viweze kuipa hadhi na thamani kubwa kama iliyopo hapo mwanzo mpaka mzungu akatoka alipotoka akaja hapa kuwekeza, lakini akaja hapa kufanya masuala ya utalii na kila kitu kwa kupitia utamaduni wetu na utamaduni wenyewe si wa huu wa kuvaa koti na kuvaa *tight* ilikuwa huo huo wa khanga mbili juu na chini, lakini wa kikoi, lakini wa msuli pamoja na kanzu ya shehe.

Mhe. Naibu Spika, mimi pia ningemuomba sana Mhe. Waziri tuna vitengo vyetu vingi hivi vya habari lakini miye nitaizungumzia ZBC Redio na ZBC TV, kwa sababu hizi ndio za Mzanzibari halisi ilikiwemo na hizo nyengine wao watatuiga kwa kupitia hizi. Ningemuomba sana Mhe. Waziri kwa vile sisi ni wana utamaduni ni wazanzibari halisi lakini kama ni wana utamaduni, kama ni Wazanzibari halisi kuna mavazi yetu maalum ambayo yalikuwa yanatumika hizo enzi za utamaduni hasa sio leo, leo hayako lakini yanajulikana na yanapatikana. Kwa hivyo kuwekwe siku maalum ndani ya vipindi hivi viwe ni kuanzia watendaji wote wanaofanya kazi katika ofisi hizi za ZBC TV na ZBC

Redio waoneshe ule utamaduni kuanzia wao, wanaokwenda pale wanatangaza wakisha onekana pale na khanga yake juu na chini mwenyewe kajipiga kikulacho au kisutu kavaa khanga yeke juu na chini mwenyewe bukheri siku hiyo anasoma taarifa ya habari pale anaoneka na khanga yake juu na chini, ule ndio utamaduni nao lakini na baba akiwepo pale kavaa kikoi chake na shati mwenyewe na koti utamaduni.

Lakini yenye mwenyewe siku zote pale anakwenda na koti au na suti ule utamaduni na siye utakuwa tunaanza kuupiga vita kwa kuanzia mule kwenye vyombo vyetu vya habari. kwa hivyo kuwe na siku maalum ya kuonyesha ule utamaduni kuanzia wao lakini mpaka na vile vipindi vinavyofuata. Hapo tutakuwa tunaupa hadhi na tunaukuza ule utamaduni lakini na hizi ngoma kipindi hicho nakumbuka kulikuwa na kipindi cha ngoma burudani asilia. Hizi burudani asilia basi nazo zionyweshwe hivi vikundi tunajua kwamba vipo kila kijiji kina utamaduni wake lakini kina ngoma zake, zilikuwa zinaonyeshwa si Msewe tu sasa hivi na Mkurungu na nyengine zipo zitafutwe ziwekewe kipindi chake zifufuke, zionyeshwe zijulikane. Kwa sababu siye tunakwisha lakini kuna wengine ambao wanachipukia huko hawazijuwi wala hawajawahi hata kuvisikia. Hivi sasa mtoto wa huko nje ukamuuliza chawa hamjui, ukamuulize chepu hamjui, kwa sababu yanakwisha kwa hivyo na haya mengine yatakwisha watakuwa hawayajui chochote.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea pia nakuja moja kwa moja kwenye suala la utalii lakini kwenye mambo haya mapango yetu ya historia. Mapango ya historia tunafahamu kwamba yapo mengi sana na kama yapo mengi sana kila ambalo limetajwa humu linahitaji kuimarishwa na kufanyiwa kazi haya mapango pametajwa na Fukuchani hapa lakini ninavyofahamu Fukuchani yapo, lakini hivi karibuni kuna pango ambalo liligundulikana pale kwa Juma Rama (Tazari) lile pango tangu lilipogundulikana pale pamekwa kibango kinaonyesha kwamba lile pango na ile njia ipo inayokwendea huko kwa Juma Rama kwenye hilo pango.

Lakini tangu kipindi hicho lilipogundulikana watalii wakenda sikui kulikuwa kuna mambo gani sijui barafu, sijui kunang'ara dhahabu sifikirii kama Wizara bado inalighulikia hili pango na linafanyiwa kazi na kuwekewa kumbukumbu na historia zake likaweza kutembelewa, likaweza kuonekana na watu wakaenda kulikagua. Kwa kweli kuna haja kubwa ya kuwekewa kumbukumbu tosha haya mapango lakini pia kuwekewa miundo mbinu mizuri ikaweza kufahamika yakaweza kutumika na yakaweza kutembelewa.

Mimi nitalizungumzia zaidi pango la Kisima cha Mangapwani Mhe. Naibu Spika Mangapwani katika historia nayo ni sehemu maarufu sana lakini pale Mangapwani tunaona kwamba kile kisima pale ndio kipo kisima tu, ukifika wewe unakikuta kisima ndio sasa hivi afadhali pamejengwa hivyo vyoo angalau mtu akifika hupata akatabaruku akaendelea mbio huko chooni lakini vilikuwa havipo pia. Lakini Mhe. Waziri kwa vile vyoo vishawapo pale kuna haja kubwa pale na kumtafuta mwekelezaji akafanya angalau kiji *restaurant* wale wageni wetu au ule utalii wetu unapokuja pale wakaweza kupata kupumzika lakini pia wakaweza kupata na viburudisho vyengine, ile pia nayo itatuengeneze pato la nchi yetu. Kkwa sababu mgeni atakapokwenda pale, historia bonde kisheliona atataka maji anywe yale na utamchotea, lakini akishakunywa yale maji pia atataka akale ubwabwa pale *restaurant* iwapo atakula.

Kwa hivyo Mhe. Waziri hili nalo ningekuomba sana ulichukuwe na ulifananyie kazi kwa kuona tu kwamba linatakapokuwepo pale hili suala basi na sisi tunaweza kuingiza chochote kama tunavyoingiza haya mengine kwa kupitia shughuli nyengine na kile nacho kinaweza kutusaidia na kutuongezea pato letu la nchi. Sehemu ile nayo ni maarufu lakini nikiangalia ile sehemu iko katika hali si nzuri kwa sababu imezungukwa na mwitu na mijiti mingi lakini pembeni yake pana upepo mzuri tuu pale wa bahari kwa hiyo nafikiri itakapokuwepo na hii sehemu ya kujipumzisha kama *restaurant* au kijihoteli kimoja wapo yaani uimara wake utazidi kuwa mzuri na utalii utakuja zaidi uzidi kwenda pale na tukaweza tukapata mapato yetu ya nchi.

Lakini pia kuna suala la pango ya Mize wa Mize Kizimkazi kwa kweli tukiangalia haya maswala ya historia mengi yanarejesha nyuma kwa sababu tunaona kama kwamba yanawekwa mbago na yakawa yanawekwa mbago yale ndio hayaonekani kwa sababu jambo utapoliweka mbago utaliweka nyuma yako na nyuma yako hulioni kama hujageuka ukalitizama. Sasa ili yasiwekwe mbago yaweko usoni uyatizame kila wakati uyaone. Kwa hivyo Mhe. Waziri ningekuomba sana kwenye maswala ya historia na utalii yafanyiwe umakini au yapewe kipaumbele zaidi ili wanahabari, lakini wana utalii, lakini na sisi wazawa tunaozaliwa tuweze kunufufaika na kufaidika na zile sehemu zile za historia ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, niendelee pia kwenye suala la uimarishaji wa vituo vyetu hivi vya ZBC TV na ZBC Redio Mhe. Waziri kwanza nikupongeze sana kwa kuvimarisha lakini pia kwa kuvipa nguvu kwa hali ya juu sasa hivi vikaweza kufanya kazi kwa umakini zaidi. Kwa kweli sasa hivi tunashukuru sana hivi vitendea kazi vyetu *wallahi* kwa kweli sasa hivi vinajitahidi kwa sababu

wafanyakazi wake tunawaona jinsi wanavyokwenda huku na huku wanavyozunguruka katika shughuli zake hizi za kutafuta habari lakini pia kwa kuyafikia yale maeneo husika kupata zile habari ambazo zinatakiwa kupatikana katika hivi vyombo.

Lakini kuna kipindi hiki cha mawiyo kipindi cha mawiyo kinawatangazaji wake mbali mbali na wamo sehemu tofauti utamsikia Suzan Kunambi sijui wapi alipo, mwengine sijui nani yuko Matemwe lakini kwenye utafutaji wa habari napo pia tukawa tunao hawa wakala ambao wako humo vijijini tutapunguza ule mzunguruko wa kuwa mfanyakazi atoke pale aende kule sehemu husika wakati kumbe njia rahisi ya kuweza kuwasiliana tu wakapashana zile habari na kama unavyotwambia sasa hivi tumeondoka na ule mfumo wa *analog* tuko kwenye *digital*, itakuwa tunaurahisi na tutafanya kazi kwa uwepesi zaidi tukiweza kuweka haya matawi katika hizi sehemu husika. Mime nafikiri kumtoa mfanyakazi mjini akenda kuchukua habari Nungwi au Makunduchi au sehemu nyengine kama Miwani na kuendelea huko kwengine. *Time* nyengine inakuwa ni usumbufu kwa sababu tunajua kama vipindi miongo inatofautika. Kuna kipindi cha mvua, lakini kuna kipindi cha jua kali, lakini kuna kipindi chengine pengine mambo yamekuwa mabaya huku.

Kwa hivyo kama kutakuwa na yale matawi wanaweza kupashana habari kupitia hiyo mifumo ya *digital* tuliyonayo sasa hivi, bila ya mfanyakazi kutoka mjini akenda kule. Kwa hivyo hili miye ningekuomba sana Mhe. Waziri tulitazame kwa upana wake ili tuone jinsi gani ya kuweza kulifanikisha hili ili kuwapa urahisi hawa wafanyakazi wetu kuweza kuhangaika na ma *camera* kwenda huku au kutafuta usafiri kwasababu time nyengine tunavijua ni vitu ambavyo vimetengenezwa na binadamu huweza vikawa *time* nyengine havifanyi kazi lakini unaweza ukampunguzia ule usumbufu yule mfanyakazi akaweza kufanya kazi yake kwa wepesi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, miye nilikuwa sitaki niongee mengi juu ya suala hili lakini kwa kumalizia kuna sehemu hizi ambazo Mhe. Waziri alitutajia hapa kwamba hili suala la sinema linafanya kazi humo vijijini kuwapasha habari wananchi, lakini pia kuwaonesha vitu tofauti vya kuhamasisha jamii lakini pia katika kuwapasha habari mbali mbali. Lakini mime ningependa kumuuliza Mhe. Waziri kwa vile hizi sehemu ambazo ulizitaja hapa zikiwepo Donge, Bandamaji, Kitope wananchi tayari wameshapata hizo habari lakini wameshaona jinsi gani wanahabari wetu wanavyofanya kazi.

Lakini kama wananchi sijui utatwambia kwamba wamefaidika vipi kwa sababu si kama ndio ulikwenda siku zote mie nafikiri kila sehemu ulikwenda kama

mara mbili au mara tatu au mwengine mara moja. Sasa je, hawa wananchi kwa kuwapelekea hii sinema siku moja au siku mbili wamefaidika vipi na vipi wameweza kuona hii hali ya hizi TV zetu au hizi sinema zetu zinazofanya kazi kwamba zinaweza kuwasaidia katika kuwaimarishia hii miundo mbinu yao angalau na wao wakaweza kupata habari tofauti zinazotokana na hawa waandishi wetu wa habari, lakini pia kujua matokeo mbali mbali yanaendelea katika nchi yetu kwa kupitia hizi sinema. Lakini pia kuona mambo ambayo yanaweza kuwaondoa wao katika sehemu moja kuwaweka katika sehemu nyengine ya upeo wao wa fahamu au akili kwa kupitia hizi sinema.

Mimi nafikiri kwamba kuna haja yakurudisha ule mfumo wa zamani hivi sinema zilikuwepo lakini zilikuwa.....

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hidaya una dakika moja malizia

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nafikiri maoni yangu umeyafahamu kwa hiyo kwa kumalizia nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa mashirikiano yake makubwa na wananchi wake lakini na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya sasa hivi miye niwapongeze sana lakini nimwambie tu Mhe. Waziri, vikundi, wasanii na wanahabari wote ni kitu kimoja kwa vile wanajenga Tanzania yetu na wanalijenga taifa letu kwa hiyo kwa vile ndio wanafanya hivyo basi kunahaja ya kuwaweka pamoja na utapowaweka pamoja hawa wakawa wanafahamiana wanakutana kwa kweli nchi yetu itakuwa katika hali ya uzuri na itakuwa katika hali ya kupasha habari katika njia ya urahisi zaidi.

Mhe. Waziri, nikupongeze sana na uzidi kufanya kazi hii ili tuone nchi yetu na TV zetu hizi na Redio zetu zinafanya kazi kila wakati muda wote, *time* zote na kila pahali yanafika mawimbi haya ya Redio Zanzibar lakini na TV Zanzibar zote zinafanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, naunge mkono hotuba hii asilimia mia moja, kwa kumwambia Mhe. Waziri kuwa, mcheza kwao hutunzwa. Ahsante Mheshimiwa *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa anayefuata ni Mhe. Bhaa, baada ya Mhe. Bhaa atafuata Mhe. Abdalla Ali Kombo na ajitayarishe Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa mchana huu kufika hapa katika Baraza

lako Tufuku kuchangia hoja muhimu sana hii kunipa nafasi katika Wizara hii ya habari, Utalii, Utamaduni na Michezo lakini kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa juhudi zake kubwa na nzuri kabisa kwenye sekta hii ya utalii, mchezo na utamaduni kwa kazi nzuri wanayoifanya na mimi kabla ya kusema Mhe. Naibu Spika, naomba niunge mkono asilimia mia kwa mia kwenye wizara hii sina matatizo nayo isipokuwa nitatoa tu maoni yangu machache.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana pia Mhe. Spika wetu jana kwa kuja kufungua Ijitimai kule Kidoti. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme tuu niwambie wanachi wa Zanzibar kwa kweli jana Ijitima ilikuwa na watu wengi hasa usiku hasa upande wa wanawake walikuwa wengi sana na mimi nilikuwa mdau pale nashughulika kufunga spika na ikiwa sauti haikuwa vizuri, basi wananchi walikuwa wanasikia vizuri mawaidha yetu kwa kweli nashukuru sana Mwenyezi Mungu atuwezeshe kufanikisha vizuri Ijitimai letu kwa pamoja kabisa na japo Wawakilishi mtakuwa hampo baadhi ya majukumu nitakuombeni dua hasa kwa usiku wa leo nitaomba Baraza letu la Wawakilishi na wananchi kwa jumla tupate kuombewa dua na kuweza kufanya kazi zetu vizuri kabisa katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze katika ukurusa wa 20 kifungu namba 44 suala la michezo katika kitabu cha Mhe. Waziri, mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri kwanza katika kitabu chake katika mambo ya michezo ni muhimu sana katika nchi yetu, lakini ukiacha michezo Mhe. Mwenyekiti ukiangalia mchezo ni mazoezi kwanza, ukiangalia michezo Mhe. Mwenyekiti ni afya kwetu sisi mimi. Mimi naomba sana Mhe. Waziri suala la michezo ukiacha michezo kwa vijana pia kwa wazee wahamasishwe wafanye mazoezi kwani mazoezi Mhe. Naibu Spika, ni afya kwa mtu yoyote unaweza kufanya mazoezi ukaacha ukatumia dawa kama za *pressure* au sukari huo utafiti umefanywa na wataalamu mazoezi ni dawa kabisa kwa maradhi hayo. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Waziri wape elimu wananchi mazoezi, michezo ni muhimu sana katika maisha yetu hasa katika mambo yetu ya afya.

Lakini niende Mhe. Naibu Spika, haraka haraka katika sekta muhimu sana hii ya utalii. Mhe. Naibu Spika, sisi nchi yetu Zanzibar tumekubali utalii asilimia 80 tumekubali utalii tunapata kodi kupitia utalii. Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi niseme huu utalii unatizamwa njia mbili. Njia moja kuna baadhi ya watu wanaupiga vita utalii, na sisi ni pato la taifa kwenye nchi yetu na tumeukubali mia kwa mia, na pia kuna watu wanasema utalii ni dhambi na ni haramu. Sasa tusichanganyishe dini na mambo haya ya sekta ya utalii ni hatari kubwa unaweza ukamuona mtu hana maadili kwa sababu ya utalii, lakini ukitizama

upande wa pili ni ajira hii kwetu sisi bila ya utalii tutaishi vipi hapa Zanzibar. Sisi wenyewe Baraza la Wawakilishi tutashindwa kulipwa, ripoti ya kamati imeeleza vizuri sana hapa mambo mengi kuhusu utalii. Kwa hivyo, mimi naomba watu wa dini wasichanganyishe, serikali haina dini, nchi yetu haina dini, chama chetu hakina dini. Mimi naomba sana tusichanganyishe mambo ya dini na sekta hii ya utalii. Kwa sababu kuna mambo sio maadili yetu kwenye utalii, na utalii tumeukubali Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme tu hapa ni-*declare interest* yangu kabisa nasema, haya mambo ya utalii jana nimechangia kuna watu wamelalamika wamesema kama mimi napotosha maadili, mimi nafanya nini. Mimi sipotoshi maadili hii ni ajira kwetu sisi upande wa utalii, upande wa mziki kwani burudani ni ajira mheshimiwa. Na ukiangalia juzi nilikuwa Bungeni kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano Tanzani Mhe. Waziri Angela Kairuki kasema kuna watu wana *masters* wamesoma sasa hivi wanaendesha bodaboda, hamna ajira. Sasa leo tukisema utalii huu tutaupiga vita au hizi ajira za utalii hatuzitaki sisi itakuwa wasanii wote watakuwa hawana kazi. Mhe. Naibu Spika, mimi nasema hivi kwa sababu na mimi nimetokea huko huko nawatetea wasanii wenzangu kuwaheshimu tuwape fursa ya kufanya kazi kuendeleza utalii.

Mhe. Naibu Spika, kule Kaskazini jana nilikuwa na Mkuu wa Mkoa na viongozi wengi wa Kaskazini kuna wageni wamekuja Mufti wetu wamekaa kwenye hoteli za kitalii. Mufti wa Malawi, Mufti wa Uganda Mufti wengi wamekaa kwenye hoteli za kitalii, lakini sasa hoteli za kitalii zina mambo mengi kunauzwa mambo ya pombe, mambo ya vileo lakini kwa sababu ya utalii wale Mufti wanajua hawawezi kusema kitu.

Mhe. Naibu Spika, lakini tuangalie shilingi ina sehemu mbili kuna huku na huku kwa hiyo tukae kati kati mheshimiwa tukubali yote kwa sababu sisi nchi yetu masikini bila ya utalii hatuwezi kupata ajira yoyote wala kupata mapato kwenye nchi yetu. Sasa mimi naomba sana watu wa dini wasichanganyishe wasituone wabaya kama sisi tunashajihisha mambo ya utalii.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niseme kitu kimoja kwamba mimi zamani miaka 20 ya nyuma au 15 nilikuwa nina sw ali Ijumaa mpaka Ijumaa, ikifika Ijumaa mimi ndio nakwenda kuswali. Nakumbuka nilikuwa nasomeshwa na Sheikh Mwalimu Aliani pale Msikiti wa Mchangani, tulikuwa na Amani Ibrahim Makungu kaka yangu akamwambia Sheikh Aliani huyu anasali Ijumaa mpaka Ijumaa tu, siku nyengine zote hasali. Sheikh Aliani akamwambia sikiliza Amani muachie huyu asali Ijumaa mpaka Ijumaa, atasali Ijumaa, atasali tena Alaasiri, atasali Magharibi kidogo kidogo na atasali Alfajiri. Namshukuru

Mwenyezi Mungu alivyoniambia vile Sheikh yule mpaka leo simsahau, na mimi nimeendelea kusali hivyo hivyo. Nimeanza kusali Laasiri kidogo, nimesali Magharibi kidogo mwisho nikasema ah kwa nini nisiswali vipindi vyote. Sasa hivi nikisia Muadhini naona tabu roho inanusuta kwa nini siende kusali mimi. Mhe. Naibu Spika, tuangalie vijana wanabadilika taratibu huwezi kumbadilisha kijana haraka haraka. Kwa hivyo, mimi naomba sana mheshimiwa tuangalie hili suala vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, nije kwa haraka katika ukurasa wa 23, kifungu cha 50 somo la utamaduni na sanaa katika skuli zetu za msingi. Mimi nampongeza Mhe. Waziri unawafundisha wanafunzi wetu katika masomo haya ya sanaa, silka na utamaduni wetu wa Zanzibar. Mimi nakupongeza sana ni vizuri kwa kuibua vipaji vyao pia, mimi nakumbuka nilipokuwa nasoma kila mwisho wa mwaka nafanya michezo ya kuigiza, wanaimba wanafunzi, wanacheza tunapata vipaji na wengine leo wamekuwa wasanii wakubwa tu. Kwa hivyo, naomba tuendeleze kuwafundisha kwa sababu hii ni ajira kubwa sekta ya utalii ni ajira kubwa kwetu Zanzibar na ni muhimu sana.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye ripoti ya kamati yetu hii ya Baraza la Wawakilishi. Nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti amefanya kazi kubwa sana kuileta ripoti hii hapa, nawapongeza wajumbe wote, kwa sababu wameona umuhimu. Ukiangalia kwenye ripoti yetu aliandika hapa ukusanyaji wa mapato katika sanaa, utamaduni walipangiwa kukusanya milioni 393 na *point* kidogo lakini wamekusanya milioni 170 tu kwa sababu mapato yameshuka katika nchi yetu. Kwa sababu hamna burudani pia yanaingiza mapato nilisema mimi juzi hapa, na sasa hivi ripoti imekuja imeshuka na ukija katika ripoti ya mwakani itashuka tena Mheshimiwa. Kwa hiyo, lazima turekebishe Mhe. Waziri tizama unavyoona na utupe mwelekeo unavyoona wewe, wewe ni dhamana wa wizara hii utupe maelekezo sote tutakufata wewe ili tuweze kuelekea mbele kwenye sekta ya utalii.

Mhe. Naibu Spika, mimi namuomba sana Mhe. Waziri angalia hilo. Mheshimiwa mimi niseme kwa haya, kwa sababu ni utalii Zanzibar ni muhimu sana inapata kodi karibu asilimia 80 ukiangalia ma-*Five Stars* hoteli zote Zanzibar zipo hapa, ukiangalia Dar es Salaam Tanzania Bara kwa hivyo sisi tuko juu kwa mahoteli. Mahoteli yale ya kitalii na ya kifahari yapo hapa Zanzibar yamejengwa fedha nyingi zimetumika. Kwa watalii wetu wanakuja wa hadhi ya juu kabisa. Kwa hivyo hili jambo sio mchezo na juzi Mhe. Waziri Haji Omar Kheir alikuwa hapa ndani ya Baraza mimi sikupata nafasi yakuchangia hoja ile ilikuwa kuhusu *CCTV camera* pesa nyingi tulitumia kwenye hizi *camera*.

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema katika Baraza hili Tukufu mimi ni mjumbe mmoja niliyebakia nilikwenda China kwenye mradi huu. Tulikwenda mimi, Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Spika Mstaafu, Katibu wa Baraza, Mhe. Abubakar Khamis Bakar Katiba na Sheria tulikwenda China Shanghai Macau kuangalia huu mradi, na mimi nilikuwa ni mmoja shahidi na nimeukubali kwa sababu hawa *ZTE* walifanya kazi hii kwa umakini mkubwa na wamefanya China karibu maeneo mengi kuangalia mradi huu ni wa teknolojia wa hali ya juu nasema. Kwa nchi iliyoendelea ndio wanafunga mitambo hii nchi nyingi zitashindwa kufunga mitambo hii, sisi tumepiga hatua na mimi nilikwenda China mheshimiwa. Kwa hiyo, wajumbe hawajui mimi sijapata kusema lakini nasema mradi ule Wazanzibari utatusaidia kwa usalama wa nchi yetu, kwa sababu ule ni *wireless* zile *CCTV camera* hazitumii waya masaa 24 usiku na mchana zinaonekana kwenye zile *camera*. Kwa hivyo, ukipita pale utaonekana.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo mradi huu sio masihara wananchi baada ya muda fulani tutaona nchi yetu ina usalama mkubwa bila ya kutumia polisi unaweza kumkamata mtu asubuhi tu kwa sababu tukio umeshaliona usiku gari fulani imepita pahala fulani, na mtu fulani gari yake anataka kuchukuliwa. Kwa hiyo, mradi huu mimi nilikuwa shahidi na nilikwenda Shanghai China na Mhe. Waziri wa Fedha aliyepita tulikwenda pamoja kuukubali mradi huu. Tena nishukuru *ZTE* wametufanyia kampuni ya wenzetu ni mkopo tu kuna nchi wanalipa *cash* wanafungiwa hizi *camera*, na kuna nchi mpaka leo hamna hawajafunga hawana uwezo wa kufunga. Kwa hivyo, mimi nawaomba wananchi wasubiri waone na hizi *camera* zitasaidia utalii utazidi Zanzibar kwa mara tatu yake.

Mhe. Naibu Spika, niendelee katika hizi kumbi za starehe sasa. Mheshimiwa kisheria zimesajiliwa, juzi nilisema watu hawajanifahamu lakini kisheria zimesajiliwa na zinalipa kodi kila kitu kwa ajili ya kuendesha burudani hii. Lakini juzi juzi Mhe. Mkuu wa Mkoa wetu alipiga marufuku mwisho saa sita, sasa ukisema Mhe. Naibu Spika mwisho saa sita, saa sita ni mapema. Juzi juzi miezi kama mitatu nyuma Marekani New York wamefanya *show* karibu wiki mbili wamefungua kama uwanja wa mpira wa Mnazi Mmoja, wiki mbili hakuna asubuhi, mchana jioni *show* inaendelea tu wasanii wanabadilika wanaimba tu. Kuingia pale kwenye ile *show* ilikuwa ni dola 500 mtu mmoja sio fedha ndogo. Sasa tuangalie hizi *show* zinakwisha saa sita, saa sita ni mapema ukitizama vijana wa sasa hivi saa sita ndio anaamka anatoka. Sasa saa sita tumpe dhamana waziri aangalie hii sekta yake anataka mapato waziri aje hapa tumsifu, leo anakuja hapa waziri tunamponda mapato madogo anayokusanya. Kwa hiyo, naomba sana hili suala la muda aachiwe waziri aangalie na usalama

wa Mkoa wapo polisi wafanye kazi yao usiku na mchana wasilale wapewe mafuta warande. Polisi wetu wanazo bodaboda warande na wakamate hawalifu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitoe mfano mdogo kwa *Airport* kaja mtu na madawa ya kulevya mtu mmoja tu…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umeniomba dakika tano eeh…

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Namalizia naomba dakika tatu nimalizie Mheshimiwa.

Kwa hivyo, *Airport* ile kama mtu mmoja kaharibu kwa hiyo *Airport* ile ifungwe kwa ajili ya mtu mmoja? Akamatwe yule mtu mmoja waliobakia waendelee na kazi zao kama kawaida. Kwa hivyo, mimi naomba sana tuangalie sana suala hili.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwa hawa vijana wetu wazaliwa waachiwe wafanye burudani wakivunja amani ya nchi yetu basi wakamatwe watiwe ndani, hilo halina tatizo na serikali iangalie hizi shughuli za burudani zina mapato mengi wafuatilia mapato. Mhe. Naibu Spika, namwambia Mhe. Waziri afatilie mapato yake, vibali, leseni za hawa Ma-DJ na nini fatilia upate mapato serikali yetu ndio sisi mshahara wetu unatoka humu kwenye hizi kodi.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme nishatembea nchi nyingi sana kuanzia Tanzania Bara nashukuru nimetembea sana, New York nimefika ukiangalia New York Manhattan Times Square ukitizama Broadway, yaani unapita pale eneo lile linastarehe kuanzia asubuhi mpaka jioni watalii wanakuja kutoka nchi mbali mbali. Haina muda, muda haujawekwa asubuhi kuna starehe, jioni kuna starehe lakini mapato yanaingia masaa 24 kama mimi muongo mheshimiwa *Times Square* kuko vipi pale katika suala zima la utalii. Ukiangalia Macau, ukiangalia Dubai pia, Faisi, Canada kote haya mambo yapo mheshimiwa kwa sababu ya mapato na tunaingiza katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuuliza Zanzibar mtalii gani amelalamika kwamba hapa kuna matatizo au kuna shida yoyote yeye haji, watalii kila siku Zanzibar wanaipenda. Kuna mtalii mmoja alikaa hapa wiki moja anaondoka analia anasema kisiwa kama hiki kizuri nitakipata wapi mimi kuishi. Kwa hivyo, leo utalii huu umefikia hapa naomba sana tuangalie Mhe. Waziri tumefikisha utalii wetu hapa kwa kazi kubwa, serikali yetu imefanya kazi kubwa kutangaza utalii, na wewe unafanya kazi kubwa. Sasa asitokezee kiongozi mmoja akaja akatuharibia mtandao wetu huu naomba sana tuangalie

kiutandani ni ajira yetu sisi vijana na mimi *interest* yangu na-*declare* kwenye Baraza na nawaombea wasanii wote wenzangu tusaidiane waniunge mkono tushirikiane kwenye sekta hii ya utalii tufanye kazi ni ajira yetu, ajira hamna sasa hivi ni shida.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, mimi naunga mkono namshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii wala sina mashaka nayo nawaomba wajumbe wote waunge mkono wasipige mabuti wamuachie waziri afanye kazi zake vizuri kabisa. Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Bhaa mchangiaji anayefuata ni Mhe. Abdalla Ali Kombo, baada ya Mhe. Abdalla Ali Kombo atafuata Mhe. Omar Seif Abeid na ajitayarishe Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Kwanza naunga mkono hotuba hii hakuna buti, hakuna kucha uko huru. Mhe. Naibu Spika, nakupa hongera sana Waziri wa Habari, hongera sana mkongwe kwa kazi yako. Nataka kumwambia tu Bi. Hidaya alisema leo tugonge kikwetu, sasa sinema haitwi senema inatwa ulaghai tu kwetu.

Mhe. Naibu Spika, kuna watu sasa katika nchi wamejifanya wababaishaji wa tamaduni zetu. Kwanza nitangaze ku-*declare* kwamba natoka Makunduchi, Makunduchi tuna utamaduni wetu na nashukuru wewe mwenyewe mwaka jana ulikuwepo utamaduni wa chakula cha kienyeji au cha kikwetu uliona mwenyewe. Lakini pia tuna sikukuu ya Mwaka kongwa kuna watu wana maneno mengi, mimi Unguja na Pemba nimeshatembea mwingi kila mtu anavaa kivyake. Ukienda Tumbatu ukiona shuka inayovaliwa utacheka, ukienda Micheweni, ukienda wapi wengine wanakula popo, wengine kenge wengine panya kila mtu na lake. Na wote hao wameikamia Makunduchi kwamba Mwaka kogwa sio, sio. Mwaka kongwa wewe huambiwi ukafanye vitendo ambavyo havina maana, Mjini hapa kuna mambo taarab Mhe. Bhaa samahani, kuna kila kitu vitu ambavyo na sisi wa shamba hatuoni vizuri. Kwa hivyo, napenda kuwajuilisha tu wale watu wa Mjini na hasa waliotia tia dini ambao wengine Makunduchi kulikuwa na Sheikh Ameir ni mwana chuoni kwa Unguja hii nambari *one*. Kulikuwa na Sheikh Fatawi bin Issa na mambo haya yote yalikuwepo, Kwa hivyo nawaambia watu watuache tupigane makoa tukale mchele.

Mhe. Naibu Spika, sasa nakuja kwenye utalii hapa nina wazo langu, niliwahi kuzungumza na baadhi ya watu ingawaje tunasema mapato yamekuwa mengi sana kwenye utalii, lakini naona bado kuna shimo la mapato yanapenya. Ningeomba wizara ikakaa na watu wa Uhamiaji na wengine wote ikawa kuna *one stop center*, mtalii anayeingia Zanzibar ndege inateremka anakwenda kwenye kituo kimoja Uhamiaji wapo, Kamisheni ya Utalii ipo na wale wote ambao wanaohusika. Tunajua watalii ambao wanaingia Zanzibar idadi fulani, wa *grade* fulani badala ya kwamba sasa jioni wengine wachukue gari waende Kiwengwa, wengine Makunduchi, wengine Jambiani, wengine kwa pikipiki watalii wamepumzika vyumbani mwao wanaanza kugongewa, hiyo nadhani sio nzuri. Naiomba serikali kupitia wizara hii ikae ifanye *one stop center* mtalii anayeingia anajuulikana analala chumba kipi, analipa kitanda kwa chumba pesa yetu tunakuwa tunaijua Uwanja wa Ndege hakuna tena kuja kumuuliza *ZRB*.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la tumepata kibali cha *CAF* sio *CUF, CAF* hii ya mpira natoa tahadhari tu tumefurahi hasa rafiki yangu Mwakilishi wa Jang'ombe amefurahi sana. Lakini Mhe. Waziri ningependa tukajitahidi, kwa sababu kuna malipo hapa na malipo yenyewe si kidogo na mechi zetu ukiacha za Jang'ombe kuna mechi za kina Bambi sijui Upupu, Simba gani ya Muyuni hazina mapato. Kwa hivyo, naomba tusifurahi tujipange tusije tukaadhirika tukashindwa kulipa pesa za watu.

Mhe. Naibu Spika, hii ni mara ya pili kumuomba Waziri wa Habari, Utalii na Michezo wenzetu vyombo vyengine vya *radio FM* hizi zote ninazisikiliza siku ya Ijumaa, Jumamosi na Jumapili huwa kuna miziki ya zamani tunahitaji kupumzika Mhe. Waziri hizi mvi wengine tumeshakuwa wazee. Taarab zile za zamani wengine sio washabiki wa taarab, hivi leo Dar es Salaam kuna mashindano ya Msondo Ngoma na Sikinde hebu na sisi tutafutie nafasi kwenye redio Zanzibar au televisheni tuone Tokomile ilikuwa inapigwa vipi, tunakuomba Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, nakuja tena hapa ningeomba kidogo ninukuu. Wanasema, "haja isiyoridhishwa husumbua fikra kama kiu isiyozimwa isumbuavyo koo siku zote". Na vile vile wanasema elimu ilipokuwa haijuulikani duniani mvi zilihesabiwa kuwa ni alama ya hekima na akili nyingi, fikra hii ilikuwa njema sana lakini wakati wake umepita wala haurudi tena. Sasa mtu kama hakuelimishwa mvi hizi hazifanyi kazi, ni suala la vijana sasa kuwaheshimu wazee kwa uzee wao. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kiu yangu haijaridhishwa bado koo yangu inasumbuka.

Mhe. Naibu Spika, nakuja na suala la nyumba inayohusiana na utalii, hii ni ya utalii. Mhe. Waziri ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliniambia niende kwa Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo na yupo jamani nakuulizeni ni najitahidi sana kutumia misemo nisitukane, hii nyumba ni ya nani? Kama ni ya *private* kama ni ya serikali madhumuni yake ni nini? Hii nchi ndugu zangu wengine bado vijana, hii nchi watu wamehangaika, hii nchi imepinduliwa wazee wamekwenda Ghana, wamekwenda sijui wapi mpaka imepatikana. Kuna mali zimegaiwa kwa halali, kuna eka, kuna majumba ya Michezani kwa nini hizi nyengine hatutaki kugawa kwa halali. Ninavyofahamu mimi hapa mawaziri suala likimshinda waziri mmoja wengine huwa wanasaidia, kwa nini nikiuliza suala hili mawaziri wengine hamsaidii? Juzi nilizungumza maneno hapa ikawa eeh huyo Mmakunduchi Kiswahili hajui, lakini leo nasema wazi kwa nini hawa wengine hamsaidii, mko 13 hawa 12 kwa nini hawasaidii? Jamani nakuombeni hii nchi inatuuma haiwezi tukachukua rasilimali za nchi hii kwa kucheza kibafta, wengi wenu watoto hamujui kibafta, unafundika muhindi kwenye mkono kibafta tatu nimekushinda, hapo ndio umepata mali. Naiomba serikali tusichukue mali za serikali kwa kucheza kibafta hii nchi inauma.

Mimi *Alhamdulillah* Mzee Karume nimemuona, anakuja Mapinduzi tunajipanga hasa, simba wetu kaja, alihangaika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Abdalla Ali Kombo zungumza na kiti.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mheshimiwa nadhani ujumbe umefika. Kwa hivyo, ninavyoomba ndugu zangu tujitahidi, naomba tena Mhe. Naibu Spika, nipewe jibu. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo nakuuliza wewe kwa kupitia Naibu Spika, lakini lile jengo hatima yake itakuwa hoteli na watu wasije wakazania labda hapa nazungumzia kibanda cha Skukuu ya Mwaka, kinajengwa mtu anakwenda zake aa. Kwa hivyo, kwa mamlaka aliyokuwanayo Mhe. Waziri naomba ile nyumba au lile jengo lipigwe picha liletwe hapa halafu tulione jengo hili mwenyewe hajulikani Zanzibar hii Unguja na Pemba kuanzia Micheweni mpaka Mtende? Kama inawezekana Mhe. Waziri namuomba tufanye hivyo.

Mhe. Naibu Spika, tufahamu madaraka haya msemaji wa Mhe. Jaku Hashim Ayoub ukiyatumia vibaya mwisho wake yanakuwa maangamizi na hatari katika nchi, kwenye vitabu vyote vya bajeti hivi mwisho tumeandika amani, utulivu, kama mwenzako Mhe. Naibu Spika, bofulo nne ziko hapa wewe una kipande hakuna amani wala utulivu na bofule zenyewe hukununua umecheza kibafta hii ni hatari.

Mhe. Naibu Spika, jengine watu wanalalamika, samahani sasa sijui kama itakuwa ni Wizara ya Habari au Baraza la Wawakilishi wanasema hizi *screen* ni ndogo, maofisa wetu huko wanasema hawaoni *screen* ziwe kubwa kidogo. Sasa sijui kama ni chini ya Wizara ya Habari au Baraza la Wawakilishi lakini wanaomba tuwe na kubwa zaidi.

Mengine wasanii baadhi yao wanalalamika kwamba *Zanzibar International Film Festival* wao si mara nyingi kushirikishwa, kweli ni wanyonge lakini wizara naiomba ikae kitako iwaweke na wao angalau waone watu wa mjini.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante nakushukuru sana Mhe. Abdalla Ali Kombo, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Omar Seif Abeid baada ya hapo atafuata Mhe. Suleiman Makame Ali na ajitayarishe Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira)

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote mimi kabla ya kuchangia mchango wangu natamka kwamba nimeiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Lakini katika michango yangu kuna maeneo ambayo nitapita ambayo yananipa wasiwasi. Sasa nitamuomba waziri anayehusika na mambo haya waziri makini aliyesifiwa na wajumbe wengi humu na sifa zake sio kwamba wamemsifu tu, lakini ni mchapa kazi mimi pia namuamini, lakini nataka aje anieleze baadhi ya humu nitakamopita kunipatia ufumbuzi ili kidogo na mimi moyo wangu uweze kuridhika.

Mhe. Naibu Spika, tuanze na ukurasa wa 7 mimi niende katika upande wa fedha zinazotokana na mchango wa serikali jumla ya shilingi 689,535,000 ambazo ni sawa na asilimia 60 ya shilingi bilioni moja zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa *Mao-tse-Tung* kwa upande wa msaada wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna kitu hapo chini kimenipa hofu ambapo anasema wizara yake bado haijapata takwimu halisi ya pesa ambazo zimetumika kutoka kwa hao wahisani, ambao wao walikuwa wamekubali kuchangia huo ujenzi kwa shilingi 5,597,500,000. Sasa nilitaka kujua wizara kazi inaendelea lakini mpaka sasa hivi hajakuwa na takwimu ya matumizi halisi yanayoendelea. Sasa kama yeye wizara hajakuwa na idadi anasema wizara yangu haijapata takwimu

halisi ya fedha ambazo zimetumika mpaka sasa, mimi jambo hili linanitia wasiwasi, kwamba ikiwa hapa mwanzo hatujaanza kupata hesabu sahihi huko mbele twendako tutakuja kuzijua zitakazotumika? Sasa mimi namuomba Mhe. Waziri jambo hili alichukulie umuhimu wake, kwa sababu hesabu ina tatizo, tatizo la hesabu unapokosa kuijua mwanzo na mwisho huiwezi, ili uweze kuifahamu hesabu upate jibu halisi lazima uijue kutoka mwanzo.

Kwa hivyo, namuomba waziri hapa atakapokuja aniambie awasiliane na watu wake hili mimi nafikiri litapita Jumatatu aweze kulieleza Baraza kwamba kwa upande ule wa wale wenzetu wametumia kiasi gani mpaka sasa hivi katika kuanzia ujenzi wa huo Uwanja. Lakini hapo hapo kwenye ule uwanja kuna kitu pia kinanipa wasiwasi, kwamba pembezoni mwa ule uwanja wenyewe upande wa kusini kuna nyumba za watu ambazo ziko chini zinaning'inia karibu na ule uwanja sijui nyumba zile wale wenyewe wakoje, wamekubaliana vipi au wameshalipwa fidia, au wataendelea kubakia pale chini ya ule uwanja. Namuomba Mhe. Waziri pia jambo hilo aje anifafanuliwe. Lakini na hizi pesa shilingi 373,785 ambazo ni mchango wa serikali kuzijua hizi katika mwanzo utumiaji wake ni vipi zimetumika kwa hiyo *feasibility study* au vipi, naomba pia hilo nalo nijue.

Mhe. Naibu Spika, tukienda kwenye ukurasa wa 16 naomba twende kwenye ukurasa huo kuhusu Magazeti ya Serikali. Mheshimiwa nimeona kitu ambacho kimenipa wasiwasi, kwamba leo Gazeti letu hili linadaiwa shilingi 400,801,780 hee! Sasa Mhe. Waziri ikiwa gazeti hili linafanya kazi linauzwa, biashara inafanyika, lakini kuna deni la shilingi 400,801,780 na kuna Taasisi za Serikali zinadaiwa na bado zimenyamaziwa kimya matokeo yake ni nini? Matokeo yake ni kuwa gazeti hili litashindwa kufanya kazi yake, litashindwa kuchapishwa, litashindwa kuwafikia wananchi Wazanzibari au Watanzania wote wakaweza kupata habari zinazotokana na gazeti hili. Mimi naomba sana Mheshimiwa, kwenye suala la deni la gazeti au la magazetu yetu lichukuliwe kipaumbele lifanyiwe kazi haraka, gazeti hili tusije tukapata aibu kwa kufungiwa lakini pia na wenye gazeti wamiliki.

Mimi nashangaa sasa hivi sisi tuna kiwanda chetu kizuri tu kuliko likawa bado gazeti hili linaendelea kuchapishwa huko Bara. Ingawa tumeambiwa hapa kwamba gazeti limeshaanza kutoka, sasa nataka nijue vipi Zanzibar Leo na haya majarida mengine yameshaanza kuchapishwa hapa kwenye kiwanda chetu cha *Zanzibar Press* au vipi. Namuomba waziri atakapokuja anijibu na anihakikishie kwamba kweli jambo hili limeanza kufanyika. Sambamba na kuzitaka hizo taasisi ambazo zinadaiwa zifanye haraka kulipa madeni haya. Pamoja na kuwa ni Taasisi zetu za Serikali lakini kila taasisi ina fungu lake,

sasa kwa nini leo watu wanashindwa kulipa. Mimi naomba na wenzetu wengi wanasema maneno haya kwamba jamani ee, sisi kule kwetu Pemba tuna msemo mmoja tunasema, "kufichana ni mwanzo wa muhali, kuambiana ni afadhali"; bora tuambiane kama watu walipe, tulipeni ili gazeti letu liweze kuendelea kuchapishwa likienda sokoni Wazanzibari sote na wananchi wakaweza kupata habari ya gazeti lao la Zanzibar Leo na majarida mengine.

Mhe. Naibu Spika, mimi kuhusu hili sitakujakuwa na muhali nitakuja kulihoji siku hadi siku, mimi si msemaji sana wa kupiga makelele lakini hili katika jambo nililokuwa silipendi ni kukuta kama taasisi moja inaizuwia taasisi nyengine kwamba isipate, kwa nini wewe unapewa huduma unashindwa kulipa. Kwa sababu umepewa huduma unatakiwa ulipe kama huwezi sema mimi siwezi achana nayo. Hiki ni kitengo ambacho kinajiendesha kibiashara, pamoja na kuwa kinaleta maslahi ya Wazanzibari kinatunufaisha kwa kupata habari, lakini pia lenyewe linatakiwa lijiendeshe kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, tukienda katika ukurasa wa 19 nimekuta hapa kuna kitu ambacho kimeandikwa napenda kukinukuu, "katika kufanikisha huduma zake, Idara ya Habari Maelezo imefanikiwa kutoa vibali 10 vya upigaji picha na uchukuaji wa filamu katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar, miongoni mwa kampuni zilizopewa vibali hivyo zimetajwa hapa, lakini hizi nilizoziona sijui kama zimo kampuni za kwetu. Kwa sababu hapa naona kuna *Tui, Reizen, Fly Dubai, Royal National Life, Boat Institution, France TV na France 3TV*.

Mhe. Naibu Spika, ningependa kujua miongoni mwa hivi vibali 10 je, hawa wote ni makampuni ya hapa kwetu au kuna makampuni ya kigeni? Si vibaya kama yamepewa makampuni ya kigeni lakini je miongoni mwa hizi zimo kampuni za kwetu au hakuna. Kama hakuna kampuni za hapa ndani za Kizanzibari je, wao kama wizara wamezishajihisha vipi kampuni hizi zikaweza kufanya kazi ambazo zinafanywa na haya makampuni ya kigeni. Kwa sababu gani nikasema hivyo, tunapozipa kipaumbele kampuni zetu si tu kwamba tunaleta faida hapa, lakini tunaongeza ajira kwa vijana wetu. Vijana wetu wanapata ajira, wanafanya kazi, wanalipa kodi, serikali inapata mapato kutokana na makampuni haya kama yataendelea kufanya kazi hapa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri namuomba suala hili unielimishe kwa faida yangu mimi na wajumbe na Wazanzibari wote wanaotuangalia.

Mhe. Naibu Spika, tukienda katika ukurasa wa 21 tulikuwa tunazungumzia Lugha ya Kiswahili, nikizungumza suala la Kiswahili Mheshimiwa katika jambo lililokuwa linanisononesha na kunisikitisha moja ni hili la matumizi mabaya ya lugha, mimi nasema matumizi mabaya ya lugha.

Leo Kiswahili utakikuta kile Kishwahili hasa kinaanza kupotea, pamoja na sifa kubwa sana tuliyokuwanayo Zanzibar kwamba watu wote Afrika Mashariki walikuwa wanakuja Zanzibar kujifunza Kiswahili, leo utakuta Kiswahili kimevamiwa na maneno yaliyokuwa hata hayaeleweki. Kwa mfano, mtu ukimuuliza habari au watu wanasalimiana mambo, utasikia poa, ee vipi bwana, kweli hiki ni Kiswahili? Sawa ni Kiswahili lakini ile lahaja yenyewe na ile hamu ya kile Kiswahili na yale matumizi yenyewe ya kusalimiana yako pale? Sasa mimi nataka kuchukua fursa hii kumuomba sana Mhe. Waziri kupitia Baraza la Sanaa na Lugha ya Kiswahili na kupitia *ZBC* kwa sababu ni taasisi aliyonayo yeye iliyoko chini ya wizara yake kuandaa vipindi, sio kipindi kidogo tu, kitoe taaluma na kielimishe jamii hasa rika la vijana. Kwa sababu tukichelea kukisimamia Kiswahili itafika kipingi tutakuja kukizungumza iwe hadithi tu, itakuwa Kiswahili chenyewe hakipo tena.

Zamani *Redio Tanzania* walikuwa na kipindi cha Mbinu za Kiswahili nakumbuka alikuwepo Bwana Abdul-Bari One, George Mbarouk, walikuwepo na wengine waliokuwa wakikizungumza na wakitoa tafsiri ya maneno ya Kiswahili. Namuomba sana Mhe. Waziri kupitia *ZBC* vitayarishwe vipindi mahasusi kwa ajili ya lugha ya Kiswahili kuzungumza misamiati ili watoto wetu waifahamu vizuri misamiati ya Kiswahili.

Leo ukienda skuli na nitamuomba Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali akija siku ya bajeti yake tutalizungumza kwa kina ni kwa nini wanafunzi wetu, watoto wetu wanafeli zaidi kwenye somo la Kiswahili kuliko masomo mengine. Ni ukweli usiofichika lazima tuambiane ukweli, kuna kasoro gani, kuna tatizo gani, watoto ilikuwa hata wakifeli Kiingereza huwezi kumlaumu kwa sababu si lugha yake, lakini leo mtoto anakwenda kufeli kwenye somo la Kiswahili lugha aliyozaliwa nayo kutoka kwa baba yake, mama yake na familia yote asili yake ni Kiswahili anakwenda kufeli kwa sababu gani. Kwa hiyo, mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, kwamba suala la matumizi ya lugha ya Kiswahili yapewe kipaumbele hasa ukitilia maanani sasa hivi kama walivyosema wenzangu kwamba lugha ya Kiswahili inakua siku baada ya siku.

Mhe. Naibu Spika, nchi zote ulimwenguni sasa hivi zinatamani kuzungumza Kiswahili, leo Redio China wana Kiswahili, Ujerumani, *BBC*, Washington D.C. mote humo wanazungumza Kiswahili. Leo Kenya ambao wakijifunza Kiswahili kutoka kwetu leo wana chuo cha Kiswahili kule watu wanajifunza Kiswahili kutoka Kenya.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana kupitia kwa waziri makini suala la lugha ya Kiswahili kwamba jamani hii ni lugha tuliyorithi sisi kwa wazazi wetu, mila,

desturi za Muafrika, za Wazanzibari hatuna budi kuziendeleza hii ni historia kubwa ni urithi tulioachiwa na wazazi wetu. Naomba sana Mhe. Naibu Spika, jambo hili liangaliwe.

Mhe. Naibu Spika, lakini tusiwalaumu wao tu na sisi viongozi pia, kwa sababu gani? Leo sisi humu Barazani tunaletewa miswada ambayo imeandikwa mtu anaona fahari kuzungumza Kiingereza kuliko kuzungumza Kiswahili lugha yake ya taifa, lakini ukienda China yeye mwenyewe anazungumza Kichina, ukienda India Wahindi wanazungumza Kihindi, ukienda Uingereza Waingereza wanazungumza Kiingereza, ukienda Waarabu wanazungumza lugha yao ya Kiarabu na mataifa yote wanazungumza lugha zao za asili, sisi tunaona fahari mtu kama hajasema Kiingereza haonekani kama ni msomi haonekani kama ni mtu. Naomba sana hata Waziri wa Sheria na Katiba juzi mimi niliumwa sikupata kuja kuichangia lakini naomba sana hata miswaada inayoletwa Barazani itungwe na sheria zetu zitungwe kwa lugha ya kiswahili kwa sababu wanaotumiwa ni waswahili.

Tunapowazungumzia waswahili tuwape haki yao huwezi kumtungia mtu sheria ya kiengereza ukenda ukamuhumu kwa kiswahili, tuzungumzwe kiswahili tuweke lugha ya kiswahili, tuizungumze lugha ya kishwahili kila kitu tukizungumzie kuhusu kiswahili. Hapo tutakuwa tumefika lengu tunalolikusudia, vyenginevyo tutakuwa tunasema tu.

Lakini utekelezaji utakuwa haupo, nilimkuta Mhadhiri mmoja anasema siku hizi kuna "Kiswa-Engilish" maneno mawili ya kiswahili manne ya kiingereza unaunganisha unganisha haileti picha nzuri haileti maana nzuri. Ni vizuri tukakuza lugha yetu ya kiswahili kwa maslahi yetu na maslahi ya kizazi chetu. Vyenginevyo haya tunayoyazungumza itafika kipindi kizazi chetu kitakuwa hawayajua maneno ya wazazi wetu. Leo kuna baadhi ya maneno ya kiswahili ukiwauliza watoto humu hawa tunaowazaa sisi hawayajui ni ukweli.

Sasa Mhe. Waziri narudia tena ombi langu kupitia *ZBC* ziwekwe vipindi ambavyo vitazungumzia mahsahususi ile misamiati na maneno ya kiswahili ya asili. Sambamba ...

Mhe. Naibu Spika: Umebakiza dakika mbili Mheshimiwa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mheshimiwa utaniongeza mbili.

Sambamba na utamaduni mwenzangu Mhe. Hidaya Ali Makame pale kazungumza maneno mazuri mazito ambayo kanifilisi. Leo kuna jambo ambalo

mimi linaniuna sana kwenye nafsi yangu. Utakuta wasanii wale wanaume wanavaa vizuri wanawaweka wanawake wanawavisha nguo ambazo hata wakati wao ndio walitakiwa wavae nguo za heshima wafanya mambo yao vizuri kwa ajili ya maslahi yetu. Ule ndio utamaduni wetu sisi Wazanzibari.

Mimi kuhusiana na kivazi cha Kizanzibari nakubaliana kabisa na msimamo wa Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi mia kwa mia. Mimi kwa hiki sitafuni maneno, "tukiacha muhali tutalala hali" wazee wa zamani walisema. Mhe. Naibu Spika, namalizia kuhusu michezo.

Mhe. Naibu Spika, namalizia kuhudu michezo, nafurahi sana na nampongeza sana Mhe. Waziri kwa bidii yake ya kuifanya Zanzibar kuwa mwanachama wa *CAF* siyo *CUF* hichi cha siasa aah! tusije tukaisema hiyo. Lakini napata hofu kwa sababu juzi niliona wenzetu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wamehoji Bajeti ya Serikali juu ya kuiwezesha *Serengeti Boys* ushiriki wake.

Je, sisi katika humu tumejipanga vipi ili pamoja na uanachama wetu wa *CAF* kuweza kusimamia vijana wetu wa timu ya Taifa ambazo zitashiriki kwenye michezo tafauti au mashindano tafauti ya kimataifa. Nakuomba Mhe. Waziri makini katika mipango yako yote utakayofanya kwenye bajeti hii lakini pia uweke kipaumbele katika bajeti yako ya matumizi kwa ajili ya timu zetu za Taifa ambazo zitashiriki katika mashindano ya kimataifa.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia muda wako umekwisha.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia na narejea kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa mchangiaji anefuata ni Mhe. Suleiman Makame Ali kesha ajitayarishe Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira) na kama muda utatosha dakika tani nitakupatia Mhe. Mohamed Said Dimwa.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hutuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya mchango wangu kwanza niishukuru wizara chini ya Mhe. Rahid Ali Juma waziri makini jembe pamoja na viongozi wote na Naibu Waziri dada yangu Mhe. Chum Kombo Khamis kwa kazi nzuri

wanayoifanya kwa kazi nzuri wanayoifanya ili kuhakikisha kwamba Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo inakwenda mbele.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia vile vile niipongeze serikali kwa jitihada nzuri wanazohakikisha kwamba Wizara hii ya Habari inafanikiwa malengo yake. Lakini pia vile vile kwa kutoa fursa kwa vyombo mbali mbali vya Habari kusajiliwa hapa Zanzibar. Pia niiombe tu wizara kwamba wahakikishe wakati wa usajili wa zile Redio na Vyombo vile vya habari vyengine kwamba wanafuata utaratibu wa Zanzibar hususan maadili na mwenendo kama unavyotakikana kwa sababu kuna baadhi ya vyombo huwa wakeshapewa zile fursa sie kule Pemba kuna msemo kwamba "Mtaraza kuna akipewa tawi huchukuwa na shina" .

Kwa hivyo, kuna wengine kuchukuwa kama wanavyotaka wao. Kwa hivyo, niombe wizara kuhakikisha kwamba wanasimamia Vyombo hivi vya Habari ili kuwahabarisha wananchi wetu habari ambazo ni za ukweli na sizo zile za kuchochea.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye suala la *ZBC*. *ZBC TV* nilisema hapa kwamba ndio mdomo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na *TBC* ni mdomo wa Serikali ya Jamhuri wa Muungano. Lakini pia vile vile cha kushangaza kwenye *ZBCTV* kwenye Kingamuzi cha *AZAM* huioni mpaka ulipie lakini *TBC* unaoiona kwenye kingamuzi cha *AZAM* bila ya malipo nchi ni moja. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri akija akijibu hapa anipe jibu ili tuweze kufahamu na wananchi wote wa Zanzibar kwamba hii nchi ni moja, kwa nini Tanzania Bara kule *TBC* waweze kuona kwenye kingamuzi bila ya malipo lakini *ZBC* tusiweze kuona mpaka tulipie. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri akija hili anijibu ili na wananchi wapate kujua.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye suala la Makumbusho. Makumbusho Mhe. Naibu Spika, ni muhimu sana kwa sababu vizazi vijavyo na sie tuliopo pia. Mimi nilikuwa sijui kwamba pale Forodhani ndipo alipokuweko yule Mwarabu, kuna siku moja tulikwenda kwenye kamati kuna makaburi pale lakini pia vile vile kama kule Mkamandume Mhe. Naibu Spika, limebakia jina tu la Mkamandume ile uhalisia wa Mkamandume haupo kwa sababu yale makumbusho yote yameshaanguka yamebakia mawe na watu wamebaikia lile eneo wanafuga ngo'mbe. Kwa hayo, yale Makumbusho ya Mkamandume mie naona sasa hivi imebakia jina na ikifika mwaka 2030 itabakia hilo jina lake tu la Mkamandume lakini ile Makandume yenyewe haipo tena kusema la ukweli. Kwa hivyo, naiomba wizara hii kuhakikisha kwamba yale makumbusho yote

yaliyobakia hivi sasa basi yaenziwe na yaboreshwe ili kuhakikisha kwamba yasipotee ili vizazi vyetu waweze kujua kunufaika na hayo.

Mhe. Naibu Spika, niende hapo hapo kwenye Makumbusho kule Pemba Makumbusho yaliyobakia nathubutu kusema ni ya Mkumbuu kule Ndagoni, kule Mkumbuu kuna historia nyingi kuna kaburi ya Mwanamwari Mhe. Suleiman Sarahani alisema hapa. Lakini pia kuna nyumba iliyoko chini ya habari kule maeneo ya Mkomani. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri na yale magofu ya magofu ya Mkumbuu uyaangalie ndani ya bajeti hii kuhakikisha kwamba ile chumvi inayosogea sasa hivi kwamba unapigia ukuta kuhakikisha kwamba yanalindwa na wanaenziwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na hili aliangalie kwa jicho la huruma kabisa kwa sababu ni historia nzuri sana ya kule Mkumbuu.

Mhe. Naibu Spika, niende kuhusu haiba ya *ZBC* pale Pemba. Mhe. Naibu Spika, kusema la ukweli *ZBC* Pemba *ZBC* Pemba imepoteza haiba kwa sababu kuna ukuta kule mpaka leo huu nadhani sijui mwaka wa ngapi, jengo lile ukuta ule hamna na sijui ilikuwa kuwaje hata ikabidi kwamba jengo lile linabakiwa kwamba kila siku bajeti hapa inapita lakini kujengewa ukuta ili kulienzi jengo lile za *ZBC* inashindikana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwenye bajeti hii aweze kuliangalia. Lakini pia vile vile *ZBC* Pemba Mhe. Waziri kuna kamera moja tu akitokea Mhe. Rais akenda kule Pemba akitokea kiongozi mwengine kutaka kufanya shughuli nyengine hapati mpaka ile kamera itoke kule iende kule. Kwa hivyo, Mhe. Waziri na huu ni usumbufu nakuomba sana uliangalie kwamba kule *ZBC* Pemba nako wanahitaji kamera kama ni mbili, tatu kwa sababu na wanaandishi pia wapo wa kutosha.

Lakini pia vile vile niende tu kwa wanaojitolea pale *ZBC* Pemba, kuna vijana pale wanajitolea sijui wanafanyakazi kwa mkataba. Lakini Mhe. Waziri ujue kwamba binaadamu si samaki, samaki kila akipea anazidi nguvu, lakini binaadamu kila akipea anapungua nguvu. Sasa leo cha kushangaza watu wale watafanyakazi kwa mkataba mpaka lini keshokutwa wanapumzika kwa sababu itakuwa wameshachoka itakuwa mafao yao hapana kwa sababu nadhani kwa mkataba itakuwa hakuna kiinua mgongo wala pencheni wanayopata. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri vijana hawa ambao kwamba wanajitolea *ZBC* kama ni Pemba kama ni Unguja basi wahakikishe kupewa kipaumbele ili wapate ajira na wao kwa sababu keshokutwa wakeshachoka kufanya kazi itakuwa hawana pa kuelekea.

Lakini pia vile vile niende kwenye Baraza la Sanaa pale Mwanakwerekwe kuna vijana wengi pale wana *design* vitu mbalimbali tena vitu vyenye ubora. Lakini

pia wale vijana wakeshamaliza kupata yale mafunzo hawapati vile vyeti vya kwamba yale mafunzo yao waliosoma wakapata vile vyeti ili wakapata kutambuliwa. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri utakapokuja na hili unipe jibu ili kwamba na wale vijana na wao waweze kujisikia. Kwa sababu kijana anakwenda pale kutaka kujifunza analipa lakini sasa cheti cha kutokea pale kwamba amekwenda kujifunza lile alilokwenda kujifunzia halionekani kwa sababu anakosa kile cheti. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri na hili uliangalie.

Mhe. Naibu Spika, mimi sina mengi naunga mkono hoja hii asilimia 90% asilimia 10% nitazuia mpaka pale Mhe. Waziri atakaponijibu maswala yangu hayo yanayotaka ufafanuzi. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono. (*Makofi*)

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba hii ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, mimi leo sitaki kusema sana na nataka kusema kwa upole kabisa kwa sababu waswahili wanasema "Mchezo kwao hutunzwa". Mcheza kwao hutunzwa kwa sababu kazi ambayo unaifanya Mhe. Waziri ni nzuri na anastahiki pongezi kwa kweli. Lakini Mhe. Naibu Spika, nichukuwe pia fursa hii kumpongeza Rais wetu wa Zanzibar Dr. Ali Mohammed Shein kwa kazi nzuri na uongozi wake bora ambao unajaa hekima na busara zake na kaweza Zanzibar kupata maendeleo yakiwemo hata hayo maendeleo ya michezo na kuweza Zanzibar kuweza kupata uanachama wa Shirika la Mpira wa Miguu Afrika. Yote haya ni uongozi mzuri na bora uliojaa hekima kwa Rais wetu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika,Waziri wetu kwa kushikirikiana na Katibu Mkuu wake wamefanya juhudi kubwa na leo Zanzibar tunajivunia tumepata sifa na jambo hili tumekuwa tukililia kwa muda mrefu kwa miaka mingi toka Mhe. Haroun Ali Suleiman, Mhe. Ali Juma Shamuhuna wote wamefanyakazi katika kuomba uanachama wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika. Lakini kutokana na uongozi na juhudi zake zaidi Mhe. Waziri leo tumefanikiwa na sasa Zanzibar ni wanachama wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika.

Mhe. Naibu Spika, mengi yalisemwa ndani ya Baraza letu hili wengine walisema nje ya Baraza, wako waliosema kwamba hatuwezi kupata uanachama labda tuvunje Muungano au twende serikali hizo waliokuwa wanazitaka. Lakini ndani ya serikali mbili leo tumeweza kupata uanachama huu, hongera sana Mhe. Waziri umetekeleza vyema ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kuleta maendeleo haya ambayo tumeyapata.

Mhe. Naibu Spika, nije katika suala zima ambalo tunajivunia. Lakini baada ya kupata uanachama huu Mhe. Naibu Spika, nitoe ushauri wangu na nasaha zangu kwa serikali kupitia wizara husika, ili kuweza kufaidika na kuweza kupata zile fursa ambayo tumeipata kwa kuleta maendeleo ya mchezo wetu huu kwa nchi yetu na taifa kwa ujumla na niishauri wizara Mhe. Waziri kwa sababu nafasi hii tulioipata ni kubwa na tutakuwa tunashiriki katika mashindano mbali mbali ya kitaifa kwa timu yetu ya Taifa *Zanzibar Heroes*, timu ya Vijana, pia timu yetu ya Taifa ya Wanawake. Mashindano haya ya kushiriki katika mashindano ya Afrika ni mashindano makubwa yana gharama kubwa. Sasa ni vyema tukajipanga tukafanya mikakati ya muda mfupi na muda mrefu ili ule uanachama wetu tulioupata tuweze kuutumia vyema kwa kuinua soka la Zanzibar na Tanzania wa ujumla.

Sasa ni vyema tukaunda kamati ya kuchangisha fedha kwa ajili kuendeleza soka letu na kuiandaa Timu yetu ya Taifa katika mashindano makubwa yanayokuja ya *AFCON*. Mhe. Waziri mashindano ya *AFCON* ni mashindano makubwa na mashindano vile vile ya Vijana ni mashindano makubwa ambayo sasa timu yetu ya Taifa ya Vijana *Serengeti Boys* imefanya vizuri katika mashindano haya na inaendelea kufanya vizuri na nichukuwe fursa hii kuipongeza sana Timu yetu ya Vijana ya Tanzania *Serengeti Boys* ambayo Wazanzibari wamo katika timu hii haya ni mafanikio makubwa hizo zote ni juhudi za viongozi wetu na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sababu vijana ambao wanashiriki katika mashindano yale Wazanzibari wamo.

Ni mashindano ambayo kwa kweli ni gharama kubwa kwa hiyo Mhe. Waziri nikuombe nikushauri ujipange mapema wako wanamichezo wako wananchi ambao wana uchungu mapenzi na nchi yetu. Wako matajiri wana mapenzi na uchungu na mapenzi ya nchi yetu, wapo viongozi ambao tuliowachagua ambao wanamapenzi na nchi yetu. Kwa hivyo, tujipange mapema ili kuhakikisha kwamba huko tunakokwenda tunafanikiwa.

Mhe. Waziri, kazi ambayo unayoifanya katika serikali katika kuinua sekta ya michezo ni kazi kubwa na ndio nikatanguliza kumpongeza Mhe. Rais pamoja na Waziri wetu katika ujenzi wa Uwanja wa *Mao Tse Tung* ni mafanikio makubwa na ahadi ambayo imo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mhe. Naibu Spika, Uwanja wa *Mao Tse Tung* wananchi wanasuburi kwa hamu katika kuuona uwanja ule unarudi katika enzi zake za zamani na kuleta haiba kuwa ya mji wetu. Lakini nimuombe Mhe. Waziri kuhakikishwa kwamba ujenzi ule unakwenda na wakati kwa sababu tulitegemea uwanja ule utaanza ujenzi katika mwezi wa Januari lakini umechelewa na ni vyema akatueleza

Mhe. Waziri atakapokuja ni sababu gani ambao uwanja ule ulichelewa hadi kufikia leo ambao umeanza shughuli ile ya ujenzi.

Lakini vile vile nimuombe Mhe. Waziri kwamba kuwe na ushirikiano na majirani katika maeneo yale zile huduma ambazo zinapatikana katika maeneo yale hususan huduma za maji basi ni vyema majirani katika maeneo yale yakawa yale maji ambayo yamefikishwa pale basi wananchi pia wanapata katika maeneo yale. Vile vile ajira ambazo wananchi wanaweza kupata basi ni vyema vijana wetu waweze kupata ajira katika kujenga uwanja ule.

Lakini mbali na hayo Mhe. Naibu Spika, tuna viwanja vyetu vya Mnazi Mmoja mbavyo zimo katika Jimbo pia la Kikwajuni. Viwanja vya Mnazi Mmoja ndio chimbuko la kuibua vipaji kwa vijana wetu, lakini hali ya viwanja vile sote tunaijua lakini juhudi kubwa ya serikali yetu kupitia Rais wetu Dr. Ali Mohd Shein kufanya miundo mbinu ya kuyatoa maji katika maeneo yale kwa kweli wamefanikia katika asilimia 80, hali ya uwanja sasa hivi angalau inaridhisha na mvua zote ambazo zimenyesha katika kipindi hichi basi athari ambayo tulikuwa tumezoa huko nyuma sasa hivi imepungua kwa kiasi kikubwa hongera Dr. Ali Mohammed Shein. (*Makofi*)

Mhe. Waziri lakini mbali na juhudi zile nimuombe sana Mhe. Waziri ili kuweza kufanya mikakati ya kuvirejesha viwanja vile katika hali ya zamani ilivyokuwa tunavitumia vilabu vyetu pale na bahati nzuri Katibu wako Mkuu ni mwanamichezo na ambaye amevitumia viwanja vile wakati enzi zake na sote tunamjua Katibu Mkuu alikuwa mwanamichezo mahiri ameonesha umahiri wake katika enzi zake wakati akiwa club ya *Small Simba* na nina imani atakuwa na uchungu na mapenzi kuhakikisha viwanja vile vinarudi katika hali yake.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuondoka hapo nije katika sekta hii ya habari. Mhe. Naibu Spika, mimi nichukuwe fursa hii kuupongeza uongozi mzima wa wizara hii. Lakini vile vile wakurugenzi wa *ZBC Redio* na *ZBC TV* kazi kubwa wameifanya, lazima ni wajibu wetu kufanya yale mazuri tuliyoyasema ni lazima tuseme, kwa kuweza kuboresha *ZBCTV* na kuweza kuweka miundombinu mpya ili wananchi tuweze kupata vitu vizuri kutoka katika televisheni yetu na *ZBC Redio*.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu wametangulia kusema hapa Mhe. Suleiman Sarahan amesema sana kuhusiana na hali halisi ya waandishi wetu wa habari na mimi niunge mkono, ili waandishi wetu hawa wawe ni kioo kizuri kwa jamii

wakati wakiwa katika kazi zao, ili kuona kwamba basi na sisi tunafikia kule tunakotaka.

Mhe. Naibu Spika, mbali na hayo, lakini Mhe. Hidaya Ali hapa kasema basi tuendane angalau kuutunza utamaduni wetu, ni vyema haya na sisi tuyaunge mkono kwa pamoja ili kuhakikisha kwamba *ZBC* inafika kule tunakotaka.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo nizungumzie suala zima la programu ndogo ambayo ni uimarishaji wa utamaduni wa maeneo ya historia. Mhe. Naibu Spika, programu hii ambayo hapa tumeelezwa kwamba katika Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni wa Baraza la Sanaa na Idara ya Kiswahili ya Makumbusho ya mambo ya kale, katika programu hii ilikuwa ikusanye jumla ya shilingi milioni 392,268,000, lakini fedha ambazo zimekusanywa ni milioni 170,110,202 tu ambayo inaonesha takriban ni asilimia 40. Ni vyema Mhe. Waziri atakapokuja atueleze ni sababu gani iliyofanya makusanyo hayo yawe madogo.

Mhe. Naibu Spika, mimi niombe kusema kwamba hii pia inatokana kwa sababu tunategemea wasanii, tunawasifu wasanii na kwa kweli wasanii ni watu ambao wanaelimisha jamii na wanapata ajira. Kwa hivyo, ni vyema tukawaenzi na tukawaunga mkoni ili kuweza kuendeleza zaidi vipaji vyao na vile vile serikali yetu kuweza kupata pato kwa kupitia wasanii. Mhe. Waziri niombe tuwaunge mkono wasanii wetu na tusiwavunje moyo wasanii wetu, pale ambapo panahitajiwa busawa na hekma nadhani ni vyema pakatumika busara na hekima ili kuweza kuwaunga mkono wasanii wetu kuweza kupata ajira na kuweza kupata pato la taifa sio kuwakandamiza na kuwaumiza katika maeneo mengine.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nimalizie kwa kusema kwamba kazi tuliyonayo ni pevu, tusivunjike moyo sisi tumechaguliwa na wananchi, wana imani na sisi kwa kupitia Rais wetu wawakilishi, wabunge ambao wana imani na wawakilishi na viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi, na Chama cha Mapinduzi ndio chama ambacho kinaleta maendeleo katika nchi hii. Viongozi wa Chama cha Mapinduzi ndio ambao wataleta maendeleo katika nchi yetu. Kwa hivyo, niwaombe sana wawakilishi wenzangu na viongozi wenzangu tuiunge mkono bajeti hii ili kuleta maendeleo kwa nchi yetu kwa faida yetu sisi na vizazi vijavyo. Pale ambao pana kasoro tukosowe lakini tuiunge mkono bajeti hii kwa faida ya nchi yetu, faida yetu sisi na vizazi vijavyo.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, kwa sababu leo nimesema awali sitaki kusema sana. Kama nilivyotangulia kusema kwamba mcheza kwao hutunzwa, hongera sana Mhe. Waziri nakutakia kila la heri, tujipange zaidi na

nina imani na wewe huko tunakokwenda mambo yatakuwa mazuri zaidi. Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema haya naunga mkono kwa asilimia 200.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Nassor Salim Ali Jazira. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa muda ambao tulionao atakuwa Mhe. Mohammed Said Dimwa. Mhe. Mohammed karibu.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe.Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kuniona, lakini leo angalau nimepata dakika kadhaa nimekuwa mzee wa dakika tano kila siku. Mhe. Naibu Spika, nikupongeze wewe kwanza kwa kuniona, lakini nimpongeze sana Mhe. Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya, lakini na majibu yao ambayo wanatujibu ya ufasaha.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana Katibu Mkuu, lakini vile vile na watendaji wake kwa kazi kubwa ya kutuhabarisha na kutupa kila aina ya habari ambayo tunaitaka.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze moja kwa moja kuipongeza sana kamati yetu. Kamati imefanyakazi kubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kukupongeza sana pamoja na kamati yako *you did well. (Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Shirika la Utangazaji *ZBC* kwanza nichukuwe fursa hii kuwapongeza sana, nimpongeze sana Mkurugenzi wa *ZBC TV* amefanya kazi kubwa kuibadilisha TV yetu kimuonekano. *(Makofi)*

Kimuonekano tunaonekana sasa tumeanza kubadilika, na hiyo ndiyo dhamira yetu kubwa sana, lakini Mhe. Mwenyekiti pamoja na pongezi ambazo nimempa bado kuna matatizo madogo madogo. Juzi wakati tunaangalia Baraza la Wawakilishi kuna matangazo yamekatika, lakini hata kuomba radhi TV hii imeshindwa, tunamuomba sana makosa haya mpaka leo hayajaombwa radhi kwa sababu gani, wananchi wanapata tabu tuombe tu likitokea suala hili tuwaambie tatizo, lakini ni kitu gani wamefanya ili basi wananchi waridhike.

Lakini jengine nataka kujua niliona kwenye habari mbali mbali, tumetoka sasa kwenye *analogue* tunaingia kwenye *digital.* Je, tumeingia lakini tumefikia wapi. Mwaka jana nilisema na nilikamata fungu, lakini safari hii nina nia kubwa sana ya kuchukua hapa fungu hili. Mhe. Naibu Spika, naomba kutangaza hadharani kwamba nina nia kubwa ya kuchungua fungu hili, kwa sababu nataka kujua tumeingia au hatujaingia, tumebaki kwenye karne ya 21 au tumerudi karne ya 10.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye *ZBC Redio*. Nilikuwepo Pemba hivi karibuni, lakini nimeona bado hazisikiki vizuri sijui kuna tatizo gani, wakati mwengine mpaka upande kwenye mti ndio uweze kupata redio yako vizuri. Sasa hili linatisha sana au uweke tayari uanze kutega ndio uweze kupata kusikia Redio Zanzibar. Nawaomba sana wajitahidi kuweza kupata Redio Zanzibar ambayo ndio Redio yetu tunayosikiliza habari za vifo sio chengine. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, *ZMUX*. Ving'amuzi hivi kwanza nataka nijuwe vile ving'amuzi tata vya miaka mingi vimefika havijafika na vina ubora gani tuweze kujua. Lakini nimeona huku katika mchango ambao umechangiwa kuingia kwenye hazina ni milioni 250, ikiwa kweli tuna nina safi sana basi mchango wao huu ni mdogo sana, lakini nielezwe kazi zake ni kazi gani, na hili shirika liko vipi linajitegemea au liko ndani ya wizara na hii hapa nitataka kujua Mhe. Waziri uniambie mimi nataka nipendekeze sana angalau basi isiwe milioni 250, tuweke milioni 300 ndio mchango wake ambao unaweza kutuongezea. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye Shirika la Magazeti ya Serikali. Nilipongeze sana shirika hili kwa muono mzuri sana ambao uko sasa, tumeanza kugeuka. Mimi nataka kusema tena tumeanza kugeuka, tulikuwa heading yetu tulikuwa tunaitoa pale mbele Zanzibar Leo, lakini sasa hivi tumeiweka pembeni, kila tunaposoma linaanza kutupa raha kweli kweli. Kw ahivyo nimpongeze sana mhariri mkuu wa gazeti hili kwa vionjo vyake vingi anavyovianza.

Lakini Mhe. Naibu Spika, tulianza kuona gazeti hili tukiwa kwenye amsha amsha, ikiwa amsha ya *ZBC Redio*, lakini vile vile kwenye vituo vya televisheni mbali mbali, kama vile *Channel Ten, ITV* na *TBC* tulikuwa tukiona vikiamshwa kwenye gazeti hili, lakini sasa haliamshwi. Lakini niliuliza kwa nini haliamshwi, nikaambiwa gazeti lile sasa linachapishwa Zanzibar. Nataka niwapongeze sana wachapishaji wa Zanzibar, nataka nikipongeze sana kiwanda chetu cha uchapaji, lakini Mhe. Naibu Spika, gazeti lile tulipokuwa tukilichapisha Bara tulikuwa tunalichapisha kwa shilingi 300 na sisi tulikuwa tunauza gazeti lile shilingi 500, kwa hivyo faida yetu ilikuwa shilingi 200. Lakini pale pale kulikuwa na wasambazaji wa gazeti lile saa 4:00 limekwisha kuchapishwa linafika Mwanza, Dodoma, na sehemu mbali mbali. Cha ajabu ninachokiona sasa hivi hakifiki, lakini tukilichapisha Zanzibar tunalichapisha kwa shilingi 600, maana yake sisi tuna mapungufu ya shilingi 100. Sasa hii sio biashara na tunakwenda katika vyombo vya kibiashara na tunakwenda katika vyombo vya kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, kasoro nyengine ambayo tuliyokuwanayo *Media Council Report* imetuambia ya mwaka jana kuwa gazeti hili ndio la tatu katika kusomwa Tanzania. Sasa leo tunaanza kurudi *reverse* inakuwaje. Nataka Mhe. Waziri hapa aniambie kwa kirefu tu imekuaje na nina nia hasa ya fungu hili kuliondoa mpaka niweze kujua hizi kasoro ambazo zipo. Lakini jengine gazeti lile limekua sasa hivi haliendi Bara, wasomaji wa Unguja kidogo, lakini faida kubwa ambayo tumeipata kwa Unguja sasa hivi tunapata kulifungia samaki kwa urahisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja, nimesema kuna deni kubwa ambalo tumeona linadaiwa. Mhe. Waziri atueleze ni mikakati gani serikali imefanya kulilipa deni hili kwa Shirika la Magazeti kule Bara, lakini na madeni ambayo shirika hili linada kwa taasisi na mawizara ya serikali tuambiwe ina mkakati gani wa kuweza kuzipata pesa hizi.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu kule Dk. Jonh Pombe Magufuli alisema kata, maana kila pahala ukate mpaka Magereza wamekatiwa umeme. Sasa tufike pahala tuseme tusipeleke magazeti kama wizara yoyote haijatulipa, au wizara ya fedha ianze kuchukua basi kwenye *OC* mbali mbali za mawizara mbali mbali na mataasisi mbali mbali kuweza kulilipa gazeti hili ili tulione basi linakwenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, niingie kwenye Kamisheni ya Utalii, niwapongeze sana wamefanyakazi kubwa sana. Lakini nimeona huku maabara ya utalii imetengewa shilingi milioni 500, ni ndogo sana kwa utalii kwa sababu tuna kazi kubwa sana. Kazi ya kwanza ni kuweza kuutangaza utalii kikamilifu, na utalii huu tumeangalia kwenye kitabu chao, wanasema wamelipia mabanda Dubai na Ujerumani ni lazima tuutangaze utalii, kwa sababu utalii ndio uti wetu wa mgongo wala sio kilimo mimi nataka kusema, kwa sababu wanatuchangia pesa nyingi. Nimeona katika mchango wao wametuchangia bilioni 4 katika serikali kwa mwaka. Sasa kwa nini tusitumie pesa nyingi kwa kuweza kuingia kwenye maabara yetu lakini tukaibuka na kitu tukasema utalii sasa unatunufaisha.

Mhe. Hussein Ibrahim Bhaa amesema watalii wote wanaokuja hapa wanasema kisiwa hiki hatutaki kuondoka. Sasa tufanye utalii wa ndani, tufanye utalii wa nje, lakini umefika wakati tutangaze hata kwenye *CNN*, tuwape pesa nyingi ili watangaze. Tukipata kutangaza tunaweza tukaingiza pesa nyingi, tukubali kupoteza pesa lakini tuingize fedha.

Mhe. Naibu Spika, tutangaze sana na utalii wa ndani, wajumbe wenzangu wengi wamesema kuna sehemu mbali mbali za kihistoria, huku wamesema kwenye kitabu chao watakwenda kwa Bihole na kwengine ili kuweza kuimarisha, tutangaze sana. Sasa hivi hata vijana wetu hawajui pengine hata sehemu za kihistoria. Sasa tushajihishe utalii wa ndani kila Jumamosi na Jumapili, angalau watu waende kule na tuweke basi kiingilio kidogo.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Idara ya Utamaduni na Michezo. Nimpe pongezi sana Mkurugenzi huyu wa Idara hii, kwa kazi nzuri ambazo ameanza kuzifanya. Sio kuwa ameanza kuzifanya tu kwenye wizara yake, lakini hata maskuli kule tunaona sasa tunaanza kushusha michezo kule, tunarudi kama zile enzi za kina Kirova walicheza kule skuli, lakini ndipo tunapopata vipaji vingi.

Mhe. Naibu Spika, tumesema tuna mpango wa kujenga viwanja mbali mbali vya wilaya, niwapongeze sana kwa hatua hii na kwa sababu watatanua wigo mkubwa sana kuweza kujenga viwanja vile. Lakini kubwa zaidi vipaumbele ambavyo wameviweka vingi, kwanza tumalize na Uwanja wa Mao Tse Tung, tukiuanza ule ndio tutaanza kwenda kila wilaya sasa.

Mhe. Naibu Spika, niseme tu pongezi kwa kupata uwanachama wa *CAF*, lakini sasa tuanze kujipanga *ZFA* ile ya mazowea sasa hivi tuanze kuondoka nayo, tuwe na *ZFA* yenye viongozi wataalamu, tusiwe na *ZFA* ile ya migogoro isiyokwisha, lakini *ZFA* ile ambayo ni kimeo tuachane na hayo. Nasema sote kwa umoja wetu tuweze kubadilika kuweza kuiendeleza michezo.

Mhe. Naibu Spika, kuandaa timu za vijana. Mhe. Nassor Salim Ali Al-Jazira sasa hivi amesema kwamba tunauona umuhimu wa kuandaa timu ya vijana Serengeti Boys, sote tumefarajika, sote tunawashangiria Serengeti Boys lakini imeandaliwa, kuandaliwa vipi. Imeandaliwa imezunguka nchi mbali mbali, kuandaa timu hizi inataka moyo sana. Sasa niwaombe sana tunakwenda kwenye *CAF* lakini tuwe na mipango imara tuweze kuoneshwa, mipango hii serikali imejipanga kuweza kuzitayarisha timu zetu.

Mhe. Naibu Spika, leo tulikuwa tunaandaa timu yetu ya *Zanzibar Queen. Zanzibar Queen* ilikuwa ikifungwa magoli sio mengi, angalau tu magoli 11, 7, 5 haiwezekani, tujitahidi sana kuweza kuandaa timu yetu. Lakini Mhe. Naibu Spika, nije kwenye Uwanja wa Amani, uwanja huu ulikuwa una vyoo mbali mbali ambavyo wakandarasi wale walipojenga walitumia mipango mingi kuweka vyoo, lakini vyoo vile sasa hivi vimegeuzwa kuwa ofisi. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri akija aniambie ana utaratibu gani, kwa sababu

hata makamanda wetu kwenye paredi ile huwa wanavitumia vile, lakini leo vimeachwa kutengenezwa na kuwa ofisi, ubora wake uko wapi, nataka kujua

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, umebakiza dakika mbili.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe.Naibu Spika, zinanitosha sana hizo. Nasema niingie kwenye Baraza la Michezo. Niseme huku Baraza la Michezo kuna nini, mbona michezo yote kama bao, baskeli, karata, iko chini. Mhe. Waziri uje utuambie Bazara la Micheo lina nini na mipango yake ni ipi Baraza la Michezo kuweza kuimarisha michezo yetu hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii sana nikupongeze leo angalau kwa kuniachia dakika 15, sio tano ulizozowea. Nikushukuru sana na nawashukuru wote. Siungi mkono hoja hii hata moja. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mohammed Said Dimwa. Waheshimiwa Wajumbe, bado tuna wachangiaji na wachangiaji hao tunatarajia sana kwamba watachangia siku ya Jumatatu asubuhi. Niwataje watakaochangia Jumatatu asubuhi ambao ni Mhe. Ali Salum Haji, Mhe. Machano Othman Said, Mhe. Ahmada Yahya, Mhe. Miraji Khamis, na Mhe. Mgeni Hassan Juma. *(Makofi)*

Pamoja na hao watachangia mawaziri Mhe. Said Soud Said, pamoja na Mhe. Salama Aboud. Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kumaliza nina tangazo. Mhe. Machano nimekutaja. Nimesema Mhe. Machano Othman.

Mhe. Machano Othman Said: Ni Machano Othman Said. Wewe umesema Machano Othman Masoud.

Mhe. Naibu Spika: Samahani sana Mhe. Machano. Ulimi umeteleza. Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kumaliza, nina tangazo moja linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, anaomba baada tu ya kumaliza kikao hiki, basi mkutane. Amesema mkutane tu hajasema sehemu gani. Kwa hivyo, nafikiri mtakutana hapo nje labda kuna mazungumzo madogo.

Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru sana kwa siku ya leo nafahamu kwamba tulikuwa na majukumu mengine, lakini bado tumeweza kutenga kuja hapa na kuendelea na shughuli yetu hii ya leo. Niwashukuru sana na niwapongeze wale wote ambao wamechangia. Sasa natangaza kwamba nimeakhirisha shughuli hii yetu ya leo mpaka Jumatatu tukijaaliwa saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 8:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 22/05/2017 saa 3:00 asubuhi)